# UHAKIKI WA RIWAYA YA *NYUSO ZA MWANAMKE* NA SAID AHMED MOHAMED: MTAZAMO WA SAIKOLOJIA CHANGANUZI

NA

MUKHATA CHRISPINUS WANYONYI

C50 / 75742 /2009

IDARA YA ISIMU NA LUGHA

University of NAIROBI Library
0370535 7

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA *MASTER OF ARTS* KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI

JULAI, 2011

## IKIRARI

"Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine cho chote."

..........................................

**MUKHATA CHRISPINUS WANYONYI**

(Mtahiniwa)

"Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii tulioteuliwa na chuo kikuu."

.................................................... ..........8/11/2011..........

SAHIHI TAREHE

**DKT. TOM OLALI**

.................................................... NA ....10-11-2011....

SAHIHI TAREHE

**DKT. ZAJA OMBOGA**

## TABARUKU

Tasnifu hii nawatabarukia mke wangu mpendwa Emily Nasimiyu, watoto wangu Hannah Nafula, Enock Juma, Timothy na Elisha ambao walistahimili wakati wote waliponikosa na kunipa motisha niendelee na masomo yangu. Walinikosa sana lakini walielewa na kunihimiza hadi mwisho.

Shukrani za kipekee kwa mke wangu aliyechukua jukumu la kuwalea watoto wakati wote huo nilipokuwa ninaendelea na masomo yangu.

Siwezi kuwasahau wazazi wangu hasa mama yangu Teresina Adhiambo na marehemu baba yangu walioniwekea msingi wa masomo. Shukrani sana.

# SHUKRANI

Ninakiri kwamba kazi hii haingekamilika bila ya usaidizi wa namna mbalimbali. Kwanza, natoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu Dkt. Tom Olali na Dkt. Zaja Omboga walionipa mwelekeo kwa mashauri yao yaliyonifaa sana. Mapendekezo na mwongozo walionipa, hasa kuhusu jinsi ya kuipanga kazi ya kitalaamu, ndio ulionisaidia kuiandika na kuipiga msasa kazi hii ikawa vile ilivyo sasa. Nitawakumbuka maishani mwangu kwa kazi yao.

Shukrani zangu pia ziwaendee wahadhiri walionifunza katika Idhara ya Isimu na Lugha: Prof. Abdulaziz, Prof. John Habwe, Dkt. Mwenda Mbatiah, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Kineene wa Mutiso, Dkt. Ayub Mukhwana, Dkt. Tom Olali, Dkt. Alfred Buregeya na Bw. Mungania. Hawa ndio walioniwekea msingi wa awali wa kazi hii.

Siwasahau wanafunzi wenzangu Bw. Mulama Shitemi, Bw. Warambo John Paul, Bi. Martha Owino, Bw.Kamotho Mwiruri, Jacob Maobe, Bw. Mirikau Suleiman na Bw. Okombo Lukwiri. Ukurubiano na ushirikiano wangu nao hasa katika mijadala ya kiusomi ulisaidia kunihimiza na kunipa changamoto kupevuka na kuendeleza kazi hii. Nawashukuru sana kwa ushirikiano wenu ambao bila kuwa nao ingeniwia vigumu na ningekuwa na upweke mwingi sana.

Singependa kuwasahau walimu katika shule yangu walionipa msaada wakati wa masomo yangu. Msaada wao hasa wa tafiti za hapa na pale ulinisaidia kufanya baadhi ya masomo. Wao ni Julias Wandabusi, Janetrix Makokha, Alice iteke na Bw. Simwenyi Musungu. Hongera kwa kunipa moyo wa kuendelea na masomo yangu.

Ndugu yangu Bw. Charles Mukhata alinifaa sana kwa kunitia moyo na kunipa msaada wa kifedha. Mbali na hayo, alinishauri kama baba na kunihimiza niendelee na masomo yangu. Asante sana kwa mazuri uliyonitendea.

Sitamsahau mke wangu mpenzi, Emily aliyekuwa mshirika wa karibu na kunikubalia kuendelea licha ya muda mrefu niliochukua kukamilisha tasnifu hii. Alihakikisha kuwa ninaishi maisha mazuri katika mazingira yafaayo. Nawashukuru watoto wangu Enock na Hannah walionielewa na kukubali kutengana nami kwa muda wote niliochukua kumaliza kazi hii kwani bila kuvumilia kwao ingekuwa shida sana kukamilisha kazi hii. Nyote Mungu awabariki.

Nawashukuru marafiki na jamaa ambao walipojua ninaendelea na masomo walinitia moyo na kunihimiza kuendelea. Hawa ni Bw. Vincent Khisa, Benjamin Wamalwa, Godfrey Masika, Godrick Simwenyi na Jesca Wabuyube. Nasema asante sana.

Hawa wote niliowataja na wengine ambao sikuwataja nawashukuru kwa msaada wenu wa kipekee. Na mwisho, namshukuru Mungu kwa mapenzi yake yaliyoniwezesha kufikia kiwango hiki.

ASANTE SANA

## UFUPISHO

k. h. j - kama hapo juu

mh. - mhariri

na. - namba

n. w. - na wenzake

tol. - toleo

uk. - ukurasa

## MUHTASARI


Tasnifu hii inahusu uhakiki wa riwaya ya *Nyuso za mwanamke* (2010) ya Saidi Ahmed Mohamed kwa mtazamo wa saikolojia changanuzi. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kuonyesha, kuchanganua na kubainisha mitagusano inayoibuka katika jamii iliyosawiriwa katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* na athari zake kwa wahusika. Ili kuthibitisha hili tulilenga kubainisha mbinu za usukaji wa matukio yenye mwelekeo wa kisaikolojia. Pia, tulidhamiria kuonyesha jinsi mwandishi alikusudia kuwasawiri wahusika ili kudokeza msukumo wa matendo yao na hali zao za kisaikolojia. Aidha, tulilenga kuonyesha riwaya hii kama riwaya ya kisaikolojia mbali na kubainisha maendelelo ya riwaya ya kisaikolojia katika kitengo cha kimaudhui, kiutanzu, kihusika, kimsuko na kimtindo. Madhumuni haya yote yalidhamiria kuchangia uelewa wa kazi za kifasihi hususani riwaya ya Kiswahili kwa ujumla wake.

Katika utafiti wetu tuliongozwa na nadharia tete tatu. Kwanza, tulitaka kubainisha kama riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* inaweza kuainishwa kama riwaya ya kisaikolojia. Pili, kama riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* inaonyesha ukamilifu katika kipengele cha umbuji wa wahusika kati ya vipengele vingine vya riwaya ya kisaikolojia. Na tatu, kama mtindo si nyenzo kuu ya kuiunda kisanii riwaya ya *Nyuso za mwanamke* kama riwaya ya kisaikolojia. Kati ya nadharia tete hizi tatu nadharia mbili za mwanzo zilitimilika vizuri huku tukipata kuwa mtindo ni nyenzo kuu katika kuiunda riwaya hii kisanii kama kazi ya kisaikolojia.

Utafiti huu ulikuwa wa maktabani. Tulidurusu riwaya husika na kazi nyingine za wataalamu wa fasihi hasa fasihi ya Kiswahili kwa undani. Pia, tulirejelea riwaya nyingine za kisaikolojia za Kiswahili ili tupate wasifu wa riwaya ya kisaikolojia vizuri. Kwa maoni yetu, ingekuwa vyema kama utafiti huu ungehusisha udurusu wa shajara za mwandishi huyu pamoja na kuwahoji watu walio karibu naye ili kujua maisha yake. Kufanya hivi kungetuwezesha kuchanganua saikolojia

yake ipasavyo.

Katika utafiti huu nadharia ya saikolojia changanuzi ilitufaa sana. Ilitufaa katika uchanganuzi wa muundo na wasifu wa ploti, umbuji wa wahusika na mtindo wa usanii wa kazi husika. Ilitufaa pia kuonyesha maudhui kama motifu inayojitokeza katika kazi hii na kazi zake za awali pamoja na kuonyesha kuwa maudhui haya ni akisi ya uhalisi ulio dhahiri katika jamii iliyosawiriwa. Hata hivyo, nadharia hii inajikita sana katika kusawiri hali za kisaikolojia za wahusika na mwandishi na kwa hivyo inawafanya waonekane kama watu walio na matatizo ya kisaikolojia. Mbali na hayo, inao udhaifu wa kuiona kazi ya kifasihi kama ndoto na kwa maana hiyo huenda wasomaji wakaichukulia hivyo na kuipuzilia mbali kama isiyo na mashiko na uhalisi.

Mbali na kuwa riwaya ya kisaikolojia haina historia ndefu imeonyesha ukuaji mkubwa sana. Kwa maoni yetu kilele cha ukuaji huo ni riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke***. Kwanza, matukio katika riwaya hii yamesukwa kwa ufundi mkubwa na uchangamano kwa mbinu za kisaikolojia kwa lengo la kuonyesha uhusiano kati ya matukio hayo na hali za kisaikolojia za wahusika. Mbinu hizi ni kama uzungumzinafsi ndani, dayolojia ya ndani, mkondo wa ung'amuzi, mbinu rejeshi, barua, ndoto na nyimbo. Wahusika wengi wamesawiriwa kisaikolojia kwa lengo la kudokeza hali zao za ndani na wanaonyesha mwelekeo mkubwa wa ubanaji, uhawilisho, uhusishi na ubadilishaji kama inavyojitokeza katika wahusika Nana, Faisal na Bimkubwa. Maudhui yamejitokeza kama motifu katika kazi hii na kazi za awali pamoja na kuwa akisi ya uhalisi katika jamii husika. Mtindo umetumika kwa ufundi mkubwa katika vipengele vyote vya fani. Uhusika umewadokeza wahusika kisitiari na kiishara kama inavyoonekana katika wahusika Nana, Bimkubwa na Faisal. Lugha ya kitamathali imetumika kwa upana sana hasa maswali ya balagha, tasifida, ritifaa, taashira na ishara kwa uamilifu mkubwa wa kisaikolojia na kuchangia kukuza wasifu wa wahusika na maudhui. Mbinu za uwasilishaji mawazo, usimulizi, italiki na sintaksia yenye nyufa zinajitokeza kwa uwazi.

Mwisho, tumeiona riwaya hii kuwa ya kuvutia na kusisimua na yenye uchangamano pamoja na

kule kuweza kuibua masuala tata na nyeti katika jamii husika. Kupitia uchanganuzi wake, tumepata kuwa riwaya ya kisaikolojia ni riwaya ya kipekee katika taaluma ya fasihi. Upekee huu umejitokeza katika usawiri wa wahusika kisaikolojia kwa kutoa mawazo, fikira na hisia za ndani za wahusika. Riwaya hii pia imetumia mbinu tendati zinazoifanya iwe na miondoko ya tamthilia kama uzungumzinafsi ndani, dayolojia ya ndani, uwasilishaji halisi wa mawazo, uwasilishaji halisi huru wa mawazo na mkondo wa ung'amuzi. Kwa njia hii inaweza kunasa raghba ya msomaji yeyote.

## YALIYOMO

**Ukurasa**

IKIRARI................................................................i

TABARUKU................................................................ii

SHUKRANI................................................................iii

UFUPISHO WA MANENO................................................................v

MUHTASARI................................................................vi

YALIYOMO................................................................ix

**SURA YA KWANZA**................................................................1

**UTANGULIZI**................................................................1

1.1 Usuli wa mada................................................................1

1.2 Tatizo la utafiti................................................................6

1.3 Madhumuni ya utafiti................................................................9

1.4 Nadharia tete................................................................10

1.5 Sababu za kuchagua mada hii................................................................10

1.6 Mipaka na upeo................................................................11

1.7 Msingi wa nadharia................................................................12

1.8 Yaliyoandika kuhusu mada hii................................................................23

1.9 Mbinu za utafiti................................................................29

1.10 Tanbihi................................................................30

**SURA YA PILI**................................................................31

**MUUNDO NA WASIFU WA PLOTI KATIKA *NYUSO ZA MWANAMKE***................................................................31

2.1 Utangulizi................................................................31

2.2 ***Nyuso za Mwanamke*** kwa muhtasari................................................................31

2.3 Dhana ya nyuso za mwanamke....34

2.4 Mbinu za kisaikolojia za ujenzi wa ploti....39

2.4.1 Uzungumzinafsi....41

2.4.1.1 Uzungumzinafsi ndani....42

2.4.1.2 Dayolojia ya ndani....44

2.4.2 Mkondo wa ung'amuzi....45

2.4.3 Mbinu rejeshi....47

2.4.4 Nyimbo....49

2.4.5 Barua....53

2.4.6 Ndoto....55

2.5 Mbinu za usimulizi....57

2.5.1 Usimulizi wa nafsi ya kwanza....58

2.5.2 Usimulizi wa nafsi ya tatu....61

2.6 Hitimisho....63

2.7 Tanbihi....64

**SURA YA TATU**....65

**UMBUJI WA WAHUSIKA KISAIKOLOJIA**....65

3.1 Utangulizi....65

3.2 Uhusika na wahusika....65

3.3 Ujenzi wa wahusika kisaikolojia....67

3.3.1 Wahusika wakuu....68

3.3.1.1 Nana....69

3.3.1.2 Faisal....75

3.3.2 Wahusika wadogo....79

3.3.2.1 Bimkubwa ..... 79
3.3.2.2 Amour ..... 80
3.3.2.3 Bi. Mau ..... 81
3.3.2.4 Bi. Chuma ..... 82
3.3.2.5 Shemsa ..... 82
3.3.2.6 Bwana Hila ..... 83
3.3.2.7 Ngware ..... 85
3.4 Hitimisho ..... 85
3.5 Tanbihi ..... 87
**SURA YA NNE** ..... 88
**MAUDHUI** ..... 88
4.1 Utangulizi ..... 88
4.2 Tafsili ya maudhui ..... 88
4.3 Maudhui katika *Nyuso za Mwanamke* ..... 90
4.3.1 Utamaduni na itikadi ..... 90
4.3.2 Ukombozi wa mwanamke ..... 94
4.3.3 Mapenzi ..... 99
4.3.4 Usasa ..... 102
4.4 Hitimisho ..... 105
4.5 Tanbihi ..... 107
**SURA YA TANO** ..... 108
**MTINDO WA USANII WA *NYUSO ZA MWANAMKE*** ..... 108
5.1 Utangulizi ..... 108
5.2 Dhana ya mtindo ..... 108
5.2.1 Sintaksia yenye nyufa ..... 110
5.2.2 Italiki ..... 111

5.2.3 Lugha ya kitamathali ..... 112

5.2.3.1 Tasifida na miko ..... 113

5.2.3.2 Ishara na uashiriaji ..... 115

5.2.3.3 Ritifaa ..... 117

5.2.3.4 Maswali ya balagha ..... 119

5.2.4 Uwasilishaji wa mawazo kisaikolojia katika ***Nyuso za Mwanamke*** ..... 121

5.2.4.1 Uwasilishaji halisi wa mawazo ..... 121

5.2.4.2 Uwasilishaji taarifa wa mawazo ..... 122

5.2.4.3 Uwasilishaji halisi huru wa mawazo ..... 123

5.2.4.4 Uwasilishaji taarifa huru wa mawazo ..... 123

5.2.4.5 Ripoti ya usimulizi wa tendo la uwazaji ..... 124

5.3 Hitimisho ..... 125

5.4 Tanbihi ..... 127

**SURA YA SITA** ..... 128

**MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO** ..... 128

6.1 Utangulizi ..... 128

6.2 Utathmini wa nadharia ..... 128

6.3 Maoni kwa ujumla ..... 129

6.4 Mapendekezo ..... 132

6.5 Sherehe ..... 134

6.6 Marejeleo ..... 136

# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.1 Usuli wa mada

Riwaya ya kisaikolojia ni riwaya inayoweka msisitizo mkubwa kwenye uhusika wa ndani wa wahusika. Hii ni aina ya riwaya ambayo inaleta saikolojia katika kazi za kifasihi kwa kuhusisha kazi hizo na fikira za binadamu zinazodhihirishwa na hali za kisaikolojia za wahusika wanaopatikana katika kazi hizo.[1] Kimsingi, kazi hizi humwelekeza mhakiki kuchanganua aina tatu za fikira za mwanadamu; fikira za mwandishi, fikira za mhusika na fikira za msomaji.

Riwaya ya kisaikolojia ya kisasa inasemekana iliibuka mwishoni mwa karne ya kumi na tisa wakati wanariwaya hasa wa Ulaya walipobadili mkondo wa msisitizo kutoka matendo ya nje na hoja pana za kijamii na kulenga uchunguzi wa kindani wa wahusika binafsi.[2] Waasisi wa kitanzu hiki cha riwaya ni kama vile George Elliot, George Meredith, Henry James na Joseph Conrad. Baadhi ya riwaya za kisaikolojia zilizochapishwa mwanzoni kule Ulaya ni kama vile ***Portrait of a Lady*** **(1881)**, ***Lord Jim*** **(1900)**, ***Heart of Darkness*** **(1902)** *(Joseph Conrad)*, ***The Wings of a Dove*** **(1902)**, ***Ambassadors*** **(1903)**, ***The Golden Bowel*** **(1904)** *(Henry James)*. Riwaya hizi za mwanzo za kisaikolojia katika fasihi ya Ki-ulaya ingawa ziliandikwa kwa kuzingatia uhusika wa ndani wa wahusika, ziliandikwa tu kwa mtindo wa kimapokeo[2] tofauti na riwaya za kisaikolojia za kisasa zilizo na mbinu za riwaya mpya. Uhusika wa riwaya hizi ulisawiri hali za kisaikolojia za wahusika na namna walivyokumbwa na vita vya ndani kwa ndani hasa riwaya za Henry James. Istilahi riwaya mpya kwa mujibu wa Wamitila (2003a: 185) inarejelea aina ya riwaya iliyozuka Ufaransa katika miaka ya 1950 na inayoakisi matumizi ya mbinu za kiubunifu na hukiuka kaida za kijadi za uandishi wa riwaya. Kimsingi, kunatumika vifaa kama vile italiki, mistari, dondoo, wino mzito na herufi kubwa kwa njia isiyo ya kawaida. Kutokana na mchango wake, Henry James anaangaliwa kama baba wa riwaya ya kisaikolojia hasa kutokana na namna ambavyo riwaya zake zilivyoandikwa.

Riwaya za kisaikolojia za Kiswahili zinaakisi baadhi ya sifa za riwaya za kisaikolojia za Ulaya. Baadhi ya sifa hizi ni kama vile usawiri kisaikolojia wa mawazo na matukio ya wahusika, matumizi ya upenyezi na upekuzi katika usimulizi wa nafsi ya tatu na mkondo wa ung'amuzi. Katika misingi hiyo basi, riwaya kama vile ***Musaleo!*** (2004), ***Bina-Adamu***! (2002) za Wamitila na ***Tata za Asumini*** (1990), ***Babu Alipofufuka*** (2001) na ***Dunia Yao*** (2006) za Said Ahmed Mohamed zinaweza kuangaliwa kama riwaya za mwanzo za kisaikolojia katika fasihi ya Kiswahili. Riwaya ya fasihi ya Kiswahili ambayo inaweza kusemwa kuwa ni riwaya ya mwanzo ya kisaikolojia ni ***Tata za Asumini.*** Ingawa inao muundo wa kimapokeo wa kuwasilisha mambo kwa njia ya moja kwa moja, inamsawiri mhusika Asumini ambaye anatatizika kimawazo na kihisia. Riwaya hizi nyingine zimekiuka kaida kwa kutumia mbinu kama vile uhalisiajabu, italiki, wino mzito, sintaksia yenye nyufa, wahusika ambao ni mizuka na kadhalika. Kazi hizi zinajitokeza kwa uwazi zaidi kama riwaya za kisaikolojia lakini hii haina maana kuwa hizi ndizo tu riwaya za kisaikolojia zilizoko katika fasihi hii.

Riwaya ya kisaikolojia ya Kiswahili haina historia ndefu kama ilivyo riwaya ya kisaikolojia ya Ki-ulaya. Riwaya ya kisaikolojia ya Kiswahili imeibuka mwishoni mwa karne ya ishirini. Tunaichukulia riwaya ya kwanza ya kisaikolojia ya Kiswahili kuwa ***Tata za Asumini*** (1990) ya Said Ahmed kama tulivyotaja hapo juu. Riwaya hii inamsawiri mhusika Asumini kama mhusika anayesumbuka ndani kwa ndani kutokana na malezi ya kudhibitiwa kwa sheria kali hasa kwa kuhofiwa kuchafuliwa na wanaume. Msuko wa riwaya hii umejengwa kwa matumizi ya uzungumzinafsi ndani, ndoto na mkondo wa ung'amuzi. Kimtindo riwaya hii imeandikwa kwa mtindo wa kimapokeo wa kusimulia matukio kwa njia ya moja kwa moja. Sifa za riwaya hii ndizo zinazorejelewa na Frye n.w. (1985: 377-378) kwa kudai kuwa riwaya hii hulenga saikolojia ya wahusika huku ikiweka msisitizo mkubwa kwenye maisha yao ya kindani kinyume na matukio ya nje yanayozungumziwa. Wanachosema ni kuwa riwaya hizi hudokeza hali za kimawazo na kihisia za wahusika zilizohodhiwa katika ung'amuzibwete[3] wao. Wamitila (2003a:298) anaeleza ung'amuzibwete kama sehemu ya akili ya mtu inayohifadhi fikira, mawazo, hofu na mitazamo hasi isiyokubalika na jamii yake. Katika riwaya hii, kama wanavyodai Frye na wenzake, msanii hana hamu sana na kilichotokea bali kwa nini

kilitokea na athari zake kwa hisia za ndani za binadamu anayehusika. Aidha, wanaongeza kuwa katika riwaya hizi, hutumika mbinu kama vile uzungumzinafsi ndani, dondoo, matumizi ya mistari, herufi kubwa, italiki, herufi nzito, matumizi ya nafsi ya kwanza na ndoto kwa njia isiyo ya kawaida. Matumizi ya mbinu hizi hasa uzungumzinafsi ndani, usimulizi nafsia na ndoto husaidia kujua hisia na fikira za ndani za wahusika.

Riwaya tunayoichukulia kama riwaya iliyoleta mapinduzi katika uandishi wa riwaya ya kisaikolojia kimuundo na kimtindo ni ***Babu Alipofufuka*** (2001). Imewasilishwa kwa mtindo wa riwaya mpya ambapo imetumia mbinu kama italiki, wino mzito, herufi kubwa, mistari, dondoo na uhalisiajabu kwa njia isiyo ya kawaida. Aidha, baadhi ya wahusika si binadamu wa kawaida bali ni mizuka kama mzuka wa Babu unaomwondoa mhusika K katika uhalisi wa maisha na kumrudisha alikotoka. Sehemu kubwa ya ploti yake inaendelea katika fikira za K. Mbinu za uzungumzinafsi ndani na dayolojia ya ndani ambazo zimetumika katika kazi hii zina mwelekeo mkubwa wa kisaikolojia. Kimaudhui, riwaya hii inadokeza maudhui ya utawala mbaya, ufisadi na uozo wa kimaadili. Riwaya hii imesawiri wahusika kisaikojia na kutumia mbinu za riwaya mpya ya Kiswahili ambazo hazibainiki katika riwaya ya ***Tata za Asumini.*** Katika riwaya hii kama anavyodai Lidell (1947:72) mpaka kati ya ploti na uhusika ni mwembamba sana kwa sababu si rahisi kubaini kwa mfano ni wakati gani uhusika wa K unasawiriwa na wakati gani matukio anamoshiriki yanadokezwa. Hata hivyo, kumewekwa msisitizo mkubwa kwenye ujenzi wa ploti kisaikolojia tofauti na ilivyo katika **Tata za Asumini.** Ni tofauti kama hizi ndizo tuliziona kama mapengo ya wazi katika maendeleo ya riwaya hii. Kama anavyodai Katie (2001: 367) mbinu za ujenzi wa ploti zinazodokeza hali ya kisaikolojia ya wahusika kama mkondo wa ung'amuzi zimetumika. Aidha, uzungumzinafsi ndani, ambao ni mbinu inayotumika kurejelea mjadala kati ya sauti bainifu na fikira za mhusika au kati ya fikira za mhusika umetumika pia.

Riwaya ya ***Bina-Adamu!*** (2002) inaweza kuangaliwa kama riwaya inayotoa picha ya kimawazo ya wahusika. Katika riwaya hii mhusika Bina-Adamu anapelekwa katika safari ya kisaikolojia kifikira ya kutambua hali za kijamii, kisiasa na kiuchumi zinazodhibitiwa_na ubepari wa mataifa yaliyoendelea. Hii ni

taswira iliyojijenga katika mhusika huyu anayewakilisha jamii ya mataifa ya ulimwengu wa tatu. Kwa mujibu wa Peck (1984: 120-121) msanii hufaulu kutokeza picha ya aina hii kwa kumruhusu mhusika kunena katika usimulizi wa nafsi ya kwanza kwa njia ya moja kwa moja. Anaongeza kuwa mhusika anaweza kudhihirisha hali yake ya kisaikolojia kwa kutumia usimulizi wa nafsi ya kwanza katika uzungumzinafsi ndani. Hii ndiyo mbinu inayojitokeza katika kazi hii. Kimtindo, riwaya hii inaonyesha namna ambavyo mwandishi anaweza kutumia usimulizi wa nafsi ya kwanza, uzungumzinafsi ndani na uhalisiajabu kuyadokeza masuala ya kawaida yanayowakumba binadamu katika jamii. Tofauti ya wazi kati ya riwaya hii na zilizotangulia ni namna ambavyo usimulizi wa nafsi ya kwanza umetumiwa kusawiri hali za kisaiokolojia za mhusika Bina-Adamu.

Riwaya ya ***Musaleo!*** (2004) inaweza kurejelewa kama kazi inayochunguza viwango mbalimbali vya kifikira vya wahusika. Kulingana na Shaw (1972:72) kunacho kiwango cha ung'amuzibwete ambapo mawazo na hisia zimebanwa na kiwango cha ung'amuzi ambapo mawazo na hisia zinatoka nje na kuonekana kwa njia ya mazungumzo na matendo. Kiwango kile cha kwanza ndicho kilichosheheni matukio ya kihisia na kifikira yanayoendelea ndani ya binadamu pasi na watu kuyaona ilhali kiwango cha pili kinacho matukio tunayoyashuhudia. Katika riwaya hii mwandishi anatudokezea yaliyo katika ung'amuzibwete wa wahusika kama vile Mukoko Wehu, Ngwena na Mzee hasa hali halisi ya kiutawala na kisiasa inayomkandamiza raia na kumnyima uhuru wa kujieleza. Kwa upande mwingine, kuna akina Anima, Zamda na Kitungule ambao usawiri wao unadokeza hali za ung'amuzi wao. Katika hali hii Mukoko Wehu anapozimia kwa kupewa sumu anasafari katika safari ya kisaikolojia na kujikuta pahali asipopaelewa. Ingawa kazi hii haidhihirishi sifa nyingi za kisaikolojia inadokeza saikolojia ya mwandishi na wahusika kwa njia ya kipekee.

Riwaya ya kisaikolojia ya ***Dunia Yao*** (2006) inaweza kuangaliwa kama kazi iliyosheheni ndoto za mchana na ndoto za kawaida za wahusika. Ndoto hizi huwa ni dhihirisho la hali zinazompitikia mhusika katika maisha yake hasa mambo yanayomtatiza na kwa hivyo kumwathiri kisaikolojia. Hali hizi humfanya akumbwe na mawazo chungu nzima yanayogeuka kuwa ndoto kama ndoto zinazomkumba Ndi. Hali ya Ndi

inatokana na kuchukizwa na mfumo wa ufisadi na utawala mbaya usiojali wanyonge, hali inayomfanya ajitenge na karamu zao. Kilele cha kujitenga huku ni pale anapotoa nguo katika karamu mojawapo. Kwa ujumla Ndi anaishi katika ulimwengu wake wa ndoto unaomtenga na jamii yake inayoporomoka kimaadili na kiuchumi. Hata hivyo ni ndoto zake zinazotufichulia mengi kuhusu uozo wa kimaadili, ufizadi na hali ya kisiasa katika nchi yake. Kimtindo, mwandishi ametumia ndoto, uzungumzinafsi ndani, mkondo wa ung'amuzi, baruapepe na uhalisiajabu kujenga ploti yake kwa njia ya kipekee. Kimaudhui riwaya hii inazungumzia maudhui mengi yakiwemo ufisadi, uozo wa kimaadili, malezi, nafasi ya mwanamke, umaskini na utawala mbaya. Kwa ujumla riwaya hii inaonyesha ukuaji mkubwa kimaudhui, kimtindo, kihusika na kimsuko ikilinganishwa na riwaya zilizotanguliwa.

Riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke*** (2010) ya Said Ahmed Mohamed ni kazi iliyosheheni uchangamano wa kimsuko, kihusika, kimtindo na kisimulizi. Kihusika, imesawiri wahusika, kama anavyodai Wamitila (2003a: 181), wanaosumbuka kimawazo kutokana na mitagusano wanayokumbana nayo kimawazo na wao wenyewe au na wahusika wengine na huathirika kisaikolojia. Hawa ni wahusika kama vile Nana, Faisal, Bimkubwa, Shemsa na Mwanamkuu. Hali hii ya kutatizika huku kwa wahusika kunatokana na kudhibitiwa na sheria na kaida za kijamii zinazowanyima uhuru wa kujiamulia hasa kuhusu masuala ya kiuana. Kimsuko, mwandishi ametumia mbinu anuwai kuijenga ploti yake. Mbinu hizi ni kama uzungumzinafsi ndani, mkondo wa ung'amuzi, barua, ndoto na nyimbo. Ni baadhi tu ya mbinu hizi zinazojitokeza katika kazi za awali tulizozirejelea. Kimaudhui, kazi hii inayadokeza karibu maudhui yote yanayokuzwa katika kazi za awali za kisaikolojia kama vile ndoa, malezi, utamaduni, uozo wa kimaadili, miundomsingi na nafasi ya mwanamke. Hata hivyo, namna ambavyo mwandishi anakuza maudhui hasa ya nafasi ya mwanamke yanaonyesha ukuaji mkubwa. Kwa mfano, katika kazi za awali wahusika wa kike wamepewa nafasi ya chini na juhudi zao za kujikwamua hazifui dafu lakini katika kazi hii mhusika Nana anaonyesha kufaulu kujikwamua na kujipata kutokana na juhudi zake. Kunayo maudhui ya usasa ambayo kwa maoni yetu hayajitokezi kwa uwazi kama yanavyojitokeza katika kazi hii. Kisimulizi, tunapata mchanganyiko wa usimulizi nafsia na usimulizi mwakote. Mwandishi ametumia usimulizi nafsia kwa

upenyezi na upekuzi wa kiwango cha juu ukiwa na mwelekeo mkubwa wa kisaikolojia.

Riwaya hii inaweza kurejelewa kama ya kimaendeleo yenye mmuliko mkubwa kwenye saikolojia ya wahusika kama anavyodai Wamitila (2008: 128) kuwa riwaya ya kisaikolojia huonyesha ukuaji kihusika. Anachosema ni kuwa msanii hubainisha jinsi wahusika wanavyokua kisaikolojia au jinsi mabadiliko katika jamii yanawaathiri kisaikolojia. Kunao ukuaji katika wahusika wa kike kama vile Nana na wa kiume kama vile Faisal na Amour. Aidha, inaonyesha ukuaji katika ujenzi wa msuko kwa kutumia mbinu nyingi na zenye mwelekeo wa kisaikolojia zinazochangia si kujenga ploti tu bali wahusika kisaikolojia na maudhui kwa njia ya kipekee. Riwaya hii inaonyesha namna ambavyo malengo, hali na matendo yanavyochipuka na kuimarika kutokana na matendo ya nje kama wanavyodai Holman na Harmon (1986:402-403) kuwa matendo ya nje yanaweza kuzua hamaniko linalowafanya wahusika waishi katika ndoto za mchana zinazoundwa upya na kujenga hadithi ya kuaminika.

Kwa kuhitimisha sehemu hii, ni muhimu kutaja kuwa Said Ahmed Mohamed anaweza kusemwa kuwa ndiye ambaye kufikia sasa amechangia pakubwa katika kuiendeleza riwaya ya kisaikolojia ya Kiswahili. Hii ni kutokana na kuwa ana kazi nyingi katika orodha ya riwaya za kisaikolojia zinazojibainisha waziwazi na kazi zake zinadhihirisha sifa kamili za riwaya ya kisaikolojia. Ni muhimu pia kutaja kuwa *Nyuso za Mwanamke* kama riwaya ya kisaikolojia imeonyesha kubadilika kimtindo, kihusika, kimaudhui na kiploti ikilinganishwa na riwaya za awali za kisaikolojia. Mabadiliko haya yanatokana na riwaya hii kuchukua zaidi muundo wa riwaya mpya kwa kutumia vifaa kama vile italiki, wino mzito, wahusika vizuu au mizuka, uhalisiajabu na ndoto kwa njia ya kipekee. Kwa maoni yetu, kilele cha ukuaji na mabadiliko katika riwaya ya kisaikolojia ya kisasa ni *Nyuso za Mwanamke.*

## 1.2 Tatizo la utafiti huu

Riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010) iliyoandikwa na Said Ahmed Mohamed ni riwaya inayozungumzia maisha ya mhusika Nana anayeathirika kutokana na maamuzi yanayofanywa na wazazi wake hasa baba yake. Kimsingi, inazungumzia masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Ni riwaya

inayoonyesha uchangamano mkubwa katika karibu vipengele vyote vya riwaya ya kisaikolojia.

Tuliitafiti riwaya hii kwa kutumia nadharia ya saikolojia changanuzi. Kutokana na uchunguzi wetu si watafiti wengi wamechanganua riwaya ya Kiswahili kwa mtazamo huu. Kwa mujibu wa Wa Mutiso (1992:20) wengi wanaiona kama nadharia tata. Kwetu sisi hatuoni utata huo kwa vile hii ni nadharia inayoiona fasihi kama ndoto ya mwandishi na ndoto hiyo inaweza kubainishwa kwa kuchanganua uhusika wa ndani wa wahusika ambao ndio kielelezo cha binadamu wa kawaida anaowaona katika jamii yake. Kama tutakavyoonyesha baadaye inayo madai yanayoeleweka na mwongozo bainifu wa kuchanganua kazi ya kifasihi.

Aidha, tafiti za riwaya za kisaikolojia tulizodurusu ni za riwaya za kiingereza kama Morroe (1977) na Imlay (1989) ambazo hazijikiti katika nadharia yoyote. Katika uchunguzi wao wanachanganua uhusika na namna ambavyo wahusika wanavyotatizika kisaikolojia. Kwa sababu riwaya ya kisaikolojia hujikita sana katika kusawiri hali za kisaikolojia za wahusika, kuna uchukulizi kuwa vipengele vingine kama msuko, maudhui, usimulizi na mtindo hazina uamilifu mkubwa wa kisaikolojia katika kazi ya kisaikolojia. Kwa maana hiyo tulionelea twende hatua moja mbele kubainisha mbinu za kimtindo na kiploti zinazojenga uhusika wa ndani wa wahusika ili kulifanya suala hili kuwa bainifu zaidi. Hali kadhalika kunayo Kazi ya Traore (2008) inayochunguza suala la familia na jamii katika riwaya za ***Asali Chungu*** (1978), ***Dunia Mti Mkavu*** (1980), ***Utengano*** (1980), ***Kiza Katika Nuru*** (1988), ***Tata za Asumini*** (1990) na ***Babu Alipofufuka*** (2001). Uchunguzi wake unajikita katika suala la wahusika na maudhui ya familia na jamii. Hata hivyo hauonyeshi hali za kisaikolojia zinazojitokeza katika kazi hizo.

Riwaya ya kisaikolojia ya Kiswahili ni ngeni katika fasihi ya Kiswahili kwa hivyo haijafanyiwa utafiti mwingi kwa sababu kwamba imekuwepo kwa muda wa karibu miongo miwili tu. Kwa maana hii utafiti wa riwaya ya kisasa ya kisaikolojia ni suala ngeni. Nyingi ya tafiti za kazi za kisaikolojia tulizokumbana nazo ni za tamthilia na ushairi kama Okello (1992), Wa Mutiso (1996) na Wamitila (2001). Kazi hizi zinazungumzia suala la motifu za ndoto katika tamthilia na motifu za vikale katika ushairi. Kwa sababu

masuala haya yanajitokeza katika riwaya kuna umuhimu wa kuyachanganua ili ionekane namna yanavyojitokeza.

Riwaya ya kisaikolojia ni riwaya ya kipekee sana katika taaluma ya fasihi. Upekee wa riwaya hii unatokana na namna ambavyo wahusika husawiriwa kwa jinsi ya kudokeza hali zao za ndani. Kwa njia hii msomaji anaweza kutambua kiyakinifu anayowaza na anavyohisi mhusika fulani. Kwa maana hiyo tunadhamiria kuchunguza mbinu za ujenzi wa msuko na uhusika ili kubainisha upekee huu. Mbali na hayo, riwaya hii hutumia mbinu ambazo huifanya riwaya kuwa tendati na yenye miondoko kama ilivyo drama. Kutokana na mbinu hizi riwaya hii huweza kunasa raghba ya msomaji yeyote. Mbinu hizi ni kama vile dayolojia ya ndani, uzungumzinafsi ndani na usimulizi saikolojia. Hivi ndivyo riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke*** ilivyo.

Hali kadhalika, riwaya ya kisaikolojia ya Kiswahili imeonyesha maendeleo makubwa tangu kuibuka kwake miongo miwili iliyopita. Maendeleo haya yanaonekana kihusika, kimtindo, kimaudhui na kimsuko. Maendeleo haya yameipa riwaya hii sura tofauti na riwaya tangulizi katika utanzu huu wa riwaya. Kwa mfano, kuna baadhi ya riwaya zinazoonyesha sura ya safari ya kisaikolojia ya mhusika ya kujitambua na kujipata kama ilivyo katika ***Nyuso za Mwanamke*** na ***Babu Alipofufuka***. Kwa upande mwingine, huchukua sura ya ndoto zisizo na kikomo zinazompitikia mhusika kama ilivyo katika ***Dunia Yao*** ilhali nyingine huchukua picha za masuala anuwai yanayompitikia msanii katika msimulizi wa nafsi ya kwanza kama ilivyo katika ***Bina-Adamu!*** Hivyo basi, ni muhimu kuchanganua vipengele vya sura ya riwaya hii ili kuonyesha namna vinavyooana, kuchangia na kuchangiana ili kuunda kiunzi kizima cha ***Nyuso za Mwanamke***.

Riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke*** ni kazi inayovutia na kuibua masuala muhimu yanayoweza kumpa hamu mtafiti yeyote kuyachanganua kwa lengo la kuyafanya yaeleweke zaidi. Riwaya hii inayadokeza masuala kama vile ndoa, mapenzi, haki za watoto, usawa wa kijinsia, usasa na umiliki wa rasilimali. Haya ni masuala yaliyo na mvuto mkubwa kwetu yaliyotufanya tukatake kuchungua jinsi yanavyojitokeza katika kazi hii tofauti na tunapoyaona katika jamii tunamoishi.

Kutokana na maelezo haya tunadhamiria kuchanganua masuala yafuatayo; ujenzi wa msuko, usimulizi, uhusika na wahusika, maudhui na mtindo. Uchunguzi wa masuala haya unafanywa kwa kuegemea saikolojia ili kuonyesha namna yanavyojitokeza kisaikolojia katika *Nyuso za Mwanamke*. Kwa maana hii utafiti wetu ni wa kisaikolojia wenye msogeleano wa kifasihi na wala si saikolojia sisisi.

## 1.3 Madhumuni ya utafiti

Dhamira ya utafiti huu ni kuonyesha, kuchanganua na kubainisha kwa uwazi mitagusano inayoibuka katika jamii husika inayosawiriwa katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* na namna ambavyo wahusika wanavyoathirika ndani kwa ndani. Tunabainisha matokeo ya kuathirika huko kihusika na matukio yanayojitokeza baadaye ndani na nje ya wahusika.

Aidha, tunalenga kubainisha mbinu za usukaji wa matukio muhimu katika riwaya hii kama matukio yenye mwelekeo wa kisaikolojia ili kuchunguza uhusiano uliopo kati ya hali za kisaikolojia za wahusika na matendo yao. Kuafikia lengo hili kutahitaji kuchunguza kwa tafsili mbinu za ujenzi wa msuko au ploti kama vile mkondo wa ung'amuzi, uzungumzinafsi ndani, ndoto, mbinu rejeshi na mbinu elekezi.

Mbali na hayo, utafiti huu unalenga kuonyesha riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* kama riwaya ya kisaikolojia. Ili kufikia lengo hili tuliichunguza riwaya hii kwa ujumla wake tukiegemeza uchunguzi wetu kwenye vipengele muhimu vya riwaya hasa vyenye msogeleano na saikolojia. Vipengele hivi ni kama vile umbuji wa wahusika, usimulizi, ujenzi wa ploti, maudhui na mtindo.

Hali kadhalika, lengo la utafiti huu ni kuchangia uelewa wa kazi ya kifasihi hususani riwaya ya fasihi ya Kiswahili kwa ujumla wake. Suala hili ni muhimu kwa sababu linatimiza lengo la utafiti la kuonyesha kitalaamu namna riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* ni riwaya ya kisaikolojia kwa kurejelea maendeleo ya riwaya ya kisaikolojia ya Kiswahili kwa ujumla.

Ni madhumuni ya utafiti huu kuonyesha namna ambavyo mwandishi alidhamiria kuwasawiri wahusika na kudokeza msukumo wa matendo yao na hali zao za kisaikolojia ili ujumbe umfikie msomaji kwa uzito

zaidi. Mchango wetu ni kuonyesha kitalaamu riwaya hii kama kazi ya kisaikolojia kisanaa.

Tunakusudia pia kuonyesha maendeleo ya riwaya ya kisaikolojia katika kitengo cha kimaudhui, kiutanzu, kihusika na kimtindo. Hivyo tunalenga kuonyesha upanuzi wa mipaka ya riwaya ya Kiswahili kushugulikia masuala ya kisasa kama vile haki za watoto, umiliki wa mali na usawa wa kijinsia.

## 1.4 Nadharia tete

Utafiti huu utaongozwa na nadharia tete zifuatazo;

1. Riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke*** inaweza kuainishwa kama riwaya ya kisaikolojia.
2. Riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke*** inaonyesha ukamilifu katika kipengele cha umbuji wa wahusika kati ya vipengele vingine vya riwaya ya kisaikolojia.
3. Mtindo si nyenzo kuu ya kuiunda kisanii riwaya ya ***Nyuso za mwanamke*** kama riwaya ya kisaikolojia.

## 1.5 Sababu za kuchagua mada hii

Tunaitafiti mada hii kwa sababu kama tujuavyo sisi, kazi ya ***Nyuso za Mwanamke*** (2010) ambayo ni ya juzi tu kuchapishwa haina tafiti nyingi tunazozijua. Kwa maana hiyo, utafiti huu utaimulika kazi hii na kujenga ufahamu mojawapo wa awali wa kazi hii. Aidha, kazi nyingi tulizozidurusu zilikuwa za fasihi ya Kiingereza na hazikujikita katika nadharia yoyote au zilichanganua tu baadhi ya vipengele vya kazi za kisaikolojia kwa kutumia nadharia nyingine. Kazi hizi ni kama Paris (1974), Morroe (1977) na Okello(1992). Kwa hivyo kunayo sababu ya kujaza nafasi ya kukosekana kwa tahakiki zaidi za kazi hizi na riwaya ya kisaikolojia ya Kiswahili kwa jumla.

Riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke*** ni riwaya inayodokeza masuala mengi tata ya kijamii. Masuala haya ni kama vile haki za watoto, malezi ya watoto, haki za wanawake, usasa, umiliki wa mali na usawa wa kijinsia. Haya ni masuala ibuka na maarufu katika ulimwengu wa sasa yaliyo katika mkondo wa midahalo mingi ya kisiasa, kijamii na kiuchumi katika vyombo vya habari, mitalaa shuleni na vyuoni na mikutano ya kitaifa na kimataifa. Kwa maana hii tulivutika nayo tuchungue ili tubainishe namna yanavyojitokeza katika kazi hii.

Mbali na hayo, riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke*** kwa maoni yetu ni mwendelezo wa riwaya ya ***Tata za Asumini.*** Sababu ni kuwa riwaya zote zinasawiri mwanamke aliyedhalilishwa na mwenye vita vya ndani kwa ndani. Hata hivyo, kuna tofauti za kihusika kati ya mhusika Asumini katika ***Tata za Asumini*** na Nana katika ***Nyuso za Mwanamke.*** Asumini ni mhusika anayesumbuka kisaikolojia bila matumaini ya kujikwamua hali inayomfanya awachukie wanaume na ashindwe kujenga mahaba nao. Kwa upande wake, Nana anaonyesha kukua kimawazo, kihisia na kiuchumi. Kwa maana hii yeye ni kielelezo cha mwanamke wa kisasa anayepigania usawa badala ya kujikunyata na kungojea apewe msaada na wanaume. Ni tofauti kama hizi zilizotuvutia tuchanganue kazi hii ili tuzibainishe namna wahusika wa kike wanakua.

Kazi za Said Ahmed Mohamed ni maarufu katika fasihi ya Kiswahili zinazoenziwa sio tu katika Afrika Mashariki na Kati bali popote pale Kiswahili kinaenziwa. Hii ni kwa sababu kazi hizi huvutia kimtindo, kimuundo, kihusika na kimsuko. Riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke*** ni riwaya iliyosheheni uchangamano karibu katika vipengele vyake vyote. Ni masuala kama haya yaliyotufanya tuchague kazi hii kama data ya utafiti wetu.

## 1.6 Mipaka na upeo

Tuliitafiti kazi hii kwa kutumia nadharia ya saikolojia changanuzi. Kuhusu nadharia hii tulizingatia mawazo ya Lacan kama anavyomrejelea Freud wala si mawazo ya Jung. Sababu ya kufanya hivyo ni kuwa madai ya Jung yanaegemea uchanganuzi wa vikale huku mawazo ya Lacan yakiegemea uchanganuzi wa uhusika wa ndani, mpangilio wa ishara na uashiriaji, msuko na usimulizi.

Mbali na hayo, tulivichunguza vipengele muhimu vinavyopendekezwa chini ya uchanganuzi wa kisaikolojia hasa umbuji wa wahusika, maudhui, ujenzi wa ploti, mbinu za usimulizi na mtindo wa uwasilishaji wa umbo la kisanii.

Aidha, tunaelewa kuwa kazi yoyote ya sanaa hususani fasihi huwa na pande mbili; ulimwengu wa kiubunifu na ulimwengu halisi. Ulimwengu wa kibunifu wa wahusika ni riale kwa ya pili na ulimwengu halisi wa watu katika jamii. Kwa maana hii, uchunguzi huu ulituelekeza kwenye uhusiano uliopo kati

ya hali za kisaikolojia za wahusika na mambo waliyopitia katika utoto wao hasa yaliyobanwa katika ung'amuzibwete wao na hali zilizopo katika jamii husika.

Mwisho, ili kufanikisha lengo letu la utafiti huu tulirejelea riwaya nyingine za Said Ahmed Mohamed kama vile ***Tata za Asumini***, ***Babu Alipofufuka***, ***Dunia Yao*** ili kuelewa namna anavyovijenga vipengele muhimu vya kazi zake. Aidha, tulirejelea riwaya nyingine za waandishi wengine kama vile ***Bina-Adamu!*** na ***Musaleo!*** za Wamitila kwa lengo lilo hilo.

## 1.7 Msingi wa nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya saikolojia changanuzi. Hii ni nadharia iliyoasisiwa mwanzoni mwa karne ya ishirini na Sigmund Freud mwananyurolojia aliyeishi kati ya mwaka wa 1856-1939. Ilijengwa na wafuasi wake wakiwemo Carl Gustav Jung, Jacques Lacan na wengine kama vile Ernest Jones, Maria Bonapate na Julia Kresteva.[6] Kati ya wanasaikolojia changanuzi hawa mawazo ya Sigmund Freud, Jacques Lacan na Carl Gustav Jung ndiyo yaliyo maarufu. Dhana hii ya saikolojia changanuzi ilitajwa na Freud kwa mara ya kwanza mwaka wa 1909 akiwa katika Chuo kimoja kule Marekani.

Msingi wa mawazo ya nadharia hii ulitokana na kitabu maarufu cha Freud kilichoitwa ***Interpretation of Dreams*** **(1900)**. Kwa mujibu wa maelezo yake katika kitabu hiki aliamini ya kwamba matukio, matamanio na tumaini za binadamu huhifadhiwa katika ung'amuzibwete na kuwa ndoto zote husheheni mambo haya yaliyohodhiwa katika ung'amuzibwete huo. Anaongeza kuwa ndoto zina malighafi kutoka siku zetu za nyuma hasa za utotoni. Kwa maana hii hivyo basi ndoto hutokana na maisha yetu ya awali hasa mawazo na matukio ambayo tumeshiriki. Kwa kutumia taswira za tajriba zetu ndoto huunda fikira kuwa njozi. Kutokana na maelezo haya ni wazi kuwa mchakato wa uotaji unahusishwa na namna mtu alivyo kihisia, kifikira, kimaadili na kimatakwa. Ni kutokana na maelezo haya Freud alikuja kuiona kazi ya kifasihi kama ndoto ya mwandishi.

Freud (1900:277-338) aliibuka na dhana nne zinazohusiana na ndoto. Kwanza, kuna dhana ya ubanaji ambayo ni hali ya mambo kudhihirika katika ndoto ambayo katika maisha ya kawaida hayapo kwa sababu ya kubanwa au kuzuiwa na kaida za kijamii. Hali hii kwa maoni yetu inaonyesha kuwa ingawa yamezuiwa

yapo tu katika ung'amuzibwete wa mwotaji. Mambo haya ni kama uchu wa kingono na mawazo hasi dhidi ya kaida za kijamii. Aidha, kuna dhana ya ubadilishaji ambayo ni hali ya kugeuza matamanio ya mhusika yaliyobanwa kabisa kwa mambo mengine. Watu katika hali hii huonekana kuyapinga mambo yaliyobanwa kwa sababu nafasi ya mambo hayo yamechukuliwa na mambo mengine. Hali kadhalika, kuna dhana ya uhusishaji ambapo baada ya matamanio ya mtu kubanwa mhusika huhusisha kilichobanwa na chochote kinachofanana nacho. Na mwisho, aliibuka na dhana ya udidimivu ambayo ni hali ya kutaka kurejelea hali za utotoni. Mambo yanayodhihirishwa na dhana hizo ndiyo aliyokuwa anayaona katika wagonjwa wa kiakili. Kwa sababu hii katika kazi ya kifasihi wahusika wanaotatizika kisaikolojia hudhihirisha hali za dhana hizi katika uhusika wao. Na hii ndiyo sifa moja ya riwaya ya kisaikolojia. Mfano mzuri wa wahusika wa aina hii ni Asumini katika ***Tata za Asumini*** na Faisal na Nana katika ***Nyuso za Mwanamke.***

Freud K.h.j (Uk:351-353) pia anadai kuwa ndoto huwasilishwa kwa ishara ambazo ni tamathali mbalimbali za kudhihirisha uana. Anaongeza kuwa ishara hazijitokezi tu katika ndoto bali pia katika utani, methali, nahau, ngano, visasili na kafara. Kimsingi, ishara hudhihirisha maana fiche za mawazo. Hivyo tunachukulia ndoto kuwa ishara ya mahusiano ya mwotaji ambayo yanapaswa kupewa ufasiri. Kutokana na mawazo haya aliibuka na tamathali za kike na za kiume. Kulingana na Freud tamathali zinazowakilisha hali za kike zina mpanuko au mfunuko kama ua na ziwa nazo tamathali zinazowakilisha jinsia ya kiume zimesimama kama penseli, kalamu au mkuki, yaani zenye ukali au zilizochongoka. Kutokana na utafiti wake tamathali hizi zilidokezwa;

| **Tamathali za kiume** | **Tamathali za kike** |
| --- | --- |
| Vijiti | boksi |
| Mwavuli | kabati |
| Visu | chumba |
| Ufunguo | kufuli |
| Chuma | mbao |

Ishara hizi zilipotokea katika ndoto wakati wa Freud ufasiri wa ndoto hizo ulitegemea ishara hizi. Hata hivyo inafaa ieleweke kuwa maana za ishara hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine ingawa baadhi

yazo zinaweza kuwa sawa. Kwa mujibu wa mawazo haya uchanganuzi wa kazi ya kifasihi kisaikolojia unafaa kuzibainisha na kuzifasiri ishara zinazotokea katika matini za kifasihi ili kupata ujumbe wa msanii kikamilifu.

Freud K.h.j (uk: 488-492) anaongeza kuwa ndoto huwa na mapengo yaliyoachwa na hujazwa na mwotaji aamkapo. Mchakato wa ujazaji mapengo ili kuipa ndoto muundo unaokubalika aliuita masahihisho ya kiupili. Mapengo yanayotokea katika ndoto yanatokana na uhalisi wa mawazo ya binadamu ambayo yana mkurupuko katika mkondo wake. Kulingana naye, kazi ya kifasihi kama dhihirisho la ndoto ya msanii hufanyiwa masahihisho ya kiupili kwa kuipa umbo la kisanii linalokubalika na wasomaji.

Mawazo ya Freud (1910:63-137) kuhusu Leonardo da Vinci ni kijenzi kingine cha nadharia hii. Leonardo alizaliwa mwaka wa 1452. Alikuwa mchoraji shupavu na baadaye akawa mhandisi. Alikuwa mnyamavu, mpole, mwenye amani na mkarimu. Kutokana na tabia yake hiyo alikataa kula nyama kwa kudai kuwa kula nyama kuliwanyima wanyama haki ya kuishi. Alijiunga na jeshi na kuunda silaha hatari ingawa alipinga vita na umwagikaji wa damu. Hakuwahi kuoa wala kuonyesha mapenzi kwa mwanamke yeyote. Inaaminika alikuwa shoga na hata wakati mmoja alishtakiwa kwa kulawiti mmoja wa wanafunzi wake. Alimpenda mama yake sana na upendo huo unabainika kutokana na orodha ya gharama kubwa ya matibabu na mazishi yake alipofariki.

Kwa mujibu wa Freud K.h.j ushoga wa Leonardo ulitokana na kumpenda mama yake sana na kukosa malezi ya baba yake. Inadhihirika kutokana na hadithi ya kumbukizi za utotoni inayodai kuwa siku moja alitokewa na tai aliyechezesha mkia wake na kupigapiga mdomo wake. Katika hadithi ya kimisri tai ni ishara ya mama na mkia ni ishara ya sehemu ya uume. Hadithi hii ni ishara ya fantasia za kunyonya au kunyonywa na mama yake. Anaongeza kuwa inaelekea mama yake alimpenda sana kiasi cha kuichezea sehemu hiyo na kumbukizi yake ilibaki ndani mwake. Hali hii ilisababisha ubanaji wa uchu wa kingono kwa wanawake kwa kuhofia kumsaliti mama yake. Ushahidi wa ubanaji huu unadhihirika katika mchoro mmoja wa mwanamke mjamzito aliyemwonyesha kuwa na titi moja bapa hali inayoonyesha kuwa hakujali sana uzazi kwani hakujishughulisha na kuona namna titi la mama mjamzito lilivyokaa. Anadai pia kuwa

Leonardo aliyabadilisha matamanio yake ya uana na juhudi za kupata ufahamu na uchoraji kutokana na kuzuiwa kwake. Aidha, mchoro aliouchora wa Mona Lisa anayetabasamu ulichukuliwa kama mabaki ya kumbukumbu ya uso wa mama yake aliokatiziwa kuwa nao kwa kuvunjika ndoa ya wazazi wake. Hii ni kwa sababu msanii huakisi hali ya mawazo yaliyohifadhiwa katika ung'amuzibwete wake.

Mawazo haya kwa mujibu wa Freud yana mchango mkubwa katika saikolojia changanuzi kwa kutoa madai yafuatayo; Kwanza, uchunguzi wa wahusika kwa mtazamo huu ni sharti ubainishe namna ambavyo matamanio ya wahusika hasa ya uana yalivyobanwa. Pili, unafaa uonyeshe juhudi za wahusika hao za kufidia ubanaji wa matamanio yao kwa kuyabadilisha na mambo mengine. Hii ndiyo hali inayotokea katika riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke*** ambapo Faisal baada ya kukosa penzi la Bimkubwa anageukia muziki. Tatu, uchunguzi huu sharti ubainishe juhudi za wahusika walioathirika kwa kurejelea matamanio yao. Hali hii ndiyo inayotokea katika riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke*** pale ambapo Nana anafaulu kujikwamua kutokana na dhuluma za baba yake na ingawa alikuwa amewachukia wanaume anasalitika tena na kuolewa na Amour.

Kwa kuongezea, Freud (1916:16-25) anadai kuwa dhana ya ubanaji ndiyo msingi wa saikolojia changanuzi. Anadai kuwa masuala mawili huibuka wakati wa jaribio la kubaini chanzo cha mtu anayetatizika kisaikolojia kutokana na ubanaji wa matakwa yake ambayo ni uhawilisho na upinzani. Uhawilisho ni hali ya mhusika kujaribu kuhamishia kwingine sababu ya hali inayomkumba ilhali upinzani ni hali ya kutotaka kufichua hali inayomkumba ili uvumbuzi upatikane. Kimsingi, uhawilisho hutokea hasa kwa mhusika kuhofia kukiuka kaida za kijamii kama zile zinazopinga mtoto kumlaumu baba yake kwa shida zinazomkumba na upinzani hutokea kwa mhusika kuona aibu ya kuyasema hadharani yanayomkumba. Mfano wa hali ya masuala haya unatokea katika riwaya ya ***Tata za Asumini*** ambapo Asumini anatinda kuongea juu ya hali yake ya kuwachukia wanaume kwa kuogopa kumkashifu baba yake na kuona aibu kukiri kuwa ameshindwa kujenga usuhuba na wanaume kwa sababu hakupewa nafasi ya kujifunza siku za utotoni.

Madai haya yana manufaa makubwa kwa uchunguzi wa matini kwa mtazamo huu. Kwanza, yanatusaidia kuelewa kiini cha vita vya ndani kwa ndani vya wahusika. Pili, yanatusaidia kueleza athari za ubanaji wa matamanio kama vile kukumbwa na kibuhuti na kuwa na jinamizi. Tatu, yanatufaa kuelewa kwa nini baadhi ya wahusika wanajitenga na hali ya kawaida ya maisha wanapokumbwa na matatizo ya kisaikolojia kama Faisal katika ***Nyuso za Mwanamke*** aliyetoroka nyumbani kwake kwa kumkosa Bimkubwa.

Hali kadhalika, Freud (1961:13-26 ) anaongeza kuwa uelewa wa ung'amuzi na ung'amuzibwete ndilo suala la kimsingi la saikolojia changanuzi. Ung'amuzi ni sehemu ya fikira za binadamu ambayo ina mawazo tunayoyafahamu barabara ilhali ung'amuzibwete ni sehemu ya fikira ambako kumehodhiwa mawazo ya mambo ambayo hatuna ufahamu wa moja kwa moja lakini hujitokeza tu kama ndoto. Mawazo na matukio yaliyohifadhiwa katika sehemu ya ung'amuzibwete ndiyo malighafi ya ndoto na kazi za kifasihi. Kwa hivyo ni jukumu la uchunguzi wa kisaikolojia kubainisha mawazo na matukio ya wahusika yanayotokana na ung'amuzibwete ambayo ndiyo msingi wa kubainisha saikolojia ya wahusika na mwandishi wa kazi husika.

Lacan (1977:30-113) naye anaiona saikolojia changanuzi kama zoezi la usemi na nadharia ya mhusika asemaye. Kwake yeye, nadharia hii hujikita katika kuchanganua usemi wa mhusika kwa lengo la kudokeza mpangilio wa mawazo na fikira katika ung'amuzibwete. Aliibuka na mipangilio mitatu inayohusiana, yaani mpangilio wa kimawazo, wa kiishara na wa kiuhalisi. Mpangilio wa kimawazo ndio uliojaa fantasia na taswira za utotoni hadi ukubwani na ni katika mpangilio huu ambapo mawazo na hisia huhifadhiwa katika ung'amuzibwete na hujitokeza kama njozi za mhusika. Nao mpangilio wa kiishara unahusiana na ishara na mfumo wa uashiriaji. Kutokana na mpangilio huu tunaiona lugha kama mfumo wa ishara na hivyo yeye anaiona fasihi kama lugha iliyojaa ishara zenye maana anuwai zinazopaswa kufasiriwa ili kuipa fasihi maana. Ishara hizi zinaweza kujitokeza kama tamathali za uana zinazotumiwa kubainisha masuala mbalimbali ya uana katika jamii kama alivyodai pia Freud. Ishara hizi ni sehemu ya utamaduni wa jamii anamoishi binadamu. Mpangilio wa kiuhalisi nao unahusiana na tapo la uana na mauti. Huu ndio mpangilio uliodhibitiwa na kaida za kijamii zinazowazuia watu kufanya na kusema mambo fulani kwa kuhofia

kukiuka kaida hizo. Lacan pia alizungumzia dhana ya msukumo na hamaniko kama dhana zilizo chanzo cha hamasa na matendo mengi ya wahusika katika kazi ya kifasihi.

Lacan kama Freud anaiona kazi ya kifasihi kama ndoto ya mwandishi. Kwake yeye ndoto hii hujitokeza kwa matumizi ya lugha ya kifasihi iliyojaa ishara ambazo zinafaa zifasiriwe ili hali ya mhusika ijulikane na maudhui yabainike. Kimsingi, mawazo haya yameathiriwa na mkondo wa kimuundo. Aidha, uchanganuzi wa wahusika unafaa ubainishe mawazo na maarifa yaliyo katika ung'amuzibwete. Kwa maana hii mawazo haya yanafaa sana katika uchanganuzi ya uhusika na wahusika, usukaji wa matukio anamoshiriki mhusika, mtindo wa umbuji wa umbo la kisanii na maudhui.

Mawazo ya Lacan yanaungwa mkono na Holman na Harmon (1986:402) wanaodai kuwa saikolojia changanuzi inaiona fasihi kama ishara na lugha ambayo bila kukusudia huelezea maana au lengo. Kwao uhakiki kwa nadharia hii hulenga matendo ya wahusika katika kazi za kibunilizi kama kipengele muhimu cha ujenzi wa matini. Uchunguzi huu hujaribu kudadisi malengo ya wahusika wanapojihusisha na matendo fulani na namna wanavyoathirika kisaikolojia. Kwao mtazamo huu unaweza kutumiwa kuchunguza usawiri wa wahusika kisaikolojia pamoja na kubainisha mbinu zake kama uzungumzinafsia, usimulizi nafsia na mkondo wa ung'amuzi.

Mchango mwingine wa nadharia hii unatokana na mawazo ya Frye n.w. (1985:377). Kwa maoni yao uhakiki kwa nadhara hii ni wa kibibliografia unaotumia ufahamu wa saikolojia kumulika maisha ya mwandishi. Linalojitokeza ni kuwa matini husaidia kuelezea maisha na matamanio ya mwandishi au maisha na matamanio ya mwandishi yanaweza kuelezea kazi yake. Wanaongeza kuwa uhakiki huu hutumia vifaa vya kisaikolojia kubainisha uhusiano kati ya tajriba na uwezo wa mwandishi na ubunifu wake katika matini. Vifaa hivi vinaweza kuwa usawiri wa wahusika kisaikolojia, ndoto na sintaksia yenye nyufa. Hizi ndizo mbinu tunazoziona zikijitokeza katika riwaya za ***Babu Alipofufuka, Tata za Asumini*** na ***Nyuso za Mwanamke.*** Madai yao yatatufaa kuchanganua uhusika na wahusika, mbinu za ujenzi wa ploti na mtindo.

Mchango mwingine unatokana na Eagleton (1996:155-168) anayeona saikolojia changanuzi kama inayoweza kutufichulia namna ambavyo matini zimeumbwa na maana ya umbuji huo. Kwamba, uchanganuzi huu unaweza kufanywa kwa mitazamo minne. Kwanza, uchanganuzi wa yaliyomo unaohusu uchunguzi wa wahusika na umuhimu na madhumuni ya matendo yao ambao unatumiwa kutafuta ishara za nguvu za kizazi. Pili, uchangannuzi wa mwandishi unaohusu jinsi mwandishi anavyojidhihirisha katika kazi yake hasa ushahidi wa mambo yaliyohodhiwa katika ung'amuzibwete kama vile matakwa na matamanio yanayomfanya aepuke uhalisi na kurejelea hali za kinjozi (kifantasia). Katika hali hii msanii huunda kiujumi matini ili kupunguza ukali wa ndoto zake za mchana na kuzifanya zikubalike na wengine. Umbuji huu wa umbo la kisanii humwezesha msomaji kuwa na furaha ya kimbele inayopunguza pingamizi zake dhidi ya matarajio ya ufanisi wa wengine na kumfanya aondoe kibano juu ya ung'amuzibwete wake ili apokee mambo yasiyoruhusiwa na kaida za kijamii. Msanii hutimiza hili kwa kutumia mbinu za kiujumi zinazoifanya kazi yake ivutie wasomaji. Mwisho, kuna uchanganuzi wa msomaji unaochunguza namna ambavyo msomaji hufasiri ujumbe katika kazi ya kifasihi ili abainishe utambulisho wake kama mtu binafsi. Kupitia kazi za kifasihi msomaji anaweza kujisoma na kujisahihisha au anaweza kujihurumia au kujichukia kwa namna alivyo. Mitazamo hii inamsaidia mhakiki achague mitazamo atakayotumia ili kuipa kazi ya uhakiki utaratibu wa kimpangilio.

Eagleton pia anaingalia kazi ya kifasihi kama akisi ya uhalisi kwani inaonyesha tajriba ya binadamu, lengo la mwandishi na muundo wa fikira za binadamu. Kama ndoto, kazi ya kifasihi sio tu akisi ya uhalisi bali ni umbo la uzalishaji wake. Hivyo basi, kazi ya kifasihi huchukua malighafi ambayo ni lugha, matini nyingine za kifasihi, mitazamo ya kiulimwengu na kuziunda kwa mbinu za kisanii kuwa matini za kifasihi. Yeye anaiona fasihi kuwa zao la mawazo, matamanio na tumaini la mwandishi na jamii anamoishi. Madai haya yanasaidia mhakiki kubainisha hali halisi zinazojitokeza katika matini zilizo katika ulimwengu wa kawaida.

Holland (1997:143-148) naye alizungumzia mkondo wa usomaji na ufasiri wa kazi ya kifasihi kwa kudai kuwa kila msomaji wa hadithi au shairi hulifasiri kwa njia tofauti na mwingine kutokana na ubinafsi unaombainisha. Sababu ni kuwa kila binadamu ana usawa na utofauti na binadamu mwingine. Wanaongeza

kuwa usawa unaweza kubainishwa kwa kuona kinachoendelea katika mabadiliko dhidi ya kisichobadilika. Kulingana naye maudhui ya kazi ya kifasihi yanaweza kubainishwa kwa kuchunguza mpangilio wa maisha ya mtu kama unavyoyafikia maudhui ya kipande cha muziki. Aidha, maudhui yanaweza kubainishwa kwa kuchunguza motifu za kimaudhui zinazojitokeza katika kazi kadhaa za mwandishi. Katika kazi za Said A. Mohamed motifu za kimaudhui ni suala linalojitokeza kwa uwazi. Kwa mfano, kuna motifu za maudhui ya ukombozi wa mwanamke, malezi na ndoa zinazojitokeza katika riwaya zake kama vile ***Asali Chungu, Utengano, Tata za Asumini*** na ***Nyuso za Mwanamke.*** Utokeaji huu si wa kisadfa tu bali dhihirisho la mawazo yake kuhusu jamii.

Aidha, aliibuka na istilahi nne za kuchanganua kazi za kifashi ambazo ni kujilinda, matarajio, fantasia na mageuzi. Kujilinda hurejelea hali ya mtu kuruhusu au kuzuia mambo kutoka nje au kuingia ndani. Matarajio nayo ni kuwepo kwa fasihi katika mkondo fulani wa matakwa ya mtu katika kipindi fulani cha wakati. Maana inayojitokeza hapa ni kuwa mtunzi yeyote huiandika kazi ya kifasihi kurejelea uhalisi fulani unaomkumba yeye na jamii yake katika kipindi mahsusi cha wakati. Nayo fantasia ni kile uonacho mtu akitoa katika ulimwengu wa nje ambacho anakishabikia sana. Kwa upande wake, mageuzi ni kuipa kazi ya kifasihi maana itakayokiuka mipaka ya kiwakati. Madai haya yanatuelekeza kuichunguza kazi ya kifasihi kwa lengo la kubainisha kwa nini wahusika katika matini wanadhihirisha uhawilishaji na upinzani kwa juhudi zinazofanywa kuwakwamua kutokana na matatizo ya kisaikolojia.

Mbali na hayo, Holland K.h.j anadai kuwa, kuwepo kwa mtoto ni dhihirisho la kuwepo kwa mzazi na kuwepo kwa mzazi ni dhihirisho la kuwepo kwa mtoto. Hoja hii ina maana kuwa anachofanya mtoto ni utambulisho wa kile mzazi alifanya. Maoni yetu ni kuwa tabia na mienendo ya mtoto kwa kiasi kikubwa hurejelea tabia na mienendo ya mzazi wake. Hii ni ithibati ya kuwepo dhana ya urithi wa kibaiyolojia. Madai haya husaidia mchunguzi wa kisaikolojia kuonyesha uhusiano kati ya tabia na mawazo ya mhusika na ya wazazi wake. Katika riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke*** tunapata kuwa kule alikovutiwa Faisal ni kule mtoto wake alikovutiwa kimapenzi. Wote wanavutiwa na Nana ambaye ni mtoto wa Bimkubwa aliyekuwa mchumba wa Faisal.

Bloom (1997: 148-152) kuhusu nadharia hii anarejelea jinsi ushairi unaweza kuchanganuliwa kisaikolojia. Kwake, kazi ya kifasihi huwakilisha kilichokuwepo kama msimamo binafsi kwa neno. Aidha, matini za kishairi ni kama roho na hutumiwa na washairi kudhihirisha ukweli fulani wa ulimwengu. Anaongeza kwamba shairi hurejelea shairi lingine na kuwa shairi moja lenye nguvu huwa mwanzo mpya wa mashairi mengine yatakayofuata. Hata lugha ya kishairi ni marudio ya lugha iliyopita. Wanaongeza kwamba nguvu za ushairi huhusiana na kujiwakilisha ambako kunaweza kufikiwa tu kwa kupita mpaka ambao ni kilele cha kishetani. Anachodokeza hapa ni kuwa uandishi wenye nguvu wa kifasihi hupita mipaka ya kaida za kijamii ambazo ni mwiko kuzitaja na ndio ushetani wenyewe. Hoja hii inaingiliana na hoja ya Aristotle inayodai kuwa ili msanii aandike kazi ya kifasihi hupandwa na jadhba fulani. Kwa maana hii, kazi ya kifasihi ndio upeo wa juu wa kuyabainisha mambo yaliyobanwa kwenye ung'amuzibwete. Kuna masuala mawili muhimu yanayoibuka kutokana na madai ya Bloom. Kwanza, kazi ya kifasihi iliyo bora huwa chanzo cha mfululizo wa kazi nyingine zinazobishana kuupiku ubora wa kazi ya awali. Kwa mfano, mfuatano wa riwaya za ***Nagona*** (1987), ***Mzingile*** (1991), ***Ziraili na Zirani*** (1999), ***Babu Alipofufuka*** (2001), ***Bina-Adamu!*** (2002), ***Musaleo!*** (2004) na ***Dunia Yao*** (2006) na *Mafamba* (2008) unaonyesha mwingiliano fulani wa kimtindo ambapo kuna matumizi ya mbinu za riwaya mpya. Katika kila riwaya inayoifuata iliyotangulia kuna jaribio la kimakusudi la kuboresha mbinu hizo au kutumiwa kubainisha mkondo tofauti wa kimtindo au wa kimaudhui. Kwa mfano, kuna mfanano mkubwa wa matumizi ya uzungumzinafsi ndani katika riwaya za ***Babu Alipofufuka, Bina-Adamu!*** na ***Musaleo!*** Kwa maoni yetu riwaya hizi mbili za mwisho ziliandikwa kama mwitikio kwa riwaya iliyozitangulia. Aidha, kuna mahusiano makubwa kati ya riwaya ya ***Tata za Asumini*** na ***Nyuso za Mwanamke*** katika mtindo wa kusawiri wahusika kisaikolojia. Tofauti inayotokea tu ni kuwa katika ***Tata za Asumini*** mhusika mkuu Asumini anakumbwa na vita vya kisaikolojia na kuangamia bila matumaini lakini katika ***Nyuso za Mwanamke*** mhusika Nana ingawa anatatizika kisaikolojia anajikwamua na kujipata.

Suala la pili ni kuwa kazi ya kifasihi inadhihirisha ukiukaji wa juu wa kaida za kijamii bila kuwa na athari ya kupingwa moja kwa moja. Kwanza, msanii huwa na jazba ya aina fulani ya kutokujijua ipasavyo. Ni

katika hali hii anapata ujasiri wa kuzungumzia masuala nyeti ambayo pasi na muundo wa umbuji wa kiujumi angeaibika kuyazungumzia na jamii ingemwona kama mtovu wa nidhamu au mwehu.

Naye Diyanni (1998:1902-1904) anadai kuwa nadharia hii huziona kazi za kifasihi kama zinazolingana na sifa, tabia za kiakili na kihistoria za msanii. Kwamba, kazi ya kifasihi hudhihirisha ung'amuzi na ulimwengu wa kiakili wa mwandishi. Hivyo uchunguzi kwa mtazamo huu huchunguza saikolojia ya mwandishi kwa kurejelea maisha yake hasa barua na shajara zake. Uchunguzi wa vitu hivi hufanywa ili kuelewa vizuri kwa nini anasawiri tabia fulani katika matini. Vilevile, mtazamo huu unaweza kutumiwa kuwachunguza wahusika hasa hali zao za kisaikolojia.

Mbali na hayo, Diyanni sawa na Freud, anaiona saikolojia changanuzi kama mbinu ya kufasiri ishara za tamaa zilizobanwa katika ung'amuzibwete wa wahusika kwa kufasiri vyombo vya kawaida kama saa, minara na vitu asilia kama moto na maji ili kubainisha vipengele vya uana au jinsia katika wahusika wa kifasihi.

Kwa mujibu wa Mbatiah (2001:91), Freud kwanza alibuni dhana ya udodosisaiko[8] kama utaratibu wa kutibu wagonjwa wa akili. Kwake udodosisaiko ni mwelekeo wa uhakiki unaoangalia kazi ya kifasihi kama taswira ya mfumo wa akili na hulka ya mwandishi katika kazi yake. Madai yake ni kuwa kazi ya kifasihi inawakilisha utekelezaji wa matamanio ya mtunzi yaliyozuiliwa na kaida, maadili na thamani za jamii yake. Mambo haya yanabakia katika ung'amuzibwete wake na kujitokeza kama ndoto yake. Kubakia kwa matamanio haya katika ung'amuzibwete ni kwa sababu kila binadamu huogopa kutoa mawazo ambayo ni mwiko au kinyume cha kaida za kijamii kuyasema hadharani asije akakemewa. Hivyo basi, uchunguzi kwa nadharia hii unafaa kuonyesha ishara katika matini ambazo zinawakilisha ung'amuzibwete wa mwandishi kama vile ishara za tabia za urathi, vikale na uana.

Kwa upande wao, Kennedy na Gioia (2005: 2218-2219) wanaongeza kuwa mchango mkubwa wa nadharia hii katika fasihi ni kudhihirisha mchakato wa fikira za binadamu za ung'amuzibwete. Wanaunga mkono madai kuhusu lugha katika utani na mazungumzo kudhihirisha hofu na matamanio ya mzungumzaji.

Aidha, wanadai ishara katika ndoto huonyesha fikira zisizo bainifu zinazoweza kudhihirika katika umbo la neno kuzuia kulaumiwa. Wanadai pia kuwa fasihi kuu hudhihirisha kikweli maisha ya binadamu. Hoja hii inaingiliana na hoja kuwa fasihi ni mali na zao la jamii[9] na kuwa inafaa iyadokeze maisha halisi ya binadamu.

Kennedy na mwenzake wanaibuka na mitazamo mitatu ya kuchanganua kazi za kifasihi kisaikolojia. Kwanza, ni uchunguzi wa mchakato mzima wa kazi ya kifasihi unaolenga athari ya fasihi kwa msomaji hasa akili na hisia zake. Pili, mtazamo wa wanabibliografia[10] wengi wa kisasa wa kuelewa msukumo na tabia za wahusika kama dhihirisho la matamanio ya mwandishi. Tatu, ni uchanganuzi wa wahusika wa kibunifu. Uchunguzi wa Freud wa ***Mfalme Edipode*** ni mfano wa uchanganuzi kwa kutumia mtazamo huu. Ingawa wanataja mitazamo mitatu wanasaikolojia changanuzi wengi wanapendekeza mitazamo minne ambapo mbali na hiyo mitatu kunao mtazamo wa kuchunguza umbo la kisanii la matini na sifa zake za kimsingi za kisaikolojia.

Wafula na Njogu (2007: 78-83) kama Freud wanaiona kazi ya kifasihi kama ndoto na kuwa usanii ni ruiya zinazoashiria matumaini na matamanio ya mwandishi na wahusika wanaopatikana katika kazi ya kifasihi kama wanadamu wanaoishi katika ndoto ya mwandishi. Wahusika hawa ni wanadamu wanaoshirikiana na mwandishi katika matatizo na matarajio yake. Kwa hivyo, maudhui, mtindo, wahusika na mandhari katika matini za kifasihi ni mambo yaliyo katika njozi za mwandishi. Aidha, wanaunga mkono madai ya Freud ya tamathali za kike na kiume na kuongeza kuwa binadamu ni tamathali fiche inayopaswa kufasiriwa. Kwa maelezo yao nadharia hii inaweza kutumiwa kuchunguza saikolojia ya mwandishi na wahusika. Wanaongeza kuwa mawazo ya mtazamo huu yalichangia kuibuka kwa mbinu kama vile mjadala nafsia, mbinu rejeshi na elekezi na ritifaa. Mbinu hizi ndizo zilizo na dhima kubwa ya kudokeza saikolojia ya wahusika.

Hali kadhalika, Wafula na Njogu wanadokeza mawazo ya Gustav Jung kama mfuasi wa Freud. Wanadai yeye alibuni dhana ya kikale[7] inayorejelea aina ya mtiririko au picha kongwe inayojitokeza mara kwa mara katika tajriba anayopitia binadamu. Kwake yeye, mtu na utamaduni wake ni nakala ya watu walioishi kabla

yake. Kwa maana hiyo mtu huathiriwa na jamii inayomzunguka na hawezi kuepukana na athari zake kama vile sherehe na matambiko. Mhakiki kwa mujibu wa mawazo haya atabainisha mambo anayopenda na anayochukia mwandishi kupitia kwa vikale. Aidha, mhakiki hana budi kuviainisha vikale vyote vinavyopatikana katika kazi ya kifasihi na kuonyesha umuhimu wake katika kazi hiyo.

Nadharia hii ina mikondo mitatu muhimu nayo ni mikondo itokanayo na mawazo ya Freud, Jung na Lacan. Mkondo wa Freud na Lacan unairejelea kazi ya kifasihi kama ndoto ya matamanio ya mwandishi na ishara mbalimbali zinazojitokeza katika kazi hiyo. Kwa maoni yetu, mtazamo wa Freud na Lacan unaegemea uhusika na wahusika, saikolojia ya mwandishi na umbo la kisanii la matini. Aidha, wanaiona kazi ya kifasihi kama akisi ya uhalisi fulani katika jamii husika na kwa hivyo maudhui yanaweza kufikiwa kwa kubainisha mpangilio wa maisha ya wahusika na hali halisi katika jamii. Mbali na hayo, kazi ya kifasihi iliyo bora huwa chanzo cha kazi nyingine kama kielelezo chake mbali na kuwa inasaidia kufanya wasomaji wabaini wanachowaza wasanii juu ya kazi hiyo. Jung naye anaegemea upande wa kubainisha vikale katika kazi ya kifasihi. Mawazo yake juu ya dhana ya vikale ndiyo yaliyopelekea kubuni nadharia ya vikale. Kwa njia hiyo saikolojia ya mwandishi inaweza kubainika kwa sababu vikale kama vipengele vya mpangilio wa mawazo, picha, matendo, vitu na hali vikijitokeza katika kazi ya kifasihi ni sehemu ya mawazo ya msanii juu ya jamii yake.

Kutokana na maelezo haya, nadharia hii inaweza kuchanganua umbuji wa wahusika, maudhui, vikale, motifu katika matini, usimulizi, ujenzi wa ploti na tabia za urithi za watoto. Masuala haya yanaweza kuchunguzwa kwa mitazamo minne ambayo ni kuchunguza saikolojia ya mwandishi, wahusika, msomaji na umbo la kisanii la matini. Mhakiki wa saikolojia changanuzi anaweza kuchanganua kazi ya kifasihi kwa mitazamo yote au achukue mtazamo mmojawapo.

## 1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada hii

Katika udurusu wetu, hatukukumbana na tahakiki ya riwaya hii ya ***Nyuso za Mwanamke*** (2010). Hata hivyo, tumezidurusu kazi za wataalamu mbalimbali ambazo zimetudokezea masuala muhimu yanayohusiana na mada yetu. Tunaamini zimetufaa kwa sababu zimeangazia masuala kama vile ndoto,

ujenzi wa wahusika kisaikolojia, mbinu za ujenzi wa ploti na motifu ambayo yanahusiana moja kwa moja na baadhi ya masuala tunayochanganua. Kwa kuzirejelea kazi hii tumeamua kuzidurusu kiutathmini ili kuweza kubainisha kwa uwazi masuala yanayojitokeza.

Kwanza, tulidurusu usawiri wa wahusika kisaikolojia. Katika udurusu huu Morroe (1977: 133-150) anaonyesha namna wahusika wanavyoshindwa kuyafikia malengo yao hutatizika kisaikolojia. Katika uchunguzi wake wa wahusika katika riwaya ya ***Sense and Sensibility***, mhusika Mariame anaposhindwa katika mapenzi anaelekeza huzuni yake katika kazi kama njia ya kudhihirisha hisia zake na kujiliwaza. Mhusika huyu kwa kiwango fulani anafanana na Asumini katika ***Tata za Asumini*** anayeelekeza chuki zake kwa wanaume kutokana na babaye kumnyima uhuru wa kukurubiana na vijana wengine jambo lililomfanya ashindwe kujenga usuhuba na wanaume. Katika riwaya ya ***Sense and Sensibility*** mkewe John Dashwood anachukizwa na kulazimishwa kuwatendea wifize kwa upole. Alibana uhuru wake na kuwatendea hivyo kukidhi kaida na desturi za jamii na kwa hivyo kuyabana matakwa yake. Ubanaji huo ulimfanya aungulike ndani kwa ndani na kwa hivyo akaathirika kisaikolojia. Aidha, alichunguza wahusika katika riwaya ya George Elliot, ***The Mill on the Floss*** (1860) ambapo anadokeza dhana kuwa kaida na mila huwanyima vijana uhuru wa kuolewa na wampendaye. Katika riwaya hiyo, Philip anazuiliwa na babaye kumwoa Maggie kutokana na uhasama uliokuwepo kati ya familia zao. Hali hii inamfanya Philip asononeke kimawazo kwani hata baada ya kumbembeleza babaye hakuridhia.

Uchunguzi huu unatufaa kwa vile unafichua msukumo wa mhusika fulani kutenda tendo fulani suala ambalo linajitokeza katika riwaya ya kisaikolojia. Aidha, dhana ya ubanaji wa matakwa na matamanio ni muhimu katika utafiti wetu kwa sababu ndiyo inayowasababishia wahusika kutatizika ndani kwa ndani kama vile Asumini katika ***Tata za Asumini*** na Nana katika ***Nyuso za Mwanamke***. Hata hivyo, uchunguzi wake hauangazii masuala mengine ya kimsingi kuihusu riwaya ya kisaikolojia kama vile ujenzi wa ploti kisaikolojia, usimulizi-saikolojia na motifu za kimaudhui yanayochangia pakubwa kudokeza hali za ndani za wahusika.

Pili, tulidurusu suala la motifu za ndoto. Motifu ni vipengele fulani katika kazi ya kifasihi vinavyotawala kama vile wahusika, maudhui, tamathali za usemi, namba na kadhalika. Suala hili lilichunguzwa na Okello (1992:2-20) aliyetafiti juu ya motifu za ndoto, uwendawazimu na hali za kifutuhi katika tamthilia za Francis Imbuga- ***Betrayal in the City, Man of Kafira, Game in Silence*** na ***The Burning of Rags.*** Katika utafiti wake, hakutumia nadharia yoyote. Anadai kuwa matumizi ya wahusika waliohamanika na kusumbuka kisaikolojia wanamsaidia mwandishi kuweka wazi matatizo ya kijamii na kubainisha athari zake. Kimsingi, uhusika wa kindani huwasaidia wasomaji wajue dhuluma na ukandamizaji unaoelekezewa wahusika hao. Anaongeza kuwa ndoto husaidia kujua asili ya binadamu na ulimwengu wake kwa ujumla na huonyesha mambo yaliyohodhiwa katika ung'amuzibwete wake.

Kwake ndoto huwa na mengi kuyahusu mambo halisi na watu huota yaliyotendeka au yatakayotendeka. Kwa maelezo haya, ni kweli kuwa ndoto hudokeza yaliyo katika ung'amuzibwete wa binadamu. Aidha, alichunguza namna ambavyo wahusika kama vile Mosese katika ***Betrayal in the City,*** Boss katika ***Man of Kafira***, Raja katika ***Game in Silence*** na Agala katika ***The Burning of Rags*** wanazukiwa na ndoto za kweli na za mchana zinazodokeza kwa uwazi madhila wanayopitia katika jamii husika. Wanaiangalia ndoto kama mbinu ya kimtindo iliyosheheni mbinu rejeshi na mbinu elekezi kwa maana kwamba ndoto hizo zinatufichulia uhalisi wa yaliyopita, yaliyopo na yajayo. Wanaona ndoto kama inayobainika kupitia mbinu za ujenzi wa ploti kama vile mkondo wa ung'amuzi na uzungumzinafsi ndani.

Utafiti wao unaonyesha ndoto kama kipengele cha kujenga ploti na wahusika kisaikolojia. Pia, unabainisha vizuri maswala ya saikolojia changanuzi kama vile ufasiri wa ndoto unaosaidia kuelewa saikolojia ya wahusika. Yeye alienda hatua mbele kwa kubainisha baadhi ya mbinu za ujenzi wa ploti kama mkondo wa ung'amuzi na uzungumzinafsi ndani. Ingawa hivyo, kuna haja ya kubainisha mbinu nyingine za ujenzi wa ploti.

Tatu, tulidurusu suala la motifu za vikale kama linavyojitokeza katika ushairi wa fasihi ya Kiswahili. Vikale kama anavyoeleza Wa Mutiso (1996:19-20) ni vipengele vya kimsingi ambavyo ni wazo, picha, tabia, tendo, kifaa, taasisi, tukio au mandhari yenye sifa za kijadi, kijumla na za kiubia zinazojitokeza

katika mashairi, nyimbo, visasili, ndoto, matambiko na sherehe za jamii fulani. Katika utafiti wake alichunguza motifu zinazojitokeza katika ***Kasida ya Burudai*** na maana zinazowakilishwa na motifu hizo. Alitumia nadharia ya vikale iliyobuniwa na Carl Gustav Jung ambayo ni mkondo mmoja wa nadharia ya saikolojia changanuzi. Nadharia hii hutumika kuchanganua vikale vinavyojitokeza katika kazi za kifasihi. Alichunguza motifu kama vile Nuru Muhammadi (Nuru ya Mtume Muhammad), Hajji na Umra (safari takatifu kuelekea Mundi), Israi na Miiraji (Safari ya Mtume kwenda mbingu ya saba), Koran Tukufu na kadhalika. Motifu anazieleza kama elementi katika kazi ya kifasihi kama maudhui au wazo linalotawala. Kwa maoni yetu, motifu si maudhui au wazo tu bali huweza kuwa wahusika wa aina fulani, mandhari, imani, namba na kadhalika mradi elementi hizo zinatawala katika kazi ya sanaa.

Uchunguzi wa motifu za vikale kama elementi za kijamii zilizohifadhiwa katika ung'amuzibwete zina umuhimu mkubwa kwa utafiti wetu kwa sababu utafiti wetu kwa kutumia mawazo ya Freud na Lacan pia unarejelea ung'amuzibwete wa wahusika na matendo yanayoakisi ndoto za matamanio yao. Aidha, uchunguzi wa motifu zilizotajwa unarejelea vipengele kama maudhui na wahusika ambavyo tumevishughulikia. Hata hivyo, tunakusudia kuvishughulikia kwa undani zaidi, kwa mkondo wa Lacan na katika riwaya ya kisaikolojia.

Hali kadhalika, tulidurusu suala la familia na jamii katika riwaya za Said Ahmed Mohamed za ***Asali Chungu*** (1978), ***Dunia Mti Mkavu*** (1980), ***Utengano*** (1980), ***Kiza Katika Nuru*** (1988), ***Tata za Asumini*** (1990) na ***Babu Alipofufuka*** (2001). Traore (2008: 63-72 ) katika uchunguzi wake alipata kuwa katika karibu riwaya zote matatizo ya kifamilia na nafasi ya mwanamke ni maudhui yanayosababisha matatizo makubwa kwa wahusika wa kike. Kwa hivyo, maudhui haya yanajitokeza kama motifu katika kazi hizi. Hali hii inadhihirika katika wahusika kama Maimuna katika *Utengano*, Semeni katika *Asali Chungu*, Asumini katika *Tata za Asumini* na Bi Kikuba katika ***Babu Alipofufuka***.

Kuhusu *Tata za Asumini*, anadai kuwa riwaya hii ni umbo la riwaya ya safari ya kisaikolojia kwa mhusika Asumini anayesononeka na kuteseka kimawazo. Asumini amepagawa na dhana ya usafi

aliyosindiliwa na wazazi wake kutoka utotoni kiasi kwamba anachukulia kukaribiwa na mwanamme kuwa ni uchafu. Ukweli huu unadhihirika katika kifungu hiki.

> Roho ya kiumbe huyu ilitakiwa itakaswe, lakini nje, ulimwengu ulikuwa mchafu unanuka. Ule ulimwengu ambao Asumini alikuwa akiishi ndani yake; ulimwengu aliokuwa akiishi kila mtu, lakini bado wazee wake wakang'ang'ania kumsuuza yeye tu. (Mohamed 1990:20 )

Hali hii ndiyo inayopelekea Asumini ayabane matamanio, matakwa na matumaini yake na kuyawekea kibano mpaka akashindwa kupenda, kuwasiliana na watu na kuishi ulimwenguni. Tajriba yake ya dhuluma za familia yake zinadhihirika mara kwa mara katika uzungumzinafsi ndani na mkondo wa ung'amuzi kama inavyoonekana katika kifungu hiki.

> Anajikumbukia Asumini, alipokuwa mdogo…Wazee wake walimwona kama kimalaika cha Mungu tu. Wakachukua juhudi kumlinda…Wakafuata miko…Mwanamke asivae hiki, asivae kile-Kwa nini?..Kwa nini awe mwanamke shetani peke yake? Asumini akazidi kujisaili..miaka yote hiyo, mpaka akapasuka. (Mohamed 2001:101-102)

Linalodokezwa na kifungu hiki ni hali za kisaikolojia za mhusika huyu kutokana na dhuluma alizoelekezewa.

Kuhusu ***Babu Alipofufuka***, anachanganua mhusika K ambaye ni mzazi wa kutojali mkewe na wanawe kutokana na ubinafsi wake. K ni mfano wa kiongozi wa Kiafrika aliye mfisadi na aliyeoza kimaadili. Anaishi maisha ya anasa na anatumia uwezo wake kujitajirisha. Kwa mujibu wa Traore, K anaingiliana na mabwenyenye wa kigeni na wenyeji na kusahau kabisa alikotoka. Mkewe anapodiriki kumkabili anasema ;

> Kila mtu na lake dunia hii… (Mohamed 2001: 67)

Usemi huu ni dhihirisho kuwa hisia zake za utu na uzazi zimekufa na kuchukuliwa na anasa za dunia. Ni katika hali hii K anapotokewa na mzuka wa babu yake. Mhusika huyu asiyeonekana anamlazimisha kutazama nyuma na kukumbuka alikotoka. Mzuka huu unampeleka katika safari ya kisaikolojia ya kutambua asili yake. Ni katika hali hii K anaposikika akiongea na mtu asiyeonekana na kuwashangaza wafanyikazi wake. Mwishoni mwa safari hii anagundua kuwa amekataliwa na maisha yake ya awali, yaani kazi amefutwa na mali yake yote imetwaliwa na serikali ya Proteus. Kwa mujibu wa Traore usawiri wa

mhusika K anayefikia mwisho wa kusikitisha ni motifu inayopatikana katika kazi nyingi za Said Ahmed Mohamed kama vile Makusudi katika ***Utengano***, Bwana Juba katika ***Kiza Katika Nuru*** na Fauz katika ***Dunia Mti Mkavu***. Ufichuzi huu ndio unaoonyesha kuwa ndoto ya mwandishi huyu ni kuangamizwa kwa mababe dume wanaowadhulumu wenzao na hasa wanawake wanaonyimwa haki zao.

Ingawa Traore anachunguza wahusika katika muktadha wa kifamilia katika jamii husika, ameonyesha namna ambavyo mifumo ya kifamilia na kijamii inavyowaathiri wahusika kisaikolojia. Kwa maana hii, uchanganuzi huu ulitusaidia kuchunguza umbuji wa wahusika na matukio yanayowapa hamasa kutenda wanavyotenda na athari ya vitendo vyao kwa wahusika wengine. Hata hivyo, kuna mapengo ya wazi katika uchunguzi wake kama ujenzi wa ploti kisaikolojia, usimulizi na mtindo.

Tulidurusu pia suala la muundo na mtindo katika riwaya ya ***Babu Alipofufuka.*** Muundo ni sura inayojitokeza katika kazi ya kifasihi inayohusiana na visehemu mbalimbali vinavyopatikana katika kazi hiyo. Kwa upande wake, mtindo ni namna mwandishi fulani ameunda matini kudhihirisha muundo fulani bainifu. Kuhusiana na mtindo, Olali (2010: 81-98 ) alichunguza riwaya ya ***Babu Alipofufuka*** kwa lengo la kubainisha muundo wake kimtindo. Anadai, riwaya hii inasimuliwa kwa viwango viwili: kiwango cha mhusika K na kiwango cha mzuka wa babu yake. K anapoingiliwa na mzuka wa babu yake, mambo yasiyo ya kawaida yanaanza kutendeka kama vile kutoweka kwa chakula cha mbwa, kuendesha, kuzungumza na mtu asiyeonekana na safari ya kisaikolojia ya K. Kwake yeye, kiwango cha mzuka ndicho kinachotufichulia hali halisi ambapo mzuka unatuorodheshea makosa ya K. Ufichuzi huu ni kama ung'amuzi wa maisha ya awali ya K. Kurejeshwa huku nyuma katika maisha asiyotaka kuyakumbuka ndiko anakodai mwanasaikolojia, Kriesteva kuwa kila binadamu hutaka kurejea alikotoka ingawa huteta sana anapokumbushwa na msukumo wa mauti.[11]

Katika uchunguzi wake, amebainisha matumizi ya mbinu kama uhalisiaajabu, sintaksia yenye nyufa, italiki, wino mzito, tashihisi, taswira, mbinu rejeshi na uzungumzinafsi ndani. Kwake, italiki na wino mzito zinalenga kuupa ujumbe nguvu na kuonyesha ukiukaji wa kaida na dunia iliyopasuka. Matumizi ya tashihisi anadai yanatumiwa kuonyesha kuwa katika dunia ya kisasa binadamu anategemea vyombo vya

kiteknolojia kiasi kwamba hawezi kuishi bila yavyo. Baadhi ya vyombo hivyo anavithamini kuliko binadamu wenzake. Matumizi ya mbinu hizi yanaweza kuzua fasiri mbalimbali kwa wasomaji kwa vile baadhi yazo ni tata na huenda asipate maana kwa njia ya moja kwa moja. Uchanganuzi huu unatufaa kwa vile baadhi ya mbinu anazozichunguza ndizo tunazotarajia kuzichanganua kama vile matumizi ya mbinu rejeshi, uzungumzinafsi ndani, uhalisiaajabu na sintaksia yenye nyufa ambazo zina mwelekeo mkubwa wa saikolojia ya wahusika. Hata hivyo, sisi tumepania kuzishughulikia kwa undani zaidi.

## 1.9 Mbinu za utafiti

Utafiti huu ulikuwa wa maktabani. Ili kutimiza madhumuni ya utafiti wetu, tulihusisha mbinu kadha wa kadha. Kwanza, tuliisoma riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke*** kwa uzingatifu mkubwa tuielewe barabara ili tuweze kuichanganua ipasavyo. Vilevile, tulisoma riwaya nyingine za Said A. Mohamed kama vile ***Utengano, Tata za Asumini*** na ***Babu Alipofufuka*** ili kuelewa mabadiliko na mwelekeo wake wa uandishi kutufanikisha kuihakiki kazi yake vyema. Tulizisoma riwaya nyingine za kisaikolojia kama vile ***Bina-Adamu!, Musaleo!, Msimu wa Vipepeo*** miongoni mwa nyingine kusudi tuelewe mbinu za kisaikolojia zilizotumiwa kuvidokeza vipengele mbalimbali vya kazi hizi.

Mbali na hayo, tulisoma maandishi yanayoelezea nadharia ya saikolojia changanuzi kama nguzo muhimu katika utafiti huu na uelewa wa undani wa nadharia ili tuwe na mwongozo bora wa kazi yetu. Aidha, tulidurusu na kuchunguza vitabu, makala na tasnifu zinazohusiana na utafiti wetu. Kwa kufanya hivyo utafiti wetu utakuwa na mawanda mapana ya kuchota ufahamu muhimu kuufanikisha utafiti wetu.

Hali kadhalika, tulizingatia ushauri ufaao kutoka kwa wahadhiri mbalimbali wa fasihi hasa kutoka kwa wasimamizi wetu. Aidha, ushauri wa wanafunzi wenzetu ulitufaa sana.

Mwisho, tulizingatia, kuzitafakari na kuziratibu data zilizokusanywa kwa utaratibu ufaao ili kutoa picha dhahiri ya riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke*** kama riwaya ya kisaikolojia.

## 1.10 Tanbihi

1. Kwa maelezo zaidi tazama Paris, B. J. ***A Psychological Approach to Fiction*** (1974). Bloomington: Indiana University Press. Uk:1

2. K.h.j. http://en.wikipedia.org/wiki/psychological novel

3. K.h.j. Olali Tom, "***Structure and Anti-structure of a Swahili Novel***" Katika The Nairobi Journal of Literature. No. 6 of 2010 uk: 83-92.

4. K.h.j. Wamitila K.W katika kazi yake, ***Kamusi ya Fasihi : Istilahi na Nadharia*** (2003) Nairobi: Focus. Uk: 298.

5. K.h.j. Uk: 139

6. K.h.j. Dorsch, T.S, ***Classical Literary Criticism***(1965). New York: Penguin. Uk:39-40

7. K.h.j. Kennedy na Gioia. ***Literature: An Introduction to Fiction, Poetry and Drama*** (2005).New York: Longman uk: 156

8. K.h.j. Mbatiah, M. ***Kamusi ya Fasih***i (2001). Nairobi: Standard Textbooks and Publishing. Uk: 29.

9. K.h.j. Mbatiah, M. k.h.j. uk: 85

10 K.h.j. Wamitila, ***Msingi wa Uchanganuzi wa Fasihi*** (2008).Nairobi: Vide~Muwa. Uk: 14-15

11. K.h.j. http://en.wipedia.org/wiki/psychoanalytic literary criticism

12. K.h.j. http://www.purdue.edu/guidetotheory/psychanalysis/pschimaframes.html

# SURA YA PILI

# MUUNDO NA WASIFU WA PLOTI KATIKA *NYUSO ZA MWANAMKE*

## 2.1 Utangulizi

Sura hii ina malengo kadha wa kadha ya kimsingi yakiwa ni pamoja na kuweka msingi wa mijadala tutakayoshughulikia katika utafiti huu. Inadhamiria kufafanua masuala ya kimsingi katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* kama riwaya ya kisaikolojia ya kisasa katika fasihi ya Kiswahili. Aidha, inakusudia kuonyesha jinsi msuko wa riwaya hii ulivyojengwa kwa mbinu za kudokeza hali za kisaikolojia za wahusika. Pamoja na hayo, tunakusudia kulifafanua suala zima la ploti, hasa kama linavyoeleweka na kutumika katika utafiti na katika fasihi ya Kiswahili kwa ujumla. Tulifanya hivyo kwa kuangazia, kuainisha na kuzijadili mbinu mbalimbali za ujenzi wa ploti kwa mkabala wa kuonyesha jinsi mbinu hizo zinavyochangia kuibuka kwa mitazamo ya kisaikolojia. Vilevile, tunaeleza kwa tafsili mbinu za saikolojia-simulizi na kuonyesha uamilifu wa mbinu hizo katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*.

## 2.2 *Nyuso za mwanamke* kwa muhtasari

Riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010) ni riwaya ya kisasa ya kisaikolojia iliyosanifiwa kwa ufundi na ubunifu wa kipekee na wa hali ya juu. Riwaya hii inazungumzia masuala ya mitagusano mseto ya kimaadili, kiuchumi, kijamii na kisiasa katika jamii ya Kisiwa cha Ungunja ambayo ndiyo jamii iliyomlea na kumkuza mwandishi wa kazi hii. Kazi hii inazungumzia maisha ya Nana, msichana anayejikuta katika mivutano ya kifamilia, kijamii, kitamaduni, kidini na kinafsi; anayeathirika na kubebeshwa makosa yaliyofanywa na wazazi wake hasa baba yake. Nana anapitishwa, anakutanishwa na kupitia katika hali nyingi ngumu za mateso na majaribu kabla hajajifahamu na kuifahamu jamii yake na nafsi yake. Juhudi zake zinaanza kubainika pale anapoanza kuzitambua hali hizi na jinsi zinavyohusiana na kuhimiliwa na mila na desturi za jamii yake, jamii inayomtukuza na kumpendelea mwanamume. Kwa ujumla, riwaya hii inamsawiri mwanamke wa jamii ya Kiafrika katika kipindi hiki cha utandawazi anayejaribu kujikwamua kutokana na minyororo ya kaida na desturi za kitamaduni.

Hadithi ya riwaya hii inaanza pale mapenzi yanapochipuka, kuota na kumea mizizi kati ya Faisal na

Bimkubwa. Mara tu mapenzi haya yanapoanza kushamiri, wazee wake Bimkubwa wanamchumbisha mume mwingine. Katika harakati hizo Faisal anahamia Abudhabi baada ya baba yake kuuwawa katika vita vya kung'ang'ania madaraka. Juhudi za Bimkubwa za kukataa mume aliyechaguliwa na wazazi wake hazifui dafu na anaishia katika ndoa ya kupangwa kwa kuolewa na Bwana Hila. Kule Abudhabi, Faisal anajitosa katika masomo ambapo anaendelea na masomo yake hadi kiwango cha juu sana na kisha anapata kazi katika benki. Kwenye benki anafanikiwa kupanda cheo hadi kuwa meneja mkuu. Baadaye anamwoa Bi. Matuka.

Ndoa ya Bimkubwa na Bwana Hila ilikuwa ya upande mmoja kwa sababu alifungiwa ndani kama mfungwa na hakupewa uhuru wowote. Walijaliwa kuzaa binti mmoja, Nana. Baada ya Bimkubwa kuvumilia sana alijaribu kumwua mmuwe kwa kumtilia vipande vya chupa katika chakula, tendo ambalo lilifanya apewe talaka. Bimkubwa aliwahi kuolewa tena na wanaume wawili, yaani Simai na Selemani Kijogoo lakini ndoa zote zilijaa balaa tupu. Ndoa yake ya tatu ilimpata kama akili zake zimevurugika kiasi cha kutokuwa timamu na kutokana na utumwa aliotumikishwa na Selemani siku moja aliamua kumchinja mumewe. Kitendo hiki kilifanya ashikwe na kushitakiwa kwa mauaji lakini baada ya kupimwa na daktari wa wagonjwa taahira aligunduliwa kuwa na ugonjwa wa akili. Alifungiwa katika hospitali ya wendawazimu hadi ilipobainika kuwa akili yake ilikuwa timamu.

Kule Abudhabi, mbali na kuwa Faisal alikuwa ametajirika na kuwa na familia, moyo wake haukuwa kule kwa sababu ya mapenzi yake kwa Bimkubwa. Kwa hivyo, aliamua kuacha kazi na baada ya kumkabidhi kijana wake na bibi yake jukumu la kuendesha biashara yake aliabiri chombo kuja Ungunja kumsaka Bimkubwa. Usasi wake wa Bimkubwa haukufua dafu kwani uliishia katika jaribio la kuawa na Bimkubwa. Aliwahiwa na wasamaria wema waliompeleka hospitalini alikotibiwa na hatimaye akapona.

Baada ya Faisal kutoka hospitalini alianza kuishi na akina Bi, Chuma na Bi. Mau. Akiwa kule alianza kazi ya uimbaji tendo ambalo linatokana na ubanaji wa mapenzi yake kwa Bimkubwa. Ni wakati huu ambapo Nana anakutana na Faisal akiwa anaimba barabarani. Uimbaji wa Faisal ulimvutia Nana na kumnasa kiasi kwamba hakumbanduka. Kwa upande wake, Faisal anavutiwa na mwanamwali huyu kwa kumnasibisha

na Bimkubwa.

Bimkubwa alipotalikiwa na Bwana Hila alinyang'anywa mtoto wake na hakuruhusiwa kumwona tena. Kwa hivyo Nana alikuzwa na baba yake mzazi na mama wa kambo. Kama ilivyokuwa kawaida ya wazazi wakati ule, Nana alizuiliwa kutangamana na watoto wengine wa hirimu yake hasa wavulana kwa kuhofia kuchafuliwa. Hata hivyo, alipewa chochote alichohitaji kutokana na utajiri wa baba yake. Alipelekwa shule na alionyesha maendeleo mazuri kwa kuibuka mwanafunzi bora nchini mwake. Ilipokuja kwenye kuchumbiwa mume, baba yake alimchagulia mchumba bila ya hiari yake lakini Nana alimkataa. Mambo yalimharibikia Nana alipomkaribisha Faisal katika sherehe ya kuadhimisha siku ya kuzaliwa kwake ambapo baba yake alimkasirikia na akampiga kibao. Hapo ndipo Nana aliamua kutoroka nyumbani kwao na Faisal.

Alipotoroka alikaribishwa kwa akina Bi. Mau na Bi. Chuma ambao walikuwa nyanya mkuu na nyanya mtu wa Nana. Wenyeji wake walikuwa wakarimu kwa kila mtu hata wale wasiowajua mbali na kuwa walikuwa watu ambao hawakujipata vizuri. Alipokuwa anaishi huko alijifunza kuosha, kufua, kufagia na kupika pamoja na kuimba alikofunzwa na Faisal. Aliinukia kuwa na kipawa cha kuimba hata wakati mmoja aliposhiriki katika majaribio ya kumchagua mwimbaji atakayekuwa anawatumbuiza wateja katika Hotel Selwa, aliibuka wa kwanza. Hata hivyo, kwa kuwaza tena alikataa kuajiriwa kwa mshahara ambao haukuwa mdogo kwa kuhofia kudhibitiwa na wanaume hasa baada ya kuambiwa kuwa alistahili kuimba nyimbo za mipashio na matusi pamoja na kuvaa vazi fupi, jambo ambalo halikumpendeza. Hata ingawa hakutaka msaada wa wanaume alikuja kugundua kuwa hangetimiza azma yake ya kuanzisha taarab bila pesa. Ugunduzi huu ulimtatiza sana kiasi cha kumdidimiza kwenye kibuhuti.

Baada ya tukio hili Nana alikuja kukumbushwa na sauti ya mzuka wa mama yake kukifungua kibegi alichoachiwa na mama yake alipofariki na alipofungua alishangaa kupata hundi ya shilingi milioni tisini. Kutokana na pesa hizo alianzisha bendi ya taarab, kituo cha redio na runinga katika jumba kubwa la ghorofa kumi na moja lililoitwa *Karibu Mwanamke* alilolijenga mwenyewe. Alionyesha bidii katika

biashara yake hali iliyofanya biashara hiyo ipanuke sana. Katika neema aliyopata Nana alipania kuwainua wanawake wanyonge na wanaume maskini kiuchumi.

Ingawa Nana alijitunza asichafuliwe na wanaume, baadaye alikuja kusalitika na penzi la mwanawe Faisal, Amour na wakafunga ndoa. Tukio la Amour kumwoa Nana lilimkosesha Faisal mwenzi wa karibu aliyemhusisha na Bimkubwa na akamwenzi kama alivyomwenzi Bimkubwa. Kwa sababu hiyo alihamia Morishas ambako alimkuta Suria mwanawe Bimkubwa aliyemzaa alipobakwa na mwajiri wake Subash. Kule Morishas Faisal aliendeleza usuhuba na Suria kama ule uliokuwepo kati yake na Nana. Aidha, anatudokezea azma yake ya kurudi nchini kwake na Suria. Kwa hivyo, anaonyesha tumaini la kuanza upya maisha yake.

Kwa ujumla hadithi hii ni safari ya kisaikolojia ya Nana na Faisal ya kutafuta uhuru, haki na mapenzi. Katika safari hii Nana anaonyesha ukuaji kimawazo, kihisia, kitabia na kiuchumi. Kwa njia hii Nana anaibuka kuwa mwakilishi wa wanawake wa kisasa walioelimika na wanaojipata vizuri katika jamii. Kwa upande wake, Faisal anaonyesha udidimifu kimawazo, kihisia na kitabia. Hadithi hii pia ni akisi ya mabadiliko ya kijamii yanayoonyesha upanuzi wa riwaya ya Kiswahili kujumuisha masuala ibuka kama usawa wa kijinsia, haki za watoto na haki za kibinadamu.

## 2.3 Dhana ya nyuso za mwanamke

Katika riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke*** mwandishi anampitisha msomaji katika mandhari na miktadha anuwai ya kijamii ambapo anapata fursa ya kusawiri nyuso mbalimbali za mwanamke katika jamii yake. Nyuso kwa mujibu wa maelezo ya kamusi ya TUKI (2004: 444) ni wingi wa neno uso lenye maana ya sehemu ya mbele ya kichwa kati ya kipaji na kidevu. Uso ndio wajihi wa mtu, yaani sehemu inayotambulisha mtu. Kwa hivyo uso ni sehemu muhimu sana ya mwili. Kwa mujibu wa kazi hii nyuso za mwanamke ni dhana pana inayotumiwa na mwandishi kuwasilisha na kuzungumzia taswira mbalimbali zinazojitokeza katika maisha ya wanawake, kama wanavyowakilishwa na wanawake wa jamii ya mwandishi. Taswira hizi zinaibuka kutokana na mambo wanayopitia katika miktadha halisi ya kitamaduni, kimaadili, kisiasa, kijamii na kiuchumi kwa kadri miktadha hiyo inavyohimiliwa na kanuni za kitamaduni

na kidini. Uhalisi huu unadhihirika katika maelezo ya mwandishi pale anaposema;

> ..Kila mwanamke alikuwa na uso wake. Nyuso za vigori zinazoonyesha hilaki mapema kabla hata ujanajike haujafumbuka na kunawiri katika nafsi zao. Nyuso za wanawari zinazosawijika baada ya kubigijwa na kukabwa na kubakwa. Au zinazotazamiwa kuozwa wanaume mapema...Nyuso za walioolewa zinazosinyaa kwa joto kali la ndoa hata kabla ya ndoa yenyewe haijasimama vizuri. Nyuso za wanawake wanaonyang'anywa mirathi yao, kwa sababu tu wamezaliwa wanawake....Nyuso na nyuso na alkuki ya nyuso za wanawake. Mohamed (2010: 183)

Kutokana na maelezo haya ni wazi kuwa mwanamke amesawiriwa kwa njia zinazomwezesha kuwakilisha nyuso anuwai. Katika uanuwai huo wa nyuso kunajitokeza aina nne za nyuso zinazoakisi awamu mbalimbali za maisha ya mwanamke katika jamii. Uso wa aina ya kwanza ni uso wa watoto wasichana ambao katika udogo wao hudhibitiwa na kuchungwa kama wafungwa, jambo ambalo hufanywa kwa madai kwamba hivi ndivyo kaida za kijamii zinanvyoelekeza malezi kwa kutowaruhusu watoto wasichana kutangamana na wavulana. Hii ndiyo sababu inayofanya Nana kupelekwa shuleni kwa gari na kurudishwa kwa gari ili asipate fursa ya kukutana na wavulana njiani. Aidha, kuna uso wa wanawali unaotokana na wao kutopewa uhuru wa kujichagulia wachumba huku wengine wakibakwa. Hali hii inawafanya wateseke ndani kwa ndani. Mifano ya hali hizi ni kama vile Nana kuchaguliwa mume na babaye, Mwanamkuu na Fatuma kunajisiwa na wajomba wao na Hawa kuuliwa kitoto chake baada tu ya kukizaa. Ni visa vya aina hii na vingine vinavyowafanya wanawali hawa wawe na nyuso zinazoonyesha huzuni, zenye vilio na ishara za maumivu ya ndani kwa ndani. Mfano mzuri wa hali inayowakumba wanawari ni mazungumzo kati ya Mwanamkuu na Nana.

> U wapi? U wapi?
> "Unatafuta nini Mwanamkuu?" aliuliza Nana.
> "Natafuta n'nachotafuta milele, kile ambacho nilinyang'anywa nilipokuwa mtoto mdogo na mjomba wangu." Mohamed (2010: 178)

Mazungumzo haya yanaonyesha jinsi wasichana wanavyodhulumiwa, ambapo kinachosikitisha ni kwamba wanadhulumiwa na jamaa zao wa karibu, watu ambao wanafaa kuwalinda badala ya kuwatenda hivyo. Baada ya wanawari hawa kutendwa hivyo wanabebeshwa hisia za hatia na wanaangaliwa na kulaumiwa

kana kwamba maovu waliyotendwa wamejitakia wenyewe. Wananasibishwa na mashetani na kuchukuliwa kuwa matambara mabovu. Matukio ya aina hii ndiyo yanayofanya wahusika hawa wasawiriwe kama wahusika wanaotatizika kisaikolojia.

Kuna tena uso wa aina nyingine uwakilishao nyuso za wanawake walioolewa. Huu ndio uso unaodhihirishwa na wanawake kama vile Shemsa, Bi. Matuka na Bimkubwa. Uso huu unatokana na maisha ya usumbufu yanayowakumba wanawake katika ndoa kama vile kufanywa watumishi wa waume zao, kufungiwa ndani, kuzuiwa kufanya kazi za ajira, kupigwa na kufanywa "mke" wa jamii yote. Uso huu wanaodhihirisha ni uso uliojaa vilio, manung'uniko na unyonge. Mfano mzuri unatolewa na Shemsa katika kauli ifuatayo;

> "..hakunifanya mke tokea mwanzo. Alinifanya mtumishi wa familia yake kubwa,...Na si kupika tu, bali kufua, kupiga pasi, kufagia, kutandika na kutandua. ....Sadiki alitaka... alitaka...aaa, siwezi...siwezi kusema! " K.h.j (uk: 211)

Mfano huu wa Shemsa kutumikishwa katika kila aina ya kazi ili kuistarehesha familia kubwa kiasi kwamba hata inaelekea alitakiwa awahudumie wote kwa ngono pia ni ithibati ya jinsi mila, desturi na kaida za jamii hii zilivyomdhalilisha mwanamke. Kwa ufupi hizi ni desturi na kanuni ambazo zinaifanya taasisi ya ndoa kuwa ya utumwa.

Kwa kiasi kikubwa aina hii ya uso wa wanawake walioolewa unadhihirishwa na Bimkubwa katika hadithi yake ya ndoa. Kulingana na Bimkubwa maisha ya ndoa yanadhihirisha karibu nyuso tatu za mwanamke katika ndoa. Uso wa kwanza ni ule anaopata katika ndoa yake ya kwanza (uk: 287). Katika ndoa hii uso wake ni wa mfungwa asiye na uhuru na mwenye upweke. Hali hii ndiyo iliyofanya akili zake kuvurugika kiasi cha kutaka kumwua Bwana Hila. Uso wa pili wa Bimkubwa unadhihirika anapoolewa na Simai (uk: 287-288). Katika ndoa hii uso wa Bimkubwa ni wenye uvimbe na mabaka kutokana na kupigwa kila kuchao. Namna uso ulivyokuwa na wajihi wa uvimbe na mabaka ndivyo moyo pia ulivyokuwa na uvimbe na mabaka ya ndani kwa ndani. Nao uso wa tatu unajitokeza wakati Bimkubwa anabakwa na Subash dukani mwake (uk:288-289). Tendo hili linamfanya ashike mimba na akazaa mtoto ambaye

alinyang'anywa baada ya siku arobaini tu. Juhudi zake za kupata haki zinaambulia patupu na anabaki na uso wa unyonge. Kwa maoni yetu uso wake wa nne ni ule unaodhihirika anapoolewa na Selemani Kijogoo (uk:290-291). Katika ndoa hii anadhihirisha uso usio na aibu, matumaini na hisia zozote. Ni wakati huu aligeuka kuwa mwehu. Ni uso huu unaodhihirisha upeo wa kudidimia kimawazo, kitabia na kihisia na ambao si hatari tu kwa mwanamke bali kwa wanaume pia. Ni hali hii ya kuporomoka ndani kwa ndani inayomfanya Bimkubwa kumwua Selemani na kumjeruhi Faisal. Kwa hivyo, jamii inafaa impe mwanamke uhuru na haki za kimsingi kama ilivyo kwa mwanamume ili ijiepushe na madhara kama tunayoshuhudia katika kisa hiki.

Hali kadhalika, kunao uso wa wanawake wanaonyang'anywa mirathi yao kwa sababu tu ya kuzaliwa wanawake. Mfano mzuri ni wa Bimkubwa kunyimwa fursa ya kuwalea binti zake Nana na Suria kama inavyoonekana katika kifungu hiki.

> Alipokwisha kumzaa mtoto na kukoga arobaini, siku moja aliingiliwa ndani ya nyumba na watu asiowajua na kile kitoto chake kikachukuliwa na hakukiona tena maishani mwake. K.h. j (uk:289)

Katika jamii inayosawiriwa na kazi hii, inaelekea watoto walikuwa mali ya wanaume na wanawake hawakuwa na sehemu katika umiliki wao kwani waliangaliwa kama chombo tu cha kuwaleta watoto duniani. Katika hali hii wanawake waliotalikiwa kama Bimkubwa walioonekana kama tasa hata ingawa walikuwa wamezaa watoto. Kwa sababu hii waliishi maisha ya upweke kama alivyoishi Bimkubwa kwenye mahame hadi kifo chake.

Kwa maoni yetu Nana ndiye anayeibuka kuwa na uso uliojaa matumaini kutokana na juhudi zake za kujikomboa kutokana na desturi za kijamii na ubabe wa wanaume. Baada ya kutoka kwao anaanza kuonyesha uso wa furaha kutokana na uhuru aliopata kwa wenyeji wake kama anavyosema mwenyewe katika kifungu kifuatacho;

> Nikakunjuka ndani na nje ya nafsi yangu. Nikajihisi nimekuwa mkamilifu hatimaye. Kiumbe huru wa mwili na mawazo yangu ... Mohamed (2010: 93)

Nana ana furaha na uhuru mpya aliopata na anadhihirisha uso wa furaha. Ni mabadiliko haya kiuso yanayompa msukumo na matumaini ya kujifunza mengi katika mazingira yake mapya kama vile kufanya kazi za nyumbani, kuimba na kufanya biashara. Anapofaulu anadhihirisha uso wa ujasiri, matumaini na utulivu.

Hata hivyo, si wanawake tu wanaodhihirisha nyuso anuwai katika jamii hii bali hata wanaume. Sababu hapa ni kuwa athari inayowasababishia wanawake kuwa na nyuso nyingi pia inawakumba wanaume. Kwanza, kuna mhusika Faisal anayedhihirisha uso wa hamaniko la mapenzi na ukinaifu wa maisha ya ndoa yake. Kutokana na hali hii anaacha kazi ya maana na familia yake kuja kusaka mapenzi ya Bimkubwa. Kama babaye, Amour anadhihirisha nyuso mbalimbali. Anapokuwa kwao Abudhabi anaonyesha uso wa ukinaifu wa maisha na ingawa anajizika katika biashara ya babaye ili kuridhi matakwa yake anafanya hivyo kwa desturi tu; kwanza kwa kumkosa baba yake na pili kwa kukosa mapenzi ya mwenzi. Anabadilisha mambo haya na juhudi kubwa katika kuendeleza biashara ya babaye. Tabia hii inaingiliana na dhana ya Freud (1957: 153) ya ubadilishaji matamanio inayodai kuwa kama matamanio ya mtu yanabanwa hurejelea hali nyingine kujaza matamanio waliyokosa. Aidha, anaonyesha uso mwingine anapomsaka Nana kwa mapenzi: uso uliojaa hamaniko na wasiwasi ya kumkosa Nana kwa kugundua kuwa anapendwa na baba yake pia. Kwa hivyo Nana anamwona kama mtu wa nyuso nyingi. Kwa maana hii hivyo basi namna wanawake wanavyodhihirisha nyuso anuwai ndivyo athari zake zinavyosambaa na kuwaathiri wanaume kitamaduni, kihisia, kimaadili na kimawazo.

Ni muhimu pia kueleza kuwa kudhihirika kwa nyuso mbalimbali hasa zinazotona maumivu na mizigo wanayobebeshwa wanawake zinaonyesha ubanaji wa matarajio na matamanio yao katika maisha yao. Ubanaji huu kama anavyodai Freud (k.h.j: 147) unawapitisha katika hatua mbili muhimu. Kwanza, ni kule kuzuiliwa kwa matamanio yao katika ung'amuzi na kila mara hutaka kutoka. Katika hatua hii mwathiriwa anaweza kujimudu kwa mambo mengi. Hii ni hatua anayodhihirisha Nana na ndio sababu hakuweza kudidimia mpaka mwisho kwani aliweza kujipata kwa kujikwamua kiuchumi na kimawazo. Hatua ya pili ni ubanaji kamili ambapo baada ya matamanio yao kubanwa kabisa hutamani na kuvutiwa na kila kitu

kinachohusiana na kile kilichobanwa na huenda asirejelee matamani hayo. Hii ndiyo hatua inayodhihirishwa na Faisal ambaye anamwenzi Nana kwa kumkosa mama yake. Hatua hii wakati mwingine huonyesha hali ya kudidimia kimawazo, kihisia na kitabia kiasi cha kuporomoka kabisa kwa maisha ya mhusika. Kwa mfano, Bimkubwa katika kazi hii na Asumini katika ***Tata za Asumini*** ambao wanakuwa wendawazimu na kuangamia.

## 2.4 Mbinu za kisaikolojia za ujenzi wa ploti

Ploti au msuko ni kipengele muhimu cha muundo wa matukio katika kazi ya kifasihi. Aristotle (1965: 39) alitambua umuhimu wa ploti kwa kusema kuwa kati ya vipengele vya tanzia kilicho muhimu sana ni ploti. Kwake ploti ni mpangilio wa matukio na uhai wa tanzia, yaani matukio ya furaha na huzuni. Anachosema ni kuwa ploti ndiyo roho ya tanzia kwa maana kuwa ndicho kipengele cha kimsingi cha kazi ya kifasihi. Hata hivyo, matukio katika ploti hupangwa kiusababishi ili kuunda kiunzi chenye umoja na mahusiano. Wamitila anaieleza ploti kwa utoshelevu kwa kusema kwamba;

> Ploti ni mfuatano wa matukio yanayopatikana katika kazi ya kifasihi kwa kutegemea uhusiano wake kiusababishi. (2002:6)

Anachosema ni kuwa ploti ni mpangilio wa matukio ambapo tukio moja linasababisha lingine. Usababishi huu ndio mara nyingi unazua taharuki kwa msomaji na kushikilia hamasa yake kuendelea kusoma hadi mwisho. Kwa upande wake, Katie (2001: 300) anaongeza kuwa ploti inaweza kuwa sahili au changamano. Usahili au uchangamano huu wa msuko unatokana na kazi ya kifasihi kusheheni matukio mengi pamoja na matumizi ya mbinu elekezi na mbinu rejeshi. Kuwepo kwa mbinu nyingi za ujenzi wa ploti kama vile ndoto na uzungumzinafsi kunaweza kufanya ploti kuwa changamano.

Ploti huwa na muundo mahsusi ambao huwa na mwanzo, kati na mwisho.[1] Ikiwa matukio yamepangwa kiwakati ploti inaweza kusemwa kuwa sahili lakini ikiwa yamepangwa kwa kwenda mbele na kurudi nyuma ploti itakuwa changamano. Huku kurudi nyuma na kwenda mbele ndiko tulikotaja kuwa mbinu rejeshi na mbinu elekezi mtawalia. Kwa mujibu wa Henderson n.w. (1994: 11) mwanzo wa kazi ya kifasihi si lazima uwe mwanzo wa tendo. Hali hii huwezeshwa na mbinu ya urejeshi na uelekezi.

Aidha, kuna msuko unaoanzia katikati ya hadithi ambapo tunaingia katika hadithi kwenye tukio muhimu. Baada ya hapo mwandishi hukunjua hadithi kwa kuturejesha nyuma kujaza matukio ya mwanzo. Kwa njia hii, yeye huzua taharuki inayomfanya msomaji atake kujua yaliyotendeka mwanzo na yanayofuatia. Mbinu rejeshi[2] ambayo ni mbinu ya kusimulia visa vilivyotokea kabla ya tukio lililopo hutumika. Katika riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke*** mwandishi ametumia ploti ya mpangilio huu kwani kisa kinapoanza tunamwona Faisal akiwa katika harakati za kumsaka Bimkubwa (uk: 1-17) ambacho ni kisa cha katikati ya hadithi. Ili kutudokezea yaliyotokea mwanzo ameutumia mzuka wa Bimkubwa katika fikira za Nana kutujuza yaliyotokea mwanzo (uk:287-292) na ndoto za mchana za Faisal. Huu ni mwelekeo mkubwa wa kisaikolojia kwa sababu visa hivyo ni sehemu ya ndoto zao za kimawazo.

Ni sharti ieleweke kuwa ploti si mfuatano tu wa matukio usio na uamilifu wowote katika kazi ya kifasihi. Aristotle (K.h.j. uk:40) anaiona ploti kama roho ya tanzia kwa maana kuwa ndiyo injini ya kazi ya kifasihi. Katika ***Nyuso za Mwanamke*** usukaji wa matukio wanamoshiriki wahusika unaonekana kuchukua nafasi kubwa kwani ploti ndiyo inayoendesha vipengele vingine vya matini.

Ploti kwa mujibu wa Forster (1974: 60) hulenga kuleta athari kwa msomaji inayotokana na taharuki ambayo matukio yanazua katika mpangilio wake. Athari hii hufanya msomaji ahuzunike, ajihurumie, achukizwe au afurahie. Kwa mfano, tukio kuu linalojitokeza katika riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke*** ni mwanamke kunyimwa haki na uhuru wa kujiamulia. Suala hili lilikusudiwa na mwandishi kumwathiri msomaji kwa kumfanya atathmini namna anavyowatendea wanawake katika jamii yake.

Aidha, Katie (2001: 300) anadai kuwa ploti husaidia kudokeza majukumu ya wahusika na matukio muhimu. Ni kupitia mpangilio wa matukio tunaweza kujua majukumu mbalimbali ya wahusika na pia kubaini matukio yaliyokuzwa zaidi ya mengine. Ni kutokana na matukio haya yaliyokuzwa zaidi tunapata maudhui muhimu yanayojitokeza katika kazi fulani. Kwa mfano, katika riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke*** matukio yaliyokuzwa ni yale yanayoonyesha namna wanawake wanavyodhulumiwa kwa kubakwa, kunyimwa uhuru wa kujichagulia na kupigwa na waume wao. Kwa upande wake, majukumu ya wahusika hasa wa kike ni kupiga vita dhuluma hizi kwa kukiuka kaida za kijamii kama vile Nana alivyofanya.

Mbali na hayo, ploti hulenga kuleta taharuki, msisimko na mshtukizo. Kulingana na Wamitila (2002: 6) taharuki ni ile hali ya matarajio ambapo msomaji huwa na hamu ya kutaka kujua kitakachotokea baadaye. Hali hii hutokana na umbuji wa kazi ya kifasihi unaozua msisimko katika mpangilio wa matukio ya kazi ya kifasihi. Kwa mfano, kifungu kifuatacho katika riwaya hii kinaweza kudokeza hali hii.

> "Hodi."
>
> Kimya.
>
> "Hodi."
>
> Makali ya upanga...
>
> Ajabu-hakutambua amefika vipi hapo, au vipi usukani wa nafsi yake umemwongoza hapo. Kasafiri ndiyo. .... (Mohamed 2010: 1)

Msomaji yeyote atakuwa na hamu ya kutaka kujua ni nani anayepiga hodi na anachosaka na kitakachotokea baada ya hapo.

Kwa kuhitimisha sehemu hii, ni muhimu kutaja kuwa ploti hujengwa kwa mbinu anuwai. Katika data yetu mbinu ambazo tunataka kuzijadili ni kama vile uzungumzinafsi, uzungumzinafsi wa ndani, dayolojia ya ndani, mkondo wa ung'amuzi, mbinu rejeshi, ndoto, nyimbo na barua.

### 2.4.1 Uzungumzinafsi

Mbinu hii kwa mujibu wa Mbatiah (2001: 109) inarejelea hali ambapo mhusika anazungumza peke yake au anatoa hotuba kwa hadhira. Wakati mwingine uzungumzi huu unaweza kuwa mrefu au mfupi. Suala la kimsingi ni kuwa uzungumzi wa aina hii unaweza kusikika na wahusika wengine au na hadhira ikiwa ni katika fasihi simulizi au usisikike. Katika riwaya hii mfano ufuatao unaonyesha hali hii;

> Hapo tena alimkumbuka marehemu baba yake...Hakusema kwa hakika, alinung'unika.."Usisikie wewe nguvu ndizo zinazotawala kila siku. Lakini nguvu zozote hazidumu milele, kwani nyumba ya nguvu moja huja ikakaliwa na nguvu nyingine. "... Halafu akaendelea."Kila nguvu ni kama mwambangoma. Kwani kila siku mwambangoma huvutia kwake. Kwa sababu hii kila nguvu ina sehemu ya kuharibu. Lakini nguvu haidumu. Haitambi milele. Na inapokuja nguvu mpya huisukuma nguvu kongwe, uharibifu huwa maradufu ..." Mohamed (2010: 9)

Mhusika Faisal anazungumza peke yake kwa kunung'unikia kifo cha baba yake. Hamzungumzii mtu maalum lakini uzungumzi wake unatuonyesha namna alivyoemewa na kumbukizi za kuuliwa kwa baba yake katika mapinduzi. Uzungumzi huu pia unatuonyesha hisia kali na za huzuni anapomkumbuka baba yake. Jukumu la mbinu hii ni kuonyesha mawazo na visa ambavyo vimewakumba wahusika maishani na kwa njia hii kusaidia kujenga msuko na uhusika wa ndani. Kuna aina mbili ya uzungumzinafsi. Nazo ni uzungumzinafsi ndani na dayolojia ya ndani.

### 2.4.1.1 Uzungumzinafsi Ndani

Kwa mujibu Katie (1986: 217) uzungumzinafsi wa ndani ni dhana inayodhihirisha mchakato wa mawazo ya wahusika ya moja kwa moja. Maelezo haya hayatuelezi namna ambavyo mchakato wa mawazo haya hutokea. Mbinu hii ni aina ya uzungumzinafsi inayodhihirisha mazungumzo ya nafsi ya mhusika au na mtu asiyeonekana kama vile mzuka, shetani au malaika anayeonekana. Kwa maoni yetu, uzungumzinafsi wa ndani husikika tu na mhusika anayehusika na uzungumzi huo. Aidha, uzungumzinafsi wa ndani huhusishwa na mazungumzo ya upande mmoja ambapo mhusika huzungumza na nafsi yake au na mtu asiyeonekana bila majibizano. Kama anavyoongezea Katie, mbinu hii hubainishwa na kiwakilishi cha nafsi ya kwanza na njeo iliopo. Katika data yetu mfano ufuatao unathibitisha ukweli huu;

> N'najua upo, ingawa wanasema umekwenda safari is'o marejeleo. Mimi siamini hivyo lakini. Japo sikuoni, ninakuhisi kwa ngozi yangu. N'najua hujenda moja kwa moja. Kabla ya kuingia msalani usiku, huona mlango unafunguliwa. Ndipo tena hukifuma kivuli chako haraka kinatoka msalani na kisha kutoweka ombweni. ... Mohamed ( K.h.j. uk:18)

Hapa kiwakilishi cha nafsi ya kwanza ni -ni- na kibainishi cha njeo iliopo ni -na-. Kifungu hiki ni mazungumzo ya Nana juu ya kumbukizi za mama yake. Nana anaongea na mzuka wa mama yake kana kwamba anaonana naye ana kwa ana. Kifungu hiki kinaibua hisia za huzuni, upweke na hamaniko na kinamfanya msomaji amhurumie Nana mbali na kuzua taharuki. Aidha, kinadhihirisha namna ambavyo mwandishi ameonyesha dhima ya upekuzi na upenyezi wa fikira za ndani za wahusika. Kwa njia hii kuna ithibati ya kutosha ya mwingiliano mkubwa na mawazo ya Wamitila K.h.j kuwa riwaya ya kisaikolojia huwa na mwelekeo wa kuchunguza undani wa mhusika au saikolojia yake.

Hali kadhalika, mbinu hii kama anavyotaja Katie (K.h.j.) huwa na matumizi ya jazanda. Istilahi jazanda inarejelea matumizi ya picha au taswira.[3] Taswira hutokana na maelezo yenye mtiririko fulani wa mawazo unaochora picha fulani katika fikira za msomaji. Taswira pia zinaweza kutokana na matumizi ya tamathali za usemi kama vile tashbihi na sitiari. Katika kazi hii taswira kwa nafasi kubwa zimetokana na mkurupuko wa mawazo yanayompitikia mhusika kama inavyoonekana katika kifungu kifuatacho;

> " Ilipovaa Abudhabi kanzu mbovu na vilemba vichakavu, ilipokwenda miguu chini juu ya ardhi kavu, iliposhindwa kujiendesha yenyewe, ilihitaji wasomi wengi hata wawe wametoka wapi. Seuze mimi Faisal niliyetoka nchi iliyowahi kuwapokea Waarabu kwa huruma hapo awali. " Mohamed (2010: 151)

Haya ni mawazo yanayompitikia Faisal anapokumbuka nchi ya Abudhabi. Taswira inayojichora ni ya nchi iliyogubikwa na uchakavu na uozo wa miundomsingi na umaskini wa vitu vyote. Si wataalamu si raslimali. Taswira hii inazua hali ya uhitaji wa uegezaji na hisia za kushindwa kwa wakati mmoja. Katika mfano huu kumetumika alama za kunukuu kuakisi namna Faisal anavyozungumza tu peke yake. Aidha, kifungu hiki kinaonyesha namna ambavyo mhusika huyu alivyojawa na mawazo tele ya maisha yake ya awali na kwa hivyo yeye ni mtu wa ndoto za jana katika maisha ya leo.

Kwa maoni yetu mbinu hii ndiyo mbinu msingi iliyotumiwa katika ujenzi wa ploti katika riwaya za ***Bina-Adamu!*** na ***Musaleo!*** Tofauti iliopo kati ya matumizi ya mbinu hii katika riwaya hizi na ***Nyuso za Mwanamke*** ni kuwa katika ***Nyuso za Mwanamke,*** matumizi ya mbinu hii yamefungamana na mbinu nyingine kama vile dayolojia ya ndani, ndoto, barua na kadhalika. Hii inaonyesha namna riwaya za kisaikolojia zinavyoingiliana kiploti na kuwa usanii wa kazi hizi unachangiana na kukamilishana.

Uzungumzinafsi ndani ni mbinu ya ujenzi wa ploti kwa sababu inadokeza matukio na mawazo muhimu katika msuko wa ***Nyuso za Mwanamke*** katika fikira za mhusika. Mbali na hayo, mbinu hii ni ya kisaikolojia kwa sababu inatudokezea anayowaza na anavyohisi na kwa hivyo tunaweza kujua undani wake. Vilevile, kutokana na mawazo yake na hisia zake tunaweza kubaini namna alivyoathirika na mambo yanayomkumba. Kwa njia hiyo, tunaweza kuelewa tabia zake.

Namna ambavyo mbinu hii imetumika katika kazi hii inaonyesha uchangamano mkubwa kwa njia ya kudokeza mawazo hai ya wahusika kwa njia ya kipekee. Kwa matumizi ya mbinu hii mwandishi ameonyesha jinsi riwaya ya kisaikolojia inaendelea kukua na kubadilika.

### 2.4.3 Dayolojia ya ndani

Kulingana na Katie (k.h.j. uk: 218) dayolojia ya ndani inarejelea mchakato wa mawazo kama mjadala kati ya sauti bainifu zikiwa ni sauti za mhusika au zilizo katika fikira zake. Katika hali hii kuna mvutano mkubwa wa kimawazo ndani ya mhusika huyu kama dhihirisho kuwa anakumbwa na vita vya ndani kwa ndani. Mvutano huu unashuhudiwa tu na mhusika peke yake. Mfano mzuri unajitokeza katika dondoo hii.

> Na hapo huzuka ule mjadala unaoendeshwa na sauti zake mbili ....
> Kwa nini jamii za wanadamu ziende namna hii?
> Kwa sababu zinaendeshwa kwa kiu ya vitu.
> Kwa nini jamii lazima iige mabaya kila siku?
> Kwa sababu ndani ya ukweli wetu hatujali mazuri.
> Kwa nini jamii yetu lazima ifuate matakwa ya watu wengine?
> Kama haikufuata itakiona cha mtemakuni. Cha mtemakuni kipi?
> Walichokiona Wa-Vietnam, Wa-Misri, Wa-Kambodia. ... Mohamed (K.h.j. uk:214)

Linalodokezwa ni hali ya kuchukizwa kwa Nana na jamii ilivyo kwa kuongozwa na tamaa pamoja na kuiga mabaya kwa maslahi ya nchi zilizoendelea. Huu ni mjadala kati ya nafsi mbili za Nana ushahidi kuwa anatatizika ndani kwa ndani na mfumo mzima wa jamii yake hali inayoingiliana na juhudi zake za kuibadili jamii yake. Katika riwaya ya ***Babu Alipofufuka*** dayolojia ya ndani inadhihirika pale ambapo mhusika K anazungumza na mzuka wa Babu jambo linalomfanya aonekane kama mwendawazimu mbele ya wafanyikazi wake kwa kuzungumza na mtu wasiyemwona (uk:70-72). Hata hivyo, katika ***Babu Alipofufuka*** inajitokeza tu katika mhusika mmoja K tofauti na ***Nyuso za Mwanamke*** ambako inajitokeza katika wahusika kadhaa. Usawiri huu wa wahusika kadhaa wanaotatizika kimawazo ni ithibati kuwa idadi ya watu wanaotatizika kimawazo katika jamii inaongezeka kutokana na kuongezeka kwa matatizo ya kijamii.

Mbinu hii kama uzungumzinafsi ndani ina mwelekeo mkubwa wa kisaikolojia. Kupitia kwa mjadala wa ndani kwa ndani tunaarifiwa masuala nyeti kama sehemu ya ploti ya kazi. Hali kadhalika, mbinu hii husaidia kujenga wahusika kisaikolojia kwa kuyadokeza mawazo na hisia zao.

### 2.4.2 Mkondo wa ung'amuzi

Dhana hii ilitumika mwanzo na William James (1890) katika kitabu chake ***The Principles of Psychology.*** Kulingana naye, dhana hii inarejelea fikira za binadamu ambazo zinafananishwa na mkondo wa maji ya mto ambayo huenda daima kwa kasi au pole pole. Maana hapa ni kuwa fikira za binadamu huwa kwenye mkondo fulani wa mawazo yasiokoma na mawazo haya huunganishwa na umoja fulani wenye ung'amuzi wa vitu anavyokumbana navyo mtu (uk:278). Kwa mujibu wa Frye n.w. (2001: 378-379) mbinu hii inarejelea mchakato wa fikira za mhusika zinazoonyesha umoja wa usimulizi na mkurupuko wa fikira. Anachojaribu kusema ni kuwa msanii hujaribu kudokeza ung'amuzi wa mhusika akijumulisha ufahamu wake, fikira zake, mahusiano ya ung'amuzibwete na kumbukizi zake za matukio yaliyopita. Kunao mwelekeo mkubwa wa matumizi ya mbinu rejeshi katika mbinu hii. Kama anavyotaja Mbatiah (2001: 50) mkondo wa ung'amuzi huwasilishwa kiuhalisia yaliyomo katika fikira za mhusika bila ya kuyafanyia mageuzi. Kimsingi, mbinu hii inalenga kuonyesha mawazo, hisia, fikira na mambo yote yanayompitikia mhusika akilini. Kwa sababu ya mbinu hii kuingiza sifa nyingi za kihalisia katika usawiri wa mkondo wa mawazo ya wahusika, inaweza kuangaliwa kama mbinu ya kisaikolojia. Sababu ya kuwa mbinu ya kisaikolojia ni kuwa inatusaidia kufahamu anayowaza mhusika na kwa hivyo kuweza kujua hisia zake na matamanio yake. Mfano huu unaakisi hali hii.

> Njiani Faisal alipeleleza kila kitu kimyakimya. Zile sauti za zamani zilizokuwa sasa zikimvumia masikioni mwake na kumtia homa- ya-kumbukizi na kutekenya zaidi upekuzi akilini mwake. Sauti za utoto wake na ujana wake, ...za rabsha na vijana wenzake, za...za...za...sauti za wahindi ...madukani. Sauti za wauza vitu...Mara: *Haya njugu...* Tena: *Jamani ladu, ladu, ladu hiiiizoooo ...* Kisha: *Kunywa togwa kunywa, kunywa togwa kunywa upate buruda ...* Na baadaye: *Moja shilingi moja, nyingine 'takuongeza.* Mohamed ( K.h.j. uk: 11)

Huu ni mtiririko huru wa mawazo ya mhusika Faisal ya utotoni yanayompitikia bila ya kufanyiwa mageuzi. Yanaonyesha namna mambo yaliyohodhiwa katika ung'amuzibwete yanavyojitokeza katika sehemu ya

ung'amuzi. Aidha, mbinu hii inadhihirisha dhima ya mwandishi ya upekuzi wa ndani wa fikira za wahusika na kutufichulia wanayowaza ambayo hayajitokezi kiusemi.

Kama anavyodai Frye (K.h.j.) kifungu cha mkondo wa ung'amuzi huwa na uwasilishaji usio na mpangilio wa mkwezo unaotokana na mawazo halisi ya binadamu yanayoonyesha mkurupuko wa fikira. Ni kutokana na hali hii ndipo kuna matumizi ya dondoo na mistari kama inavyoonekana katika kifungu hapo juu. Matumizi ya dondoo na mistari yanaonyesha namna kulivyo na mapengo katika mkondo wa mawazo ya binadamu. Matumizi ya vifaa hivi viwili yanaonyesha uhalisia na uchangamano wa fikira na hisia za binadamu na jinsi mambo yaliyohifadhiwa katika ung'amuzibwete yanastahili kupangwa upya ili yalete mantiki fulani. Suala hili linaweza kurejelewa kama dhana ya Freud (K.h.j.) ya masahihisho ya kiupili inayodai kuwa ndoto au mawazo katika ung'amuzibwete huwa na mapengo ambayo hujazwa ili kubuni kisa cha kimantiki.

Aidha, katika kifungu hicho hapo juu kumetumika italiki. Matumizi ya kifaa hiki ni sifa nyingine ya mkondo wa ung'amuzi kama anavyodai Frye (K.h.j.). Katika kifungu husika mwandishi ametumia italiki kuonyesha sauti alizozisikia mwenyewe. Kwa njia hii, anaonyesha umuhimu wa maneno hayo kwa namna fikira zake zilivyoweza kuyadokeza kwa usahihi ilhali ni maneno aliyoyasikia miaka mingi iliyopita. Matumizi ya italiki kama anavyodokeza Olali (K.h.j uk:86) hulenga kuupa ujumbe nguvu na uzingatifu. Kwa njia hii inamfanya msomaji auzingatie kwa mtuo na wala si kuakisi tu maneno ya lugha nyingine yaliyokopwa katika Kiswahili.

Mkondo wa ung'amuzi haurejei tu mawazo ya utotoni bali hudokeza mawazo mazito yenye athari kwa kazi nzima. Kwa mfano, kifungu kifuatacho kinaonyesha namna Nana alivyo mtambuzi wa masuala yanayoathiri jamii.

> Hapo nilimkumbuka Derrida na ubomozi wake anaouita *(de)Construction.* Kila kitu lazima kiwe *deconstructed.* ... Nilipomkumbuka tu alidhani ninamwita. ... Nilimsoma zamani ..... Nilimhusudu ndiyo, lakini siku zote hizi nimekataa kumwabudu. Falsafa ni maisha yenyewe. ... Kinyume chake, lazima maisha yetu yatawale falsafa. Sikubaliani nao wanaotilia mkazo kitovu cha duara. Nguvu tunazoambiwa zimeumbwa ili wanaoishi pembezoni lazima wavutwe ndani kusujudu kitovu. Nionavyo

> mimi lazima ukingo wa duara uvunjwe ili vilivyo ndani vimiminike nje na vya nje viweze kupenya ndani .... Bila ya hivyo walioko pembezoni mwa maisha watajikuta wako pembezoni- wamezugwa kabisa... Mohamed (K.h.j uk: 60)

Mkondo wa mawazo ya Nana unatupa mawazo ya Derrida yanayoangalia vitu kuwa vimevunjikavunjika na wala havionyeshi umoja.[4] Ingawa anamhusudu anapinga dhana ya falsafa kutawala maisha badala ya maisha kutawala falsafa. Vinginevyo, anatudokezea hali ya matajiri viongozi kila mara kuwa kitovu cha kila mfumo wa kijamii na kwa hali hiyo kuwaweka maskini pembeni pasi na pa kushikilia. Hili ndilo suala nyeti lililo sababu ya dhuluma zinazoendelezwa na jamii hii. Kwa njia hii mkondo wa ung'amuzi ni sehemu muhimu ya kuujenga msuko wa kazi ya kifasihi na maudhui ya kazi hii. Vilevile, unatuonyesha hali yao ya kihisia na kimawazo na kwa hivyo kuchangia kuwajenga wahusika kisaikolojia.

### 2.4.3 Mbinu rejeshi

Mbinu rejeshi ni mbinu ya ujenzi wa ploti ambapo matukio yaliyotokea kabla ya wakati wa usimulizi wa matini yanasimuliwa. Mbinu hii ina dhima ya kujaza mapengo katika ploti ya kazi ya kifasihi kwa kutujuza matukio ambayo yamekwisha kutendeka na kwa hivyo kutusaidia kuwa na uelewa wa kisa kizima cha kazi yenyewe. Kwa ujumla mbinu rejeshi hutusaidia kujibu maswali kama vile: kulitokea nini kabla ya tukio hili? Na, kwa nini mhusika huyu akafanya tendo hili? Wamitila (2008: 154-157) ameainisha aina kumi za mbinu rejeshi ambazo ni mbinu rejeshi ya ukamilishaji, ya nje, ya urudiaji, ya ubinafsi, ya ndani, ya mseto, ya muktadha wa karibu, ya muktadha mpana, ya ndani ya mbinu rejeshi na ya kikufu. Tumerejelea aina nne tu za aina hizo kumi ambazo tunaona zimejitokeza kwa uwazi zaidi nazo ni mbinu rejeshi ya ukamilishaji, mbinu rejeshi ya nje, mbinu rejeshi ya kibinafsi na mbinu rejeshi ya ndani.[5]

Mbinu rejeshi ya ukamilishaji kwa mujibu wa Wamitila (K.h.j) huhusu urejelezi wa matukio au maelezo kwa lengo la kukamilisha au kujaza jambo lililotokea. Katika riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke*** (uk: 250), Faisal anarejelea tukio la kukutana kighafla na Amour. Urejeshi huu unalenga kujaza jambo lililotokea na kumwondoa Nana karibu na Faisal. Mbinu hii imetumiwa kujaza pengo ili tuelewe mabadiliko ya kitabia, kimawazo na kihisia katika wahusika hawa. Vilevile, hadithi ya Bimkubwa kwa bintiye (uk:287-292) inatusaidia tuelewe maisha yake ya awali ambayo Nana hakuyashuhudia. Hii ni kama ndoto inayompitikia

katika tafakuri ya Nana iliyofanyiwa masahihisho ili iwe kiunzi kizima cha maisha ya ndoa ya Bimkubwa yalivyokuwa. Kwanza, mbinu hii imetudokezea hali ya kisaikolojia ya Nana ya kumwaza mama yake sana. Pili, sehemu hii inatujuza namna Nana alivyotaka sana kujua hali halisi ya maisha ya mama yake.

Aidha, kuna mbinu rejeshi ya nje ambayo inarejelea matukio au mawazo yanayaoanza na kumalizika kabla ya mwanzo wa hadithi husika. Kwa mujibu wa Wamitila (K.h.j) urejeshi huu uko nje ya mwanda wa wakati wa matini husika. Maana hapa ni kuwa matukio na mawazo yanayorejelewa yametengana kiwakati na matini husika kwani yalitokea kabla kisa cha ***Nyuso za Mwanamke***. Mfano mzuri wa urejelezi huu ni pale Nana anarejelea viongozi mbalimbali wa dunia ambao mawazo yao ya kimapinduzi yalichangia kuleta mabadiliko makubwa katika nchi zao na ulimwengu mzima (uk:85-86). Kumbukizi za viongozi hao ingawa Nana ametengana nazo kiwakati zinaonyesha namna ambavyo ameathirika na mawazo yao kwa kiasi cha kutokea kwao katika ndoto zake za mchana. Ni mawazo yao kuhusu amani, haki, na uhuru yaliyompa msukumo wa kupigania haki zake na kujiendeleza. Urejelezi huu una uamilifu mkubwa katika kazi hii kwa kutujuza mawazo yaliyoathiri tabia, mwenendo na ari ya Nana na wahusika wengine.

Mbali na hayo, kumetumika pia mbinu rejeshi ya kibinafsi. Hii ni mbinu rejeshi inayorejelea matukio au mawazo yanayomhusu mhusika mwenyewe. Kama anavyoeleza Wamitila (K.h.j.) mbinu hii hutumiwa pale ambapo kuna maelezo ya ndoto au kumbukumbu zinazomhusu mhusika binafsi. Uamilifu wa mbinu hii hususani hulenga kudokeza hali ya kisaikolojia ya mhusika kama inavyoonekana hapa chini.

> Sasa suala moja lilifululiza akilini mwake: 'kwa nini alimpiga vibaya namna hivyo Ngware?' Yote haya ya kudidimia ardhi ya saba yasingelitokea labda kama asingempiga Ngware, na si kumpiga tu kusema kweli, ni kumtwanga vibaya. Ngware aliona atumie nguvu kwa sababu yeye kijana shababi, kwa sababu yeye ni mwanamume, kwa sababu ana nguvu nyingi. Lakini Nana alimkabili kwa maarifa ya karate. Matokeo ni kwamba ilibidi Ngware kulazwa hospitali na mlipa gharama ni Nana. Mohamed (K.h.j uk: 274)

Nana anarejelea namna alivyomtia adhabu Ngware alipompiga Bi. Mau. Ni wazi kuwa anajutia tukio hilo na anafikiria huenda ndilo lililomfanya apigwe na kibuhuti. Katika urejelezi huu suala analorejelea Nana linamhusu yeye mwenyewe na linaelekea kumwathiri kimawazo na kihisia. Linazua hisia za huzuni, majuto na huruma. Na hii ndiyo dhima ya mbinu hii ya urejeshi.

Nayo mbinu rejeshi ya ndani hurejelea urejelezi ambao upo ndani ya wakati unaodhihirishwa na matini husika. Hii ina maana kuwa matukio au mawazo yanayorejelewa yamo katika mandhari ya kiwakati ya tukio kuu la kazi ya kifasihi. Katika *Nyuso za Mwanamke* (uk:9) Faisal anarejelea namna baba yake alivyouawa katika ghasia za kupigania madaraka. Tukio hili ndilo lililomnyima fursa ya kuwa karibu na Bimkubwa kwani baada ya tukio hili ilibidi ahamie Abudhabi. Urejelezi huu umejikita katika kisa kikuu cha kazi hii kwani tukio hili ndilo linalofuata tukio la mapenzi kati ya Faisal na Bimkubwa. Urejelezi huu unaathiri wasomaji kwa kuwahamasisha juu ya matukio ya wahusika. Ni kumbukizi ya matukio ya aina hii ndiyo inayomwondolea Faisal hamu ya maisha na kumfanya atafute hata visivyokuwepo tena.

Kwa kuhitimisha kisehemu hiki, ni muhimu kutaja kuwa mbinu rejeshi kama kijenzi cha msuko wa matini hutokea kama kumbukumbu ya matukio yaliyopita au mawazo yaliyopita. Aidha, mbinu hii imetokea kama sehemu ya mbinu nyingine kama vile uzungumzinafsi, ndoto na hata barua. Mbinu hii imetumika kwa kiasi kikubwa kurejelea matukio mengi ambayo yamechangia katika ujenzi wa ploti ambayo bila kurejelewa hadithi ya kazi hii haingekamilika.

### 2.4.4 Nyimbo

Nyimbo kwa mujibu wa Wamitila (2003b: 107) ni tungo zenye mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka. Neno mahadhi lina maana ya hali ya kupanda na kushuka kwa sauti katika wimbo. Kimsingi, nyimbo ni kipera cha utanzu wa ushairi ambacho huundwa kwa lugha ya mkato na vipengele vyake hupangwa kwa mapigo ya muziki. Kunazo nyimbo za aina nyingi kama vile mbolezi, bembezi, nyimbo za mapenzi, nyiso na wawe. Nyimbo hulenga, kama anavyoongeza Wamitila (K.h.j), kukejeli, kuliwaza, kusifu, kutumbuiza, kubembeleza na kufunza.

Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* kuna nyimbo nyingi zilizotumiwa na mwandishi kama vijenzi vya msuko wa kazi. Hii ni kwa sababu nyimbo hizi zimedokeza matukio na mawazo yenye lengo la kupeleka mbele kisa na maudhui ya kazi hii. Nyingi ya nyimbo hizi ni za mapenzi. Kuonyesha umuhimu wa nyimbo katika ujenzi wa ploti, nyimbo zimetumika karibu katika kila sura ya kazi hii. Mfano ufuatao unaonyesha dhima yake.

Njia ni'pitayo

| | |
|---|---|
| Njia ni'pitayo | imejaza zogo |
| Kani na kamiyo | nazipa kisogo |
| Na vingi viliyo | kamwe si vidogo |
| Hisi zi'ngiayo | mwingi mkorogo |
| Huu moyo wangu | umeshikwa tego |
| Naumwa umiyo | kubwa hili pigo |
| Njia nifwatayo | imezingwa ugo |

Njia ni'pitayo! Mohamed (K.h.j. uk: 40)

Huu ni wimbo aliouimba Faisal, Nana alipomwona mara ya kwanza barabarani. Ni wimbo unaodokeza taabu za Faisal za kumsaka Bimkubwa na vikwazo dhidi ya juhudi zake za kusaka penzi lake. Unatufichulia anayowaza na anavyohisi. Kwa njia hii unatudokezea hali yake ya ndani kwa sababu kama anavyodai Wamitila (2008: 309) lugha ya kishairi huwa msingi muhimu wa kutoa mawazo yenye uhisivu fulani na huhusishwa zaidi na mambo au hali zenye mhemko au hisia nzito. Kwa njia hii Faisal ameweza kuyatoa mawazo yake na hisia zake bila kukiuka kaida za jamii kwa sababu kama angewaambia wanajamii kuwa ameacha aila yake kuja kutafuta mapenzi ya Bimkubwa angeonekana kama mwenye kichaa.

Baadhi ya nyimbo katika kazi hii zinaibua mawazo mazito yenye hisia za huzuni, huruma na hofu katika hadhira. Uibuaji huu wa hisia hutegemea maudhui yanayoendelezwa. Wimbo ufuatao unaonyesha hali hii;

Baba na mama watende
Kunioza dume kongwe
Halisafiri halende
Kazi kupiga matonge
Likingia mvunguni
Kazi kuvunja vikombe
Likilala kitandani
Languruma kama gombe
Mmm mtoto,mmm-un-
Mmm mtoto, mmm-un Mohamed (K.h.j. uk:175)

Bi. Mau aliusikia wimbo huu ukiimbwa na mzuka wa Bimkubwa ili kumbembeleza Nana. Ingawa ulikusudiwa kuwa bembezi maneno yake si ya kumwongoa mtoto alale bali unarejelea maisha ya ndoa kati ya Bimkubwa na Bwana Hila. Badala ya kumliwaza Nana unamtahadharisha dhidi ya maisha ya ndoa. Hiki ni kinaya cha hali dhidi ya ndoa katika jamii na wazazi wanaowaoza binti zao bila ya kufikiria hatima ya ndoa hizo. Ni wimbo unaoibua hisia za huzuni, huruma na hofu kwa vijana kama Nana ambao watataka kuolewa. Vilevile, unafichua namna ndoa ni taasisi yenye dhuluma dhidi ya wanawake kwa kuwanyima haki zao.

Mbali na hayo, nyimbo zimetumiwa katika kazi hii kuibua hisia za furaha na mapenzi. Nyimbo za aina hii zinaonyesha namna mhusika alivyohamanikia kitu fulani kama inavyodhihirika katika wimbo ufuatao;

Ewe Mwezi

Unapochomoza Na uzuri wako
Unanipumbaza Kwa kicheko chako
Kuwa n'naweza N'ngekuja kwako

Kiitikio:-

Ewe mwezi ewe azizi Nipe mbawa nirukiye
Ewe mwezi ewe mpenzi Nipe ngazi nipandiye

Nikiona sura yako Akili zinaniruka
Lakini umbali uliko Vipi huko nitafika?
Nataka shauri lako Kama nawe wanitaka

Kiitikio:-

Ewe mwezi ewe azizi Nipe mbawa nirukiye
Ewe mwezi ewe mpenzi Nipe ngazi nipandiye Mohamed (K.h.j uk:228)

Huu ni wimbo ulioimbwa na Nana kumhusu Amour. Ni wimbo wa mapenzi unaonyesha jinsi Nana amesalitika na mahaba ingawa alikuwa amejiasa kutojihusisha na wanaume kutokana na mateso aliyoyapata mama yake. Anaeleza namna anavyotaka amfikie Amour bila mafanikio. Tabia hii ya Nana ndiyo aliyodhihirisha mama yake kuwa hata baada ya kudhulumiwa na Bwana Hila bado alisalitika na mapenzi na kuolewa na wanaume wengine wawili. Kama anavyodai Holland (K.h.j.) kile anachofanya

mtoto ni utambulisho wa kile alichofanya mzazi. Hali hii ya Nana kushabikia wanaume na ndoa ilhali alikuwa amewaogopa inafanana na ya Leonardo da Vinci aliyekubali kuunda silaha hatari za maangamizi ingawa alikuwa mpole na hakutaka kuwauwa wanyama.[6] Hali hii ya kuyarejelea mambo anayopinga ni ushahidi tu wa kubanwa kwa matamanio ambayo badala ya kuyaenzi anayapinga. Vilevile wimbo wa Nana katika arusi yake unathibitisha namna alivyomfurahia mume wake na taasisi ya ndoa kwa ujumla (uk: 299-300).

Katika wimbo huu mwezi ni sitiari ya kurejelea Amour. Matumizi ya mwezi kurejelea Amour, ambaye ni mwanamume, yanakiuka mpangilio wa tamathali za kike na za kiume ambapo vitu vya mviringo na uwazi huwa tamathali za kike huku vitu vilivyochongoka na vikali huwa tamathali za kiume. Hizi ni tamathali au ishara zilizobuniwa na Freud na zinapatikana katika jamii nyingi ulimwenguni. Urejelezi huu unaokiuka mpangilio huu ni mfano mzuri wa mawazo ya kiuana yaliyobanwa Nana alipokuwa mdogo na kwa hivyo hakuweza kujifunza jinsi tamathali hizi zinaweza kurejelewa kwa kukosa utangamano ufaao. Hali hii pia ilijitokeza katika michoro ya mchoraji maarufu wa Kitaliano Leonardo da Vinci aliyeishi katika karne ya 15. Katika mmoja wa michoro yake, alichora mwanamke mjamzito ambapo alionyesha titi moja likiwa bapa badala ya kuonyesha limesimama tisti kifuani. Kwa mujibu wa maelezo ya Freud mchoro huo unadhihirisha kuwa hakuwa na haja ya kumwangalia mwanamke ili aelewe namna mwanamke mjamzito anavyoonekana. Hali hii inatokana na dhana hiyo hiyo ya ubanaji wa mawazo ya kingono.

Faisal naye anaonyesha mawazo ya uana yaliyokomaa katika wimbo wake alioutunga kuomboleza kunyimwa Bimkubwa.

Kipepeo

| | |
|---|---|
| Huruka na kunijia | Na kutua mikononi |
| Vyema anavyonukia | Na pambo linalo shani |
| Huja kunitembelea | Kipepeo wa moyoni |
| Kiitikio:- | |
| Kipepeo wende na kurudi | Mpaka tupojaliwa |
| Itapotimu miadi | Roho zetu zitapowa Mohamed (K.h.j uk:252) |

Katika wimbo huu Faisal anamrejelea Bimkubwa kama kipepeo. Kipepeo ni mdudu mrembo na mtulivu kama alivyo mwanamke. Ukomavu wa mawazo ya Faisal unatokana na kaida za jamii hii zinazowapa wavulana uhuru wa kujitawala tofauti na wanavyowadhibiti wasichana. Hali hii ndiyo inayompa uhuru wa kupekua mambo mengi zikiwemo tamathali za uana ipasavyo.

Kwa maoni yetu, nyimbo zimetumiwa katika kazi hii kusawiri hali za kisaikolojia za wahusika kwa kuibua mawazo na hisia zao za ndani zinazowakumba. Aidha, kutokana na nyimbo hizi tunapata mawazo na visa vingi walivyovishiriki wahusika ambavyo vinasaidia kukuza ploti na maudhui.

### 2.4.5 Barua

Kwa mujibu wa kamusi ya TUKI (2004: 23) barua ni maandishi yenye ujumbe yanayopelekwa kwa mtu mwingine kwa njia ya mkono au kupitia posta. Aghalabu, barua huwa na ujumbe ambao mwandishi hulenga kumpasha mpokezi wake. Katika enzi hii ya utandawazi kuna barua pepe inayotumwa kwa njia ya tovuti. Kimuundo kuna aina mbili muhimu za barua ambazo ni barua rasmi na huria. Barua rasmi huwa na muundo funge ambapo hamna utokaji nje mwingi. Kwa upande wake, barua huria au ya kirafiki hurejelea aina ya barua ambayo ina muundo huru wa kutamba kwingi katika uandishi wake. Kunayo pia barua ndefu ambazo ni riwaya.[7]

Barua ni kijenzi muhimu cha msuko wa kazi ya kifasihi kwa sababu hudokeza mawazo ya wahusika na matukio muhimu yaliyotokea au yanayotarajiwa kutokea katika kazi ya kifasihi. Kwa sababu ya uamilifu huu, barua zinaweza kutumiwa kuyadokeza masuala mazito yanayowakumba wahusika kama inavyodhihirika katika barua ambayo Bimkubwa alimwandikia Nana (uk:172). Katika barua hii anamwarifu Nana kuwa amemwachia urithi wa shilingi milioni tisini. Aidha, anamfahamisha juu ya maisha yake ya kubaguliwa, kunyimwa uhuru wa kujiamulia na umaskini. Kwa maelezo haya tunapata kuelewa maisha ya awali ya Bimkubwa, vita dhidi ya ubabedume wa wanaume na mapenzi ya dhati aliyoyaona kwa Faisal. Katika barua hii tunapata matukio muhimu yaliyo sehemu ya ploti ya kazi hii kama wanawake kupigania haki zao, kupendana kwa Bimkubwa na Faisal na kuzuiwa kwao kuoana.

Baadhi ya barua katika kazi hii zinazua hisia kali kwa wasomaji kwa sababu ya masuala nyeti na tata ambayo zinadhihirisha. Mfano wa aina hii ya barua ni barua ambayo Bimkubwa alimwandikia Nana kumwomba msamaha kwa kukosa fursa ya kumlea (uk: 231). Katika barua hii anasikitika kwa kutomlea na anamwarifu kuwa halikuwa kosa lake bali la baba yake. Mbali na hayo, inamwarifu juu ya ndoa tasa kati yake na baba yake. Kwa maelezo haya Nana alichukuliwa akawa kama anayemwona na kumsikia mama yake ana kwa ana. Ufasiri wa hali hii ni kuwa Nana anamwaza sana mama yake kiasi cha kugeuka ruiya kiasi cha mawazo haya kujijenga na kuwa sehemu ya ung'amuzi na ung'amuzibwete wake. Ni barua hizi alizokuwa anasoma zilichochea hali ya kumwona mwanamke wa kindoto akishiriki katika kipindi cha *Dukuduku* ambaye ni yeye tu alimwona. Aliamini kuwa huyo alikuwa mama yake. Kwa maoni yetu barua hii na nyingine ziliibua hisia kali kwa Nana kiasi cha kumwondoa katika uhalisi.

Barua ya mwisho katika riwaya hii iliandikwa na Faisal kumwarifu Nana kuwa amehamia Morishas (uk:308). Katika barua hii anamfahamisha kuwa amekutana na nduguye, Suria. Hapa tunaona namna Faisal alivyodididimizwa na mawazo ya mapenzi kwa Bimkubwa kiasi kwamba anahusisha na kukienzi chochote kinachohusishwa na Bimkubwa kwa kumkosa yeye.

Ni muhimu kusisitiza kuwa barua zina uamilifu mkubwa katika mchakato wa ujenzi wa ploti ya kazi ya kifasihi. Uamilifu huu unatokana na barua kuchangia matukio na mawazo muhimu katika mpangilio wa visa katika ploti. Aidha, barua zinachangia kujenga ploti kisaikolojia kwa kusawiri mawazo ya ndani ya wahusika kuwahusu wahusika wengine na athari ya matukio wanamoshiriki. Barua zimetumika katika kazi hii kwa njia ya kipekee ya kuzua hisia kali kwa wasomaji pamoja na kuyadokeza mawazo na tabia za wahusika. Pia, zina mchango mkubwa kuonyesha mahusiano yaliyokuwepo kati ya wahusika mbalimbali katika kazi hii na kudokeza maudhui kama ukombozi wa mwanamke.

### 2.4.6 Ndoto

Kwa mujibu wa Malcom (1959: 94) ndoto ni mtiririko wa mawazo ya ndani ya mtu aliye macho au anayelala yanayoambatana na maono, taswira za matukio, mazingaombwe, fikira za uwongo, udhanifu, ndoto za mchana, ukisiaji, uwepo na malengo, matarajio na matamanio. Kutokana na maelezo yake ni wazi

kuwa ndoto huambatana na picha na mawazo na matukio kana kwamba ni matukio na mawazo yanayotokea katika hali halisi. Kulingana na Hall (1966: 2-3) ithibati ya kuonyesha mtu anaota ni kule moyo kupiga sana au kupiga nduru, kutembea na kuongea anapolala. Si kwamba dalili hizi zote huonekana mtu anapoota lakini baadhi yazo huonekana mtu anapokuwa na jinamizi. Hall anaongeza kuwa mwotaji wa ndoto ni mtu ambaye hana uwezo juu ya yaliyomo katika ndoto hata akiwa macho wakati wa kuota. Maana inayojitokeza ni kuwa mtu yeyote anayekosa umakini wa kufikiria na anazungumza mambo yasioeleweka au anatoa majibu yasiolingana na aliyoulizwa anaweza kusemwa anaota. Kwa hivyo, ni wazi kuwa mtu anayeota huwa katika hali ya ung'amuzibwete wa aina fulani iwe ni katika ndoto ya mchana au ya usiku.

Kama anavyodai Malcom (K.h.j.) ndoto ni kifaa cha kufasiri sifa na tabia za mtu. Anachosema ni kuwa ndoto huhusiana na maisha ya kawaida ya mwotaji kwa sababu mambo yanayojitokeza katika ndoto ni yale yaliyotendeka au yanayotarajiwa kutokea katika maisha ya mhusika. Aidha, ndoto huakisi matarajio yetu hasa ya utotoni na hudokeza mambo ambayo kwa kawaida hatungetamka au hatungetenda katika maisha halisi kwa kuhofia kaida za kijamii. Kwa maana hii basi, ndipo kazi ya kifasihi inaangaliwa kama ndoto ya mwandishi ambayo imeundwa kisanii na msanii huweza kudokeza mambo ambayo katika hali ya kawaida yangekuwa marufuku kwake kuyadokeza.

Katika data yetu ndoto nyingi zinazojitokeza ni za mchana. Ndoto hizi zinatokea wakati wahusika wanazama katika mawazo mazito. Katika hali hii, wanaelekea kupoteza uhalisi wa mambo yanayowazunguka. Mfano mojawapo wa ndoto ya aina hii ni wakati Nana na Faisal wanasafiri wakielekea mjini (uk:122-125). Nana anawaona watu wanaotembea pembezoni mwa barabara wakiwa mifupa na ngozi na wenye vichwa vikubwa kama sangara. Baadaye anawaona watu hao wakiwa na manna na selwa vikiwa vimening'inia usoni pao na wanarukaruka kuvikamata. Mwisho, aliona kijana katika gari la *Rolls Royce* asiye na shingo wala kichwa. Kwa mujibu wa Freud (1953: 14) ndoto ni ushahidi wa kumbukumbu za matukio na mawazo ya mwotaji. Katika ndoto hii tayari Nana alikuwa amewaona watu wa Sambejambe namna walivyogubikwa na hali ngumu ya maisha. Mawazo ya hali ya watu hawa ilikuja kutawala mawazo yake na lazima angewaona kama wanavyojitokeza katika ung'amuzi wake. Kwa mujibu wa ufasiri wa

ndoto ishara huchukua sehemu kubwa katika ufasiri wake. Katika ndoto hii kuna ishara karibu nne; watu ambao ni mifupa na ngozi, watu wenye vichwa vikubwa, manna na selwa iliyoning'inia usoni pao na kijana asiye na shingo wala kichwa. Katika ndoto ya mtumishi wa Farao katika Biblia Takatifu kitabu cha Mwanzo (Sura ya 41:25-36), ng'ombe saba waliokonda waliowala wale saba wanono walikuwa ishara ya njaa ya miaka saba. Kutokana na ufasiri huo hivyo basi, watu ambao ni mifupa na ngozi ni ishara ya umaskini na uhitaji wa watu wa Sambejambe navyo vichwa vikubwa kama sangara vinaweza kuchukuliwa kurejelea shida nyingi zinazowakumba watu hawa. Sangara ni samaki mkubwa wa maji baridi mwenye magamba na mdomo mpana ambaye asili yake ni Mto Nile. Kwa upande wake, manna na selwa ambavyo vyote ni vyakula vitakatifu vinaweza kurejelea riziki ambayo iliwapiga chenga bila wao kuipata kama ilivyoonekana na tendo lao la kurukaruka. Naye kijana asiye na shingo au kichwa ni ishara ya mabadiliko yaliyotarajiwa kutokea katika maisha ya Nana. Hii ni kwa sababu ilionekana aliwafuata na kuwapita kila mara kama mwenye lengo fulani.

Kutokana na ufasiri wa ishara za ndoto hiyo, tunaweza kukisia kuwa Nana anawahurumia watu wa Sambejambe kutokana na hali ya umaskini uliowakumba na alitaka sana hali hii iboreke. Sababu hii ndiyo inayompelekea Nana kuanzisha biashara ambayo ilikuja kuwaauni watu wanyonge hasa wanawake kwani hiyo ndiyo iliyokuwa ndoto yake. Vilevile, kuna uwezekano wa kutokea mabadiliko katika maisha ya Nana kutokana na hamaniko lililompata alipomwona huyo kijana aso na shingo wala kichwa kwa maana kwamba unayoyaona kuwa siyo huja kuwa. Hii ndio maana tunamwona Nana akisalitika kuolewa na Amour ingawa hakutaka kudhibitiwa na wanaume mbali na mzuka wa mama yake kumwasa kutoolewa.

Hali kadhalika, kuna ndoto ya Faisal inayotokea wakati ameketi msituni (uk:251-252). Katika ndoto hii Faisal anawaona vipepeo wengi wenye rangi za kupendeza na baadaye akatokewa na kivuli cha Bimkubwa. Baada ya hapo mazingira yalibadilika na kukatokea kipepeo anayefukuzana na mabonge ya mawingu kisha miti ya maua yanayonukia inatokea na kuwalika ndege na vipepeo kufyonza viriba vyao vya asali. Ni wakati huu anakumbushwa wimbo wa kipepeo na akiwa katika kumbukizi hiyo anaona kivuli cha Bimkubwa kikimjongelea hatua kwa hatua. Alizindukana alipoisikia sauti ya Nana na akatambua

kumbe hakuwa Bimkubwa bali alikuwa Nana. Kabla ya ndoto hii Nana alikuwa amemwambaa Faisal. Jambo hili lilimwondolea Faisal furaha na kumletea mawazo chungu nzima hasa kuhusu mahaba yake na Bimkubwa. Huu ulikuwa msingi wa ndoto hii. Kuna ishara zinazojitokeza ambazo ni vipepeo, kipepeo na mabonge ya mawingu na vipepeo na ndege kufyonza viriba vya maua. Vipepeo katika jamii nyingi ni ishara ya mapenzi na kwa hivyo vinaashiria mapenzi kati ya Bimkubwa na Faisal. Naye kipepeo anayefukuzana na mabonge ya mawingu ni ishara za juhudi za Faisal zisizozaa matunda za kutafuta mapenzi ya Bimkubwa kwani mawingu ni mvuke tu usioweza kukamatika kama yalivyo mapenzi. Navyo viriba vya maua ni ishara ya wanawake ambao huwavutia na kuwafurahisha wanaume na vipepeo na ndege wenye vidona wanarejelea wanaume wenye kufaidi uzuri wa wanawake. Ufasiri huu unatokana na dhana ya tamathali za kike na za kiume ya Freud (K.h.j) kuwa vitu vyenye uwazi ni ishara ya mwanamke na vitu vyenye ncha au vilivyochongoka ni ishara ya wanaume. Kutokana na ufasiri huu hivyo basi, ni wazi kuwa Faisal amegubikwa na mawazo ya mapenzi juu ya Bimkubwa na ingawa amekwisha kufariki haamini kwamba amekufa bali anaona kuwa anaweza kutokea siku moja. Ukweli huu ulidhihirika wakati Nana alipokuwa anakuja alimwona kama Bimkubwa, hivyo akaingiwa na hamu ya kukutana naye. Hali hii inaonyesha athari ya dhana ya udidimifu inayodai kuwa mtu anayetatizika kisaikolojia hurejelea hali zake za awali hasa za ujana au utotoni.

## 2.5 Mbinu za usimulizi

Usimulizi unaweza kuangaliwa kama mchakato mzima wa mawasiliano kati ya msanii na msomaji au msikilizaji. Usimulizi kama mchakato wa mawasiliano unarejelea uelezaji kwa njia ya mtiririko wa matukio katika kazi ya kifasihi. Kwa mujibu wa Wamitila (2003a: 325) uelezaji huwa na mtiririko wa kimwendelezo unaoonyesha mshikamano wa mawazo. Analodokeza ni kuwa usimulizi hubainishwa kwa mtindo wa kinathari ambapo kuna mfuatano wa matukio yanayosimuliwa. Kama anavyodai Rimmon-Kenan (2002:2) mfuatano wa matukio kimtiririko ndio unaozitofautisha kazi za kinathari kama vile riwaya, novela, hadithi fupi na tarihi na kazi zisizo za kinathari kama vile ushairi. Kunazo mbinu mbalimbali za usimulizi ambazo ni usimulizi anuwai, usimulizi ngazi, usimulizi maizi, usimulizi dukizi, usimulizi sawia, usimulizi tangulizi na usimulizi nafsia.[8] Kwa mujibu wa utafiti wetu tumezijadili mbinu za usimulizi

ambazo zina mwelekeo mkubwa wa kisaikolojia. Mbinu za aina hii zinaweza kurejelewa kama usimulizi-saikolojia. Hii ni dhana iliyotumiwa mwanzo na Cohn (1978: 11) kama inayodhihirisha ung'amuzi wa hisia na mawazo ya mhusika. Mbinu hii hutumia mbinu kama vile usimulizi wa nafsi ya kwanza, usimulizi wa nafsi ya tatu na usimulizi mwakote. Mtindo unaonekana kuwa maarufu katika kazi nyingi za kinathari ni kutumia mchanganyiko wa mbinu za usimulizi. Hii ndiyo hali inayojitokeza katika riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke, Dunia Yao*** na ***Tata za Asumini.*** Tofauti inatokea katika ***Bina-Adamu!*** ambako usimulizi wa nafsi ya kwanza unatawala na katika ***Babu Alipofufuka*** ambako mwandishi ametumia usimulizi wa nafsi ya tatu. Mwandishi katika riwaya hii ametumia aina zote za usimulizi nafsia na usimulizi mwakote.

Usimulizi kama mbinu ya kimtindo una dhima kubwa katika kazi ya kifasihi. Kwa mujibu wa Rimmon-Kenan (2002) usimulizi ni nyenzo kuu ya kuipa matini sura kwa kubainisha matukio muhimu na wahusika wake katika matini. Aidha, una dhima ya kutujuza mandhari ya kiwakati pamoja na kuweka wahusika katika visa na matukio wanamoshiriki. Kwa njia hii usimulizi huwa nyenzo ya kukuza uhusika na maudhui katika kazi ya kifasihi. Mbali na hayo, usimulizi husaidia kukita uzungumzi na uwasilishaji wa mazungumzo na mawazo katika matini. Kutokana na maelezo haya ni wazi kuwa usimulizi una umuhimu mkubwa katika ujenzi wa kazi ya kifasihi.

### 2.5.1 Usimulizi wa nafsi ya kwanza

Kwa mujibu wa Mohamed (1995: 84) usimulizi huu hutumia kiwakilishi *mimi* au kiambishi kiwakilishi cha nafsi ya kwanza -ni- cha umoja au -tu- cha wingi. Kimsingi katika aina hii ya usimulizi msimulizi huwa mshirika au mhusika wa matukio yanayosimuliwa. Ingawa usimulizi huu si maarufu sana katika riwaya nyingi kama usimulizi unaotawala kazi nzima unajitokeza katika riwaya kadhaa za fasihi ya Kiswahili. Hizi ni riwaya kama vile ***Ukiwa*** (Katama Mkangi), ***Bina-Adamu!, Musaleo!*** (Wamitila) na ***Dunia Yao*** (Said A.Mohamed). Mfano mzuri ni huu ufuataao kutoka katika ***Bina-Adamu!***

> Nilikuwa na bahati ya kumkuta amekaa juu ya gogo kubwa lililochomwa nusu na aliponiona tu alibwata kwa sauti, "Yule kichaa alisema kweli kumbe, *atakuja siku moja kutaka kukusaidia,* kumbe hana kichaa kabisa!" Mwanzo sikujua kama alinikusudia mimi. Niligeuka na kuangalia kama kulikuwa na mtu (kwa siku

chache zilizopita nilikuwa na hisia za kufuatwa na mtu; kila nikitembea huhisi kuna mtu lakini nigeukapo simwoni). K.h.j. (uk. 8)

Usimulizi huu unabainika kuwa wa nafsi ya kwanza kwa kiambishi -ni- na kiwakilishi *mimi*. Msimulizi katika kifungu hiki ni mshirika wa tukio husika.

Katika riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke*** mwandishi amewapa wahusika hadhi ya kusimulia visa vyao ambapo wao ni washirika wa matukio hayo pia. Wahusika hawa ni kama vile Nana, Bimkubwa, Faisal, Bi. Mau, Hawa na Shemsa. Kwa kumtumia mhusika mwenyewe asimulie kisa chake, tunaweza kubaini mawazo yake asilia yasioingiliwa na mawazo ya mwandishi au mhusika mwingine. Aidha, matukio anamoshiriki yanachukuliwa kama yanayotokana na mawazo yaliyo katika uang'amuzi wake na hisia zake. Mwandishi amefaulu kufanya hivi kwa kutumia usimulizi huu katika uzungumzinafsi ndani, dayolojia ya ndani na mkondo wa ung'amuzi kama inavyoonekana katika kifungu hiki.

> Bado zamu yangu. Zamu gani? Zamu ya nini? Ningojee mpaka lini? Hapa wapi? Kwa nini niko hapa? Je, hapa ndipo mwisho wa safari yangu? Ndipo nilipotaka kufika baada ya yote yale niliyoyatazamia? Aaa, kwani nilitazamia nini? Kitu gani? Kwani nilitazamia kitu nilipoondoka? Si niliondoka tu na hiyo ilitosha kwangu? K.h.j. (uk:76)

Katika kifungu hiki kibainishi cha usimulizi huu ni kiambishi -ni-. Ametumia maswali ya balagha kujisaili mahali alipo. Balagha ni mbinu ya kitamathali ambapo mhusika huuliza maswali ambayo hayana haja ya kujibiwa kwani majibu yake huenda yako dhahiri. Kujisaili huku ndiko kunakoendeleza usimulizi huu katika uzungumzinafsi ndani. Kwa njia hii tunaona namna ambavyo mhusika huyu anatatizika kimawazo na hali ngeni aliyojikuta ndani. Huu ni usawiri wa hali ya kisaikolojia ya mhusika Nana.

Hali kadhalika, mwandishi ametumia wasimulizi wengi wa nafsi ya kwanza. Wahusika hawa ni kama vileNana, Bimkubwa na Faisal. Mwandishi amefanya hivi ili kuondoa ukinaifu unaohusishwa na matumizi ya usimulizi huu kama anavyodai Mohamed (K.h.j.). Kwa kutumia wasimulizi wengi katika usimulizi huu amepanua upeo wake kuhusu kazi hiyo kwa sababu mara nyingi msimulizi mmoja anapotumika upeo wake wa kupanua mawazo huwa finyu. Kifungu kifuatacho kinaonyesha mfano mmojwapo;

> Mara nyingine wewe huja ghafla kunigutua kwa jambo la hatari linalonikabili – nami hukushukuru. Mara ngapi umenivuta bega kwa haraka ninapopigwa na bumbuwazi huku gari liko mbele yangu tayari kunimaliza? Au pale mpanda baiskeli alipokosea kunizoa na kunitupa chini kunionya mauti na baadaye kunikaripia: "Wewe kipusa! Unataka kufa mapema enh? K.h.j. (uk:18)

Usimulizi wa nafsi ya kwanza umetumika katika uzungumzinafsi ndani. Kwa njia hii mtiririko wa mawazo ya Nana unatudokezea namna anavyohamanika kumhusu mama yake. Hapa mwandishi anadokeza mawazo yasiosemwa ya mhusika huyu na kwa njia hiyo kuweza kudhihirisha hali zake za kisaikolojia. Matumizi ya usimulizi huu kwa njia hii husaidia tubaini mhusika anavyohisi na anavyowaza na athari inayotokana na mawazo hayo kama inavyojitokeza katika mfano huu.

> Baada ya kitambo kizuri cha wakati, ghafla ilinijia tu kuhisi ule ulikuwa wakati wa vita vya 'zima taa', ...Jana vita hivyo viliitwa *First World War*. Baadaye vikageuka kuwa *Second World War*. ... Na sasa vita hivyo vinaitwa utandawazi. ... Lakini nilijua yafuatayo: Hivi ni vita vinavyojificha katika giza kubwa zaidi kuliko giza la zima taa. Ni giza linalomzunguka kila mtu.... K.h.j. (Uk.81)

Msimulizi wa nafsi ya kwanza, Nana, anazungumzia vita vinavyowakabili watu hasa katika Bara la Afrika ambavyo vinawadidimiza kiuchumi, kisiasa na kijamii. Mawazo haya ni mapevu kwa msichana kama Nana ambaye ana umri wa miaka isiyozidi miaka thelathini. Hata ingawa alimaliza masomo ya shule ya upili, hangekuwa na ukomavu wa kujadili masuala kama haya kwa undani huo. Mfano mwingine wa Nana kama msimulizi wa nafsi ya kwanza kupewa mawazo mapevu kushinda tajriba yake ni wakati anatusimulia kumhusu Derrida na suala la udenguzi (uk:60). Mwandishi amemwinua hivi ili tajriba yake ya kimawazo iende sambamba na ushiriki wake katika matukio ya kazi hii kama vile kuanzisha taarab maarufu sana na idhaa ya redio na runinga. Aidha, ameruhusu Faisal kuwa karibu naye ili kumsaidia kimawazo. Hali hii pia inaonyesha kwa nini Nana anafaulu kumudu hali ya kutatizika kisaikolojia kuliko Bimkubwa na hata Faisal ambao wote wanadidimia chini sana.

Kinachofanya usimulizi wa nafsi ya kwanza kuwa mbinu ya usimulizi-saikolojia ni kule wasimulizi wake kuweza kutoa mawazo yao, hisia zao na hali zao za ndani. Aidha, kuweza kubaini athari ya mitagusano yao na wahusika wengine kwa tabia zao na hisia zao inaibainisha mbinu hii kuwa ya usimulizi-saikolojia.

### 2.5.2 Usimulizi wa nafsi ya tatu

Kulingana na Mohamed (1995:86) hii ni aina ya usimulizi ambapo msimulizi hukaa nje ya matukio yanayosimuliwa wala si mshirika wa matukio na mawazo anayosimulia. Msimulizi katika usimulizi huu mara nyingi huwa hana uhusiano wa moja kwa moja na hadithi bali anaijua na pengine amehusika kuiunda. Huu ndio usimulizi uliozoeleka katika kazi nyingi za kinathari na hasa ngano na visasili.

Kama anavyoeleza Frye na wenzake (K.h.j) wakati mwingine msimulizi wa nafsi ya tatu anaweza kuchukua hadhi ya kujua kila kitu kwa kuwa kila mahali akiingia na kutoka katika mawazo, fikira, hisia na makusudi ya wahusika. Msimulizi wa aina hii anaweza kuwa mwandishi mwenyewe au mhusika mwingine aliyepewa jukumu la kupenya ndani ya wahusika wengine. Ikiwa usimulizi huu umehusishwa na mwandishi unaweza kuitwa usimulizi mwakote. Usimulizi mwakote, kama aina hii ya usimulizi wa nafsi ya tatu huwa ni sauti ya mwandishi inayomwingia, kumpekua na kujua kila mhusika na kila kitu katika kazi ya kifasihi, hasa riwaya.[9] Kwa njia hii sauti hiyo huangaza matukio, mawazo, hisia, matamanio na tabia za wahusika kama inavyojitokeza katika kifungu hiki.

> Tokea alipotua kwa *Gulf Air* hajatulizana kabisa. Miezi mitatu sasa hana hamu ya mtu wala kitu, … amekuwa akitafuta kito cha thamani. Alitafuta kama ule mchezo wa kitoto: *saka mke wangu, saka mke wangu …Hapa hayupo, hapa hayupo!* Hamu na matarajio yamemfanya amwulize kila mtu. …Vipi mtu anaweza kusahaulika namna hii? … Kwa ufupi hakuchoka. K.h.j. (uk: 7)

Katika sehemu hii msimulizi anatuelezea jinsi Faisal ametaabika kumtafuta Bimkubwa pasi na mafanikio. Kifungu hiki kinazua hisia za huruma na huzuni. Kwa njia hii inaelekea msimulizi anamwona, anamhisi na anaona mwendo wa mawazo ya mhusika huyu. Kwa hali hii msanii ndiye kiini cha ung'amuzi na mawazo, hisia na malengo yanayojitokeza ambayo yanakaribiana na yake.

Aidha, kunajitokeza katika kazi hii msimulizi wa nafsi ya tatu ambaye ni msimulizi-andishi. Huyu ni msimulizi ambaye ni mwandishi na anaonyesha dhima ya upenyezi na upekuzi wa ndani wa fikira na hisia za wahusika ili kubaini hali zao za kisaikolojia.

> Wakati huu ndipo Faisal alipozindukana kutokana na ile ndoto ya maisha yake ya wakati uliopita. Mbele yake aliona mvua ya vipepeo ikinyesha. Vipepeo vya kila aina, vya kila sanaa ya mpangilio wa rangi na

> kila vimo na wasifu. ... Hapo ...alikumbushika wakati ule wa Bimkubwa na yeye. ...Ili kubabaisha mawazo hayo yanayochinja ndani ya moyo wake, alikitafuta kivuli cha Bimkubwa. ... akakivuta machoni mwake. ... Hapohapo ... akawaza wakati kama huu alipokuwa akimsubiri Bimkubwa afike hapo. ...akakawia...alikata tamaa ya kumwona siku hiyo. Mohamed (K.h.j uk: 251)

Hapa msimulizi amepenya ndani ya mhusika, Faisal, kiasi cha kuyafichua yaliyo katika ung'amuzibwete mambo yanayojitokeza katika ndoto; kama vile Faisal kumwona hayati Bimkubwa kama alivyokuwa hai. Kuyatoa mawazo na hisia za wahusika kwa mbinu hii ni mwelekeo mkubwa wa kuwasawiri wahusika kisaikolojia. Mbali na hayo, Faisal kuyarejelea mawazo na matukio ya ujana wake ni dhahiri kuwa anaota mchana jambo ambalo ni dhihirisho kuwa anadidimia kimawazo kutokana na kuemewa na mawazo kumhusu Bimkubwa.

Katika kazi hii msimulizi wa nafsi ya tatu anaonekana kufuatilia kisa cha mhusika fulani ndipo ageukie kisa kingine. Kwa njia hiyo anavidokeza visa vinavyofungamana na kisa hicho hadi ukamilifu wake. Kwa mfano, kisa cha Faisal (uk:3-17), kisa cha Nana na Faisal (uk:147-153) na kisa cha Bimkubwa (uk:283-292). Kusimulia kisa cha mhusika mmoja bila urejelezi mwingi wa visa vya wahusika wengine kama inavyojitokeza katika mifano hii hujenga mantiki na umoja wa visa hivyo. Kwa maoni yetu msimuliaji huu hukusudia kujenga uelewa wa matukio na mawazo yanayojitokeza kutokana na mhusika fulani. Kwa mfano, kutokana na hadithi ya kurasa chache tumeweza kuyaelewa maisha ya ndoa za Bimkubwa yalivyokuwa. Usimulizi wa nafsi ya tatu unaweza kujitokeza kama usimulizi-saikolojia ikiwa msimulizi ametumia upenyezi au upekuzi wa mawazo na hisia za wahusika. Msimulizi atafaulu kufanya hivyo ikiwa anakuwa kila mahali na anatoka na kuingia katika mawazo, hisia na makusudio ya wahusika. Ikiwa hakuna upenyezi na upekuzi wa aina hii basi hakutakuwa na usimulizi-saikolojia.

## 2.6 Hitimisho

Katika riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke*** matukio yamesukwa kwa njia ya kutokeza nyuso mbalimbali za mwanamke katika jamii husika. Wanawake katika jamii hii wanaonyesha nyuso za huzuni, wasiwasi, hofu, unyonge na maumivu kutokana na kudhulumiwa na wanaume kwa kunyimwa uhuru na haki zao. Kwa maana hii jamii ina jukumu la kubadilisha hali hii ili kuboresha hali ya maisha ya wanawake.

Katika riwaya hii matukio yamepangwa kiusababishi kwa njia ya kuzua mshtukizo na taharuki. Ili kutimiza lengo hili mwandishi ametumia mbinu ainati kama vile uzungumzinafsi ndani, dayolojia ya ndani, mkondo wa ung'amuzi, ndoto, barua na nyimbo. Mbinu za uzungumzinafsi ndani, dayolojia ya ndani na mkondo wa ung'amuzi zimetumiwa kama mhimili mkubwa wa kudokeza hali za kisaikolojia za wahusika. Mbinu hizi zimesaidia kubainisha namna wahusika wanavyokumbwa na vita vya ndani kwa ndani kwa kudokeza mawazo yao, hisia zao, matamanio yao na makusudio yao.

Kwa kiasi kikubwa urejelezi wa matukio ya nyuma kujaza matukio yaliyotendeka awali umetumika. Mbinu hii inajitokeza kama sehemu ya mbinu nyingine za ujenzi wa ploti kama vile ndoto, uzungumzinafsi, mkondo wa ung'amuzi na barua. Ndoto, barua na nyimbo zimechangia matukio na mawazo muhimu katika mpangilio wa ploti. Aidha, usawiri wa matukio haya kwa mbinu hizi umefanywa kwa njia ya kutoa hisia na makusudio ya wahusika.

Kwa kukamilisha sehemu hii, ni muhimu kutaja kuwa usimulizi aina tatu unajitokeza dhahiri katika kazi hii. Katika matini husika mwandishi amewapa wahusika wengi hadhi ya kusimulia visa vyao kwa njia ya kusawiri hali zao za ndani kwa usimulizi wa nafsi ya kwanza. Aidha, usimulizi wa nafsi ya tatu na usimulizi mwakote umetumiwa kwa njia ya upenyezi na upekuzi ili kudokeza ung'amuzi wa wahusika.

## 2.7 Tanbihi


1. Kwa maelezo zaidi tazama Frye n.w ***Harper Handbook of Literature*** (1985). London: Harper Collins. Uk: 351-352.
2. K.h.j. Meyer, M. , ***The Bedford Introduction to Literature*** (2002). London: Bedford/ St Martins
3. K.h.j. Wamitila, K.W. ***Kamusi ya Fasihi: Istilahi na nadharia*** (2003). Nairobi: Focus. Uk:72-73
4. K.h.j Wafula, R. n.mw. ***Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*** (2007). Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation. Uk: 110-111.
5. K.h.j. Wamitila K.W. ***Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.*** (2008). Nairobi: Vide-Muwa. Uk:154-157
6. K.h.j. Freud, S. ***Five Lectures on Psychoanalysis, Leonardo da Vinci and Other Works*** (1910). London: Hogarth Press. Uk: 69.
7. K.h.j. Mbatiah, M. ***Kamusi ya Fasihi*** (2001). Nairobi: Standard textbooks and Publishing. Uk: 72
8. K.h.j Wamitila K.W. (2003) uk: 325-328.
9. K.h.j. K.h.j. Mohamed, S.A. ***Kunga za Nathari ya Kiswahili: Tamthilia, Riwaya na Hadithi Fupi*** (1995). Nairobi: E.A.E.P. Uk: 84.

# SURA YA TATU

## UMBUJI WA WAHUSIKA KISAIKOLOJIA

### 3.1 Utangulizi

Katika sura hii tunafafanua suala la umbuji wa wahusika kisaikolojia. Kwanza, tunafafanua dhana za uhusika na wahusika ili kuweka msingi wa kuelewa masuala ya kimsingi katika mada hii. Aidha, tunachanganua wahusika wakuu na wadogo na kuonyesha namna ambavyo wahusika hawa wamekuzwa kisaikolojia. Kukuzwa huku kisaikoljia kunatokana na hali wanazokumbana nazo, matukio wanayoshiriki na mitagusano inayotokea kati yao na wahusika wengine au na jamii pana katika mazingira yao. Aghalabu, hali hizi ndizo zinazosababisha athari kwa wahusika na kuibua hisia kali na kuwafanya watatizike kimawazo na kihisia. Jambo hili ndilo linaloleta mhemko wa kifikira na kihisia unaowafanya watatizike kisaikolojia. Wahusika wa aina hiyo ndio wanaotajwa na Njogu na Chimerah (1999:40) kuwa wahusika wa kisaikolojia. Kulingana nao wahusika wa aina hii hukumbana na matatizo mengi ya kijamii na wanaibua hisia za huruma kwa wasomaji.

### 3.2 Uhusika na wahusika

Uhusika ni mbinu zinazotumiwa na waandishi kuwasawiri wahusika katika kazi ya kifasihi. Kwa mujibu wa Shaw (1972:71) uhusika ni umbuji wa taswira za watu wa kufikirika katika drama, riwaya, ushairi au hadithi. Kupitia kwa uhusika viumbe wa kibunifu huwa bainifu kwa msomaji kwa kiasi kwamba anawaona kama watu halisi. Usawiri mzuri wa wahusika unawafanya wasomaji wajitambulishe nao kwa kuhisi wanavyohisi au kuwaza wanavyowaza. Kwa maoni yake, uhusika ni kipengele muhimu cha ujenzi wa ploti. Sababu ni kuwa uhusika ndio unaoendeleza ploti na kwa hivyo ploti hutegemea uhusika katika ujenzi wake. Hivyo basi, bila ya uhusika hakuna tasnifu[1], ploti, au mandhari yatakayozua taharuki kwa msomaji.

Kuna mbinu kadhaa zinazotumiwa kusawiri wahusika. Mbinu hizi ndizo msingi wa uhusika wa kazi ya kifasihi. Kwa mujibu wa Roberts na Jacobs (1992:140-141) kuna mbinu tano muhimu za kuwasawiri wahusika. Kwanza, kuna uhusika kupitia katika matendo ya wahusika. Msanii huwaweka wahusika katika matendo kwenye hali na mazingira mahsusi ili kuonyesha tabia, mitazamo, udhaifu au ukakamavu wao na

ukuaji wao katika matini. Pili, kuna usawiri wa wahusika kupitia maelezo juu ya wasifu wa wahusika na mazingira wanayodhibiti. Maelezo haya hutokea katika nafsi ya tatu. Kwa njia hii tunaweza kupata wasifu wake, hisia zake na mitazamo yake. Kifungu kifuatacho kinasadifu maelezo haya;

> Katika hali kama hii ilikuwepo hamu yake ya kunyanyua sanaa na utamaduni wa kweli wa jamii yake, hadi sanaa na utamaduni vitakapokuwa vitu muhimu vya kupatia watu riziki zao za kila siku za kuendeleza maisha yao. Mohamed K.h.j. (uk:189)

Hapa msimulizi tunayekisia kuwa mwandishi anaeleza azma ya Nana ya kuendeleza utamaduni pamoja na kuwauni maskini katika jamii yake. Kwa hivyo, kifungu hiki kinatudokeza kuwa yeye ni mkarimu na mfadhili wa jamii yake. Aidha, kinaonyesha namna msimulizi anavyopenya ndani ya mhusika huyu na kutufichulia wasifu wake.

Tatu, kuna mbinu ya uhusika kupitia yale wanayosema wahusika wenyewe. Wakati mwingine wahusika hutumia usemi unaoficha malengo yao. Hata hivyo, uchunguzi wa makini wa usemi wao utakufichulia malengo yao na mitazamo yao. Usemi wao unaweza kutokea katika uzungumzinafsi ndani, mkondo wa ung'amuzi, usimulizi wa nafsi ya kwanza na dayolojia ili kudokeza hali za ndani za wahusika. Kwa mfano;

> Hakuzindukana mpaka aliposikia sauti ikimwambia.
>
> "Unaniambaa siku hizi Faisal?".......
>
> " N'najua hujibu kitu hata ukiulizwa," aliendelea Nana huku akijipweteka ubavuni mwa Faisal...
>
> "Aa, sijui kwa nini n'nakuwa hivi siku hizi. N'nakuchama burebure," aliendelea Nana akijaribu kutaka radhi.
>
> "Si burebure," alijibu Faisal ndani ya mawazo yake. Mohamed K.h.j. (uk:253)

Huu ni mfano wa dayolojia inayotufichulia hisia za upweke na huzuni alizo nazo Nana kutokana na kumkosa Faisal kwa muda fulani. Aidha, kinatudokeza kuwa wawili hawa wanaenziana ingawa kuna mshikili fulani uliotokea kati yao.

Nne, kuna mbinu ya uhusika inayotokana na yale wahusika wengine husema juu ya wahusika wenzao. Mbinu hii hutusaidia kujua wanayowawazia wahusika wenzao na kwa njia hiyo hutufichulia tabia zao na mitazamo yao juu ya masuala yanayokuzwa katika ***Nyuso za Mwanamke***. Mwisho, kuna mbinu ya uhusika ambayo inarejelea yale mwandishi anasema juu ya wahusika kama msimulizi au mshuhudiaji wa matukio

katika kazi ya kifasihi. Kupitia katika yale anayosema mwandishi juu ya wahusika tunaweza kubainisha sauti, toni na mtazamo wa msanii.

Kwa mujibu wa Baldic (2001:70) neno wahusika lilitokana na kazi ya Theophratus, ***The Characters,*** katika karne ya tatu kabla ya Kristo. Kulingana naye, lilirejelea viumbe wa kisanaa wanaopatikana katika matini wanaofanana na watu wanaoweza kujulikana katika ulimwengu wa kawaida. Viumbe hawa wanaweza kuwa watu, wanyama, miti, mawe na viumbe wa kufikirika kama vile majitu, malaika, miungu, vizuu au mizuka. Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999:45) wahusika hubuniwa kutokana na mazingira anamoishi msanii. Mazingira haya yanaweza kuwa ya kijiografia, kihistoria, kijamii, kitamaduni au ya kisiasa. Ni muhimu kuelewa kuwa wahusika wa aina yeyote wawe ni watu au viumbe hurejelea na huakisi sifa na tabia za binadamu katika jamii husika. Aidha, wahusika wanafaa wawe wa kuaminika na wenye msimamo thabiti ili waweze kuakisi binadamu katika ulimwengu wa kawaida. Kwa maoni yetu, ili wahusika hawa waaminike, msanii ni sharti awape lugha inayolingana na tajriba zao. Lugha hii lingani huakisi kiwango chao cha kiuchumi, kielimu na kitabaka. Kwa mfano, katika riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke*** mhusika Nana amepewa lugha na mawazo mapevu yanayoonyesha kuwa amesoma na ni msichana wa nyumba kubwa iliyostaarabika.

Wahusika wana dhima kubwa katika kazi ya kifasihi. Kwanza, huwasilisha ujumbe wa mwandishi au msimulizi. Ujumbe huu hutokana na matendo wanayoshiriki, mazungumzo yao, mawazo na hisia zao zinazojitokeza dhahiri katika kazi hiyo. Kwa njia hii maudhui huweza kukuzwa na kudokezwa kwa uwazi zaidi. Pili, wao ni mhimili wa matukio na vitushi katika kazi ya kifasihi na ndio wanaosaidia kusukuma mbele msuko na hadithi ya matini. Tatu, wahusika huwasilisha na huwakilisha binadamu wa kawaida katika jamii na kwa hivyo usawiri wao husaidia kuonyesha wasifu wa binadamu hawa. Kwa njia hiyo husaidia kutukuza na kubeza tabia njema au mbaya katika jamii mtawalia.

## 3.3 Ujenzi wa wahusika kisaikolojia

Usawiri wa wahusika kisaikolojia unakusudia kudhihirisha wahusika wenye sifa zifuatazo. Kwanza, wanaweza kusawiriwa kama wahusika waliokumbwa na mawazo mengi yanayowazagaa kiasi cha kugeuka

ndoto za mchana. Hali hii hudhihirika kwa dalili za kuwapata wakiwa katika tafakuri nzito. Pili, kusawiriwa kwa namna ya kudokeza mawazo na hisia zao za ndani. Usawiri huu hutokea hasa wanaposhiriki katika uzungumzinafsi ndani, dayolojia ya ndani na mkondo wa ung'amuzi. Tatu, kuumia ndani kwa ndani kutokana na kukumbwa na masaibu mengi yasiyo na suluhu. Hali hii wakati mwingine huweza kudhihirika kama kibuhuti, hangaiko au shinikizo la moyo kama inavyotokea kwa mhusika Nana na Faisal katika ***Nyuso za Mwanamke*** na Ndi katika ***Dunia Yao.*** Nne, wahusika wanaweza kusawiriwa kisaikolojia kama wasifu wao unatokea kama motifu katika matini na kujirejelea katika kazi za awali za mwandishi yuyo huyo au waandishi wa eneo moja. Sifa hii ya nne inadhamiria kuchanganua saikolojia ya mwandishi kwa kurejelea motifu za kihusika katika kazi zake na mbinu za mwanzo tatu zinalenga kuchanganua saikolojia ya wahusika. Aidha, wahusika hawa hukumbwa na ndoto zinazodokeza mambo na mawazo ya ung'amuzibwete wao.

### 3.3.1 Wahusika wakuu

Mbatiah (2001:48) anarejelea wahusika wakuu kama wahusika ambao wanajitokeza wazi kuwa ndio nguzo katika kazi ya kifasihi kuliko wahusika wengine. Mara nyingi hawa ndio wahusika waliojengwa vizuri kwa undani zaidi kuliko wahusika wengine. Kwa maoni yetu hili ndilo kundi ambamo hutoka nguli[2] au shujaa wa kazi ya kifasihi. Kwa mfano, katika data ya utafiti huu wahusika wakuu ni Nana na Faisal naye nguli wa kazi hii ni Nana.

Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (K.h.j. uk:41) wahusika wakuu huwa na dhima ya kuisukuma riwaya mbele kwa sababu migogoro na matendo yote muhimu inawahusu. Wao ndio washiriki katika matendo na migogoro muhimu katika kazi. Kwa njia hii wanadhibiti msuko wa matukio makuu na visa au vitushi huzunguka maisha yao. Katika ***Nyuso za Mwanamke*** matukio muhimu yanawazunguka wahusika Nana na Faisal yakiwemo urafiki wa Faisal na Bimkubwa, usasi wa Bimkubwa na Faisal na kutoroka kwa Nana kutoka kwao. Aidha, dhamira kuu na msimamo wa mwandishi hujitokeza kupitia wahusika wakuu. Dhamira na msimamo huu hujitokeza katika matendo na usemi wa wahusika pamoja na maingiliano baina yao. Kwa mfano, matendo na maingiliano kati ya wahusika kama Bimkubwa na Faisal, Nana na Faisal na

Bwana Hila na Nana yanatudokezea dhamira kuwa ni vizuri mwanamke apewe uhuru wa kujiamulia na nafasi ya kujiendeleza.

### 3.3.1.1 Nana

Nana ndiye mhusika mkuu katika riwaya hii pamoja na Faisal. Hata hivyo, yeye anachukua nafasi kubwa kuliko Faisal. Nana ni mwanawe Bwana Hila na Bimkubwa. Hakuwahi kupata malezi ya mama yake kwa sababu baada ya kuzaliwa baba yake alimtaliki mama yake na akalelewa na mama wa kambo Bi. Siri na baba yake. Hali hii ya kukosa malezi ya mama ilimwathiri sana na ikajijenga kuwa mawazo na ndoto kiasi kwamba katika baadhi ya ndoto hizi anamwona mama yake akimnyonyesha (Uk.285). Hali hii ya kukumbwa na mawazo kumhusu mama yake ilimdidimiza na kumzuia kuvunja ungo kama anavyosema mwenyewe katika kifungu kifuatacho;

> Sijui kama unahisi maumivu nihisiyo mimi. Mimi niliyetimbwa na maumivu tokea utotoni nilipokuhitaji zaidi. Mimi ninayeendelea kubeba maumivu hata humu ujanajarini. Maumivu na uchungu wangu wa akili umenizuia nisivunje ungo mapema. (uk:19)

Kifungo hiki kinaonyesha namna mawazo na maumivu ya ndani kwa ndani yalivyo na athari kwa hali za kimwili za kizazi. Kushindwa kuvunja ungo kwa wakati wa kawaida ni ishara moja ya mpagao unaowakumba watu wanaotatizika kisaikolojia kama anavyodai Freud (1899:53). Kutokana na mfano huu ni wazi kuwa athari za kisaikolojia huathiri mfumo wa mwili kihasi.

Hata hivyo, Nana alilelewa kwa tunu na tamasha. Alifanyiwa sherehe chungu nzima kama vile za kuadhimisha siku ya kuzaliwa, kununuliwa gari mpya na kuvunja ungo (uk:29). Sherehe hizi zilifanywa kutokana na ukwasi mkubwa aliokuwa nao baba yake.

Kama ilivyokuwa kawaida ya wazazi wakati wake, Nana alidhibitiwa kwa sheria kali kama kufungiwa ndani ili asipate nafasi ya kutangamana na vijana wa hirimu yake kwa kuhofiwa kuharibiwa na wanaume (uk:118). Ingawa Nana alidhibitiwa hivyo alionyesha ukaidi kwa sheria hizo kama vile kukataa kupelekwa shuleni kwa gari na mchumba aliyechaguliwa (uk:38). Kudhibitiwa huku kulisababisha ubanaji wa matamanio na matarajio ya Nana hasa ya uana kama tulivyotaja hapo juu. Matamanio na matarajio yake

kama vile kutangamana na vijana wenzake, kusuhubiana na wavulana na kuchagua mchumba ampendaye yalimfanya awaogope na asiwaamini wanaume. Hofu hii ni uhawilisho wa aina fulani. Kama tulivyotaja hapo juu, ubanaji ulisababisha Nana kukosa kuzitumia ishara za uana katika wimbo alioimba kumrejelea Amour ambapo Amour anarejelewa kama mwezi ilhali tunajua mwezi hurejelea mwanamke.

Mwandishi pia amemkuza sana Nana kwa kumpa lugha, uwezo, hekima na maarifa yanayolingana na majukumu aliyopewa kuyatimiza. Kwanza, amempa lugha na mawazo yanayoafiki kiwango chake cha elimu kama msichana aliyeibuka kuwa mwanafunzi bora nchini mwake. Kwa mfano, anazungumzia masuala ya kinadharia, kifalsafa, kisiasa na kiuchumi kwa lugha na mawazo mapevu sana (uk:60, 81, 85-86). Ingawa kuna chuku katika jambo hili, kwani hatutarajii msichana wa miaka yake kuwa na mawazo mapevu kama haya ambayo yanaafiki wahadhiri au wasomi wa kutajika, ukuzaji huu unaoana na majukumu yake vizuri. Pili, amempa maarifa ya kiuchumi ya kuanzisha na kuendeleza biashara. Si kawaida katika jamii inayowadhalilisha wanawake kuibuka mwanamke, hasa kijana, kuanzisha miradi mitatu ya kibiashara na kunawiri ilivyonawiri. Yaani, bendi ya taarab na kituo cha redio na runinga (uk:197-198). Tatu, amempa hekima ya kuweza kuendeleza mjadala na Profesa wa Chuo Kikuu, PKA (uk: 275- 282). Nana ambaye PKA alitarajia kumfunza, alitoa hoja nzito zilizompa mafunzo makubwa na kumshangaza. Kwa ujumla mwandishi amemsawiri Nana kama mhusika anayekua kimawazo, kihisia, kimaarifa, kielimu na kiuchumi.

Nana pia amesawiriwa kama mhusika anayepigana kujikomboa kutokana na ubabe wa wanaume. Kama tulivyotaja alikaidi maagizo ya baba yake alipohisi kuwa yalilenga kumnyima uhuru kama binadamu. Baba yake alipompiga aliamua kutoroka nyumbani ili apate uhuru wa kujiendesha na kujiendeleza. Ingawa tabia hii haiwezi kukubalika na wazazi wengi inafidiwa na yeye kujiweka safi kama baba yake alivyong'ang'ania kwa kutokuswa na mwanamume hadi alipoolewa. Katika kujikomboa huku alikataa kudhibitiwa na sheria na itikadi za kijamii na kidini zilizodhamiria kuwakandamiza wanawake. Mwenyewe anasema hivi;

> Nikifumba macho kuangalia kila upande ndani ya jamii yangu, huchukia mno tabia ya mwanamke kuwa mwanamke kwa namna ...zilizopangwa na mwanamume. K.h.j. (uk: 108 )

Ni wazi kuwa anapinga kaida za kumnyima mwanamke haki na uhuru wa kujiamulia katika jamii yake kama binadamu. Kwa njia hii anayatoa yaliyo katika ung'amuzibwete wake bila kuhofia kuenda kinyume na jamii yake tofauti na Asumini katika ***Tata za Asumini*** aliyejiharibu kwa kutofanya lolote. Tofauti hii inaonyesha jinsi wahusika wa kike katika fasihi ya Kiswahili walivyopevuka kuakisi jamii iliyoendelea kijamii na kisiasa kama inavyojitokeza katika mfano huu.

Aidha, Nana kama kiongozi wa waleta mapinduzi alijilinda kimaadili ili asiporomoke kama wanawake wanavyofanya. Kwanza, alikuwa msalihina na mshika dini tabia iliyomsaidia asitetereke kimaadili (uk.98). Pili, hakukubali kujiuza kingono kama ilivyo tabia ya wanawake wengi wanapokosa mahitaji ya kimsingi (uk:158). Tabia hiyo ingemdhalilisha na kumuumbua na hangefika alipofika. Tatu, alijishughulisha na uimbaji na kufanya mazoezi wakati hakuwa na mtaji wa kuanzia biashara (uk:139-140). Shughuli hizi zilimsaidia asipumbae jambo lililomsaidia kutojiingiza katika upotovu. Nne, hakukubali kujidunisha kwa kuwafurahisha watu ilhali anaona anaenda kinyume cha matakwa yake. Jambo hili linatokea pale ambapo anakataa kuajiriwa kuwatumbuiza wateja wa *Hotel Selwa* alipoambiwa anafaa aimbe nyimbo za matusi na kuvaa nusu uchi. Kama mwenyewe anavyosema mahali pengine, alitaka kufuata honne yake, nafsi yake ya ndani. Tano, hakukubali kudharauliwa eti kwa sababu yeye ni mwanamke. Kwa mfano, Ngware alipomtukana baada ya Nana kumtishia kwa kumpiga nyanya yake, alimtia adhabu kwa kumtwanga Ngware hadi akalazwa hospitalini (uk:275). Hoja hizi zinadhihirisha namna Nana ni mhusika anayejidhibiti na kujilinda kimaadili. Mwandishi kumkuza alivyomkuza kulilenga kuonyesha kuwa mwanamke si mtovu wa maadili kama wanaume wanavyomchukulia kama binadamu aliyepotoka kitabia na asiye na msimamo thabiti.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003:181) riwaya ya kisaikolojia huwa na wahusika wanaosumbuka au kusumbuliwa. Usumbufu huu ni ishara ya kutatizika kisaikolojia. Nana kwa kiasi kikubwa amesawiriwa kama mhusika anayetatizika kisaikolojia kwa njia nyingi. Kwanza, tunamkuta akizungumza peke yake. Kuzungumza huku kunadhihirika katika uzungumzinafsi ndani na dayolojia ya ndani pale anapozungumza na mama yake asiyekuwepo, anapojadiliana na nafsi yake ndani kwa ndani na anapozungumza na Bi. Mau

usingizini (uk:18-24, 42,76,81,135-136). Mjadala wa ndani kwa ndani ni ishara ya kukumbwa na vita vya ndani kwa ndani. Vita hivi vinatokana na hali ya kutanzwa na masaibu ambayo hayapati uvumbuzi na kwa hivyo hubaki kama tato la nafsini. Ni vita hivi pamoja na mawazo mengi kumhusu mama yake yanayomsababishia maumivu ya ndani kwa ndani (uk:19, 20).

Hali kadhalika, mhusika huyu amesawiriwa kisaikolojia kwa kule kukumbwa na ndoto za mchana na za usiku. Kwa mujibu wa Freud (1953:48) ndoto hutokana na shughuli za kimawazo na mambo yaliyohodhiwa katika ung'amuzibwete wa binadamu. Hii ndiyo maana ndoto nyingi anazoota zinatokana na mawazo aliyokuwa nayo kuhusu mama yake, mawazo ya kukandamizwa na baba yake na ya mapenzi kumhusu Amour. Kwa mfano, katika mojawapo ya ndoto, Nana anatokewa na mama yake aliyeonekana kuwa katika uchungu wa kuzaa kama taashira ya Nana kuvunja ungo (uk:26-27). Katika baadhi ya ndoto anakumbana na wanawali wanaolia machungu kutokana na dhuluma ambazo wanaume hasa jamaa zao waliwatendea kama ubakaji na kuuliwa vitoto vyao vichanga. Hawa ni Hawa na Mwanamkuu (uk:178-179). Kukumbana na wahusika hawa katika ndoto ni dhihirisho kuwa Nana alipitikiwa na mawazo juu ya ubakaji, mauwaji na ukandamizaji wa wanawake ambayo ni mambo aliyoyashuhudia na kuhadithiwa na jamii yake. Kutokea kwa mambo haya katika ndoto zake ni dhihirisho kuwa mambo haya hutokea katika jamii hii.

Nana pia anaonyesha dalili za kutatizika kisaikolojia kutokana na hali ya kupigwa na kibuhuti na mfadhaiko wa mara kwa mara. TUKI (2004:156) wanadai kibuhuti ni mshtuko au bumbuazi anayokuwa nayo mtu kwa sababu ya fikira au mawazo ya huzuni. Kibuhuti kinachompiga Nana kinatokana na mawazo juu ya kumkosa mama na hali ya kukandamizwa na baba yake. Mfadhaiko na kibuhuti vilikuwa vikimdidimiza katika hali ya kutojitambua kwa muda mrefu sana. Anapokumbwa na mfadhaiko, hutokewa na taswira anuwai za mzuka wa mama yake na kukutana na viumbe wa ajabu (uk: 62-63, 97, 133-134 na 137). Hali hii humlaza kitandani kwa muda mrefu ambapo hawezi kuamka wala kufanya lolote.

Nana ni mhusika anayeonyesha dalili ya kutotulia na kutaka kuzua fujo. Kutotulia hutokana na usumbufu fulani wa kimawazo au kihisia anaopitia mhusika nako kutaka kuzua fujo hutokana na mtafaruku wa

mawazo ambayo humwondoa mtu katika mkondo wa amani na utulivu na anapokumbwa na utata wowote huwa mwepesi wa hasira. Wepesi wa hasira unaonekana anapomkasirikia Faisal bila kosa lolote baada ya majaribio ya kuimba Hotel Selwa (uk:145). Hasira ya mara kwa mara ni dalili moja ya kuwepo kwa kibuhuti. Mfano mwingine ni pale Nana anapokatazwa na mhazili kuwa hakuwa na miadi ya kumwona Meneja Mkuu wa *Hotel Crescent*, anataka kuzusha zogo na anaingia bila kuruhusiwa (uk:162-163). Aidha, anapoongea na Meneja Mkuu anatumia lugha ya matusi na ya kumkashifu. Tabia hii yake inaonyesha ukosefu wa ustaarabu ambao unahitajika kwa kila mwungwana. Uhusika huu wa wepesi wa hasira unaweza kunasibishwa na wa Asumini katika ***Tata za Asumini*** anayewakasirikia wenzake mara kwa mara. Kwa hivyo ni motifu ya kihusika katika kazi hizi.

Tabia ya Nana kumchukia baba yake na kutoroka nyumbani ina kiini chake katika hali yake ya kisaikolojia. Aghalabu, watoto wa kike huwa na mshikamano mkubwa sana na baba zao. Hoja hii inatokana na dhana ya mshikamano wa uana ya elektrika inayomfungamanisha mtoto wa kike na baba yake na kumfanya amchukie mama yake kwa kuchukua nafasi yake karibu na baba. Kwa mujibu wa Frye n.w. ( k.h.j. uk.160) dhana ya elektrika ilitokana na kisasili cha kiyunani ambapo mhusika Elektrika alilipiza kifo cha baba yake Agamemnon kwa kuhimiza mama yake, Clytemnestra auwawe kwa kuhusika na kifo cha baba yake. Dhana hii hutumika kuchanganua saikolojia ya wahusika hasa wa kike wanaoonyesha upendo usio wa kawaida kwa baba zao. Ingawa Nana hamchukii mama yake, anaona mtu wa karibu na ambaye anafungamana naye ni baba. Kwa hivyo, tabia ya baba yake ya kumzuia asitangamane na vijana wengine na kumpiga kibao katika sherehe yake inamshangaza sana Nana kama inavyodhihirika katika kifungu hiki;

> Amenizaba kibao baba! Amenizaba. Kibao amenizaba. Kinauma. Maumivu yake ni ya milele.
> Kimeota shavuni. Alama yake haifutiki. Haitafutika kabisa. K. h. j. (uk:44 )

Uradidi wa kauli hii ni msisitizo kuwa hili ni jambo ambalo hakutarajia litokee na ingawa aliona anamzuia kwa mengi alijua anampenda na hangemfanyia hivyo. Hali hii ilimwathiri Nana sana kiasi cha kuwaogopa wanaume na hakufikiria hata kidogo kuwa angeolewa. Baadaye lakini anakuja kuyahamisha mapenzi kutoka kwa baba yake hadi kwa Faisal aliyemwona mpole, mkarimu na mwaminifu. Uhamishi ni

dhana aliyoibuni Freud inayorejelea tabia ya binadamu ya kugeukia hali au kitu kingine kutokana na kubanwa kwa matamanio yake. Vilevile, anaonyesha tabia ya uhusishi kwa kumhusisha Faisal na baba yake na kumwamini ilhali hakumjua hata chembe kutokana na tabia yake njema. Uhamisho huu wa mapenzi ya baba yake kwa Faisal ni dhihirisho kuwa alimpenda baba yake na haikuwa kupenda kwake kutengana naye.

Nana kwa upande mwingine, amejibainisha kama mhusika anayepigania si maslahi yake tu bali maslahi ya wanyonge katika jamii. Kwanza, anaanzisha kipindi cha *Dukuduku* katika kituo chake cha runinga ambapo wanawake waliodhulumiwa walipata fursa ya kutoa fadhaa zao hadharani. Kipindi hiki kilichangia pakubwa kuhamasisha wanawake kuamka ili wapiganie haki zao (uk:199-211). Alianzisha pia, mradi wa kuwasaidia watoto wanaorandaranda mitaani na vijana wanaotumia madawa ya kulevya. Miradi hii ilichangia kubadili tabia za vijana wengi na kuboresha maisha ya watoto hao. Hali kadhalika, alipinga hali ya ufadhili unaopitia katika mashirika yasio ya kiserikali kuishia katika mifuko ya waratibu na wasomi badala ya kuwanufaisha walengwa ambao ni maskini (uk:191). Tabia hii iliwaacha maskini, mayatima na wajane kuteseka ilhali kama ufadhili ungewafikia wangepata afueni. Usawiri huu unamfanya Nana ajitokeze kama mwanaharakati anayepigania maslahi ya wanyonge na maskini katika jamii yake.

Ingawa Nana amesawiriwa kama mwanamke shupavu, mkakamavu na mwenye busara, yeye ni binadamu tu wa kawaida. Sababu ni kuwa ijapokuwa alikuwa amejiasa kutokudhibitiwa na wanaume, baadaye alisalitika na mapenzi ya Amour na wakafunga ndoa. Mwenyewe anakiri katika kifungu kifuatacho;

> Kwenye ndoa zipo shida ndio-si uwongo, lakini shida ndiyo mbolea ya furaha. Siri ya maisha ukichungua sana, ni maji kupwa na maji kujaa, ni kuzama na kuibuka na kuzama tena, na kuibuka tena; hivyo hivyo mpaka Mungu aichukue roho yake. K.h.j. (uk: 294)

Kutokana na kauli hii ni wazi kuwa Nana anaishabikia ndoa kwa kuziona shida zake kuwa kihamasisho cha kuendeleza ndoa hiyo. Mfano huu unathibitisha kuwa Nana ameweza kumudu hali yake na kurejelea matamanio yake ya awali yaliyohifadhiwa katika ung'amuzibwete.

### 3.3.1.2 Faisal

Faisal ni mhusika mkuu kama Nana. Yeye ndiye aliyekuwa mpenzi wa Bimkubwa na wangeoana kama si vizuizi vya wazee wa Bimkubwa waliomchumbia mume mwingine. Faisal amesawiriwa kama mhusika aliyeelimika hadi kiwango cha juu. Aidha, alikuwa tajiri wa kutajika kule Abudhabi. Aliwahi kuwa Meneja Mkuu wa benki moja kule Abudhabi. Mkewe alikuwa Bi. Matuka na biniye mkubwa alikuwa Amour.

Katika kazi hii Faisal amesawiriwa kama mfadhili na mshauri wa Nana. Kwanza, alipotaka kutoroka alimpeleka kule alikokuwa anakaa na akina Bi. Chuma na Bi. Mau. Haijulikani Nana angetorokea wapi kama Faisal hangekuwepo na hadithi hii ingefikia tamati. Pili, kule walikohamia alichukua jukumu la kumfunza Nana uimbaji, fani ambayo baadaye ilikuja kuwa mojawapo ya biashara yake kubwa alipounda kikundi chake cha taarab. Tatu, alimlipia gharama katika hoteli kubwa kubwa ili wapate nafasi ya kustarehe na kufanya mazoezi kama vile katika *Hotel Selwa* (uk:129-130). Fursa hii ilimsaidia Nana asijihisi mpweke baada ya kutoroka kwao mbali na kumpa wasaa wa kufahamiana na watu wa tabaka lake.

Mbali na hayo, Faisal anajibainisha kama mhusika anayeheshimu vijana na umri wake. Hoja hii ni kweli kwa sababu ingawa alikurubiana na Nana kwa karibu sana alijizuia kumwingilia kingono kwa sababu ya kulinda heshima yake (uk:128). Alifaulu hata ingawa alikabiliwa na majaribu kwa kuvutiwa na msichana huyu aliyefanana na Bimkubwa. Kwa hivyo, uhusiano wake na Nana ulibaki wa baba na binti yake. Hata alipohamia Morishas na kumkuta Suria dada yake Nana na kumpenda, mapenzi yao yalikuwa ya ubinti na ubaba (uk:308). Mbali na hayo, Amour, mwanawe alipomwoa Nana aliona haikuhalisi kukaa nyumba moja na watoto wake kama ilivyo katika jamii husika. Ni msimamo wa aina hii uliomfanya Nana amgande Faisal kiasi cha Amour kushuku kuwa baba yake alikuwa na mahaba na Nana jambo lililomsumbua sana kwa sababu ni Nana yuyo huyo aliyempenda na kumwenzi. Kwa maelezo haya, Faisal amesawiriwa kama mhusika aliyekomaa kimaadili.

Faisal amesawiriwa kama mwanamume anayewajali wanawake na kuwaheshimu kama wanadamu. Usawiri wake huu unatokana na usemi wa Bimkubwa katika barua aliyomwandika Nana (uk:172-173). Katika ujumbe wake anatufichulia kuwa ni Faisal aliyekuwa anamtumia pesa alizomwekea Nana katika benki.

Kati ya wanaume wengi katika jamii hii, Faisal amesawiriwa kama mwanamume wa jamii ya kisasa anayetambua umuhimu wa usawa wa kijinsia. Kwa mfano, kwenye karamu ya kualikwa Amour kwa Nana, aliweza kupika kinyume na ilivyo desturi ya wanaume wanaoona upishi ni kazi ya wanawake. Picha ya mhusika huyu inaweza kurejelewa kama msimamo wa mwandishi wa namna anavyolichukulia suala zima la usawa wa kijinsia kutokana na kutangamana kwake na watu wa asili mbalimbali ulimwenguni.

Kama Nana, Faisal amesawiriwa kama mhusika anayetatizika kisaikolojia. Ukweli wa kauli hii unabainika katika kauli ifuatayo;

> ..Faisal anasibiwa na ugonjwa ule ule wa Nana. Ingawa yeye ugonjwa wake una sababu na taathira tofauti. ...Taathira ...hii ya kuwa mnyonge. Hana uchangamfu,mkimya au mtu kasoro mwenye ububu. K. h. j. (uk:149)

Linalodokezwa hapa ni kuwa matatizo ya kimawazo na kihisia yaliyomkumba ndiyo yaliyomkabili Nana kama kupigwa na kibuhuti, kukumbwa na mpagao na shinikizo. Nana alipokumbwa na mpagao (uk:62-63) mwenyewe anatufichulia kuwa shida hiyo kama anayeifahamu. Kuna baadhi ya siku ambazo alipokumbwa na mawazo alianza kudidimia kwenye mpagao au kibuhuti lakini tofauti na Nana hakufika mpaka kwenye kiini cha chini (uk:154-155). Lililo dhahiri ni kuwa Faisal amejifunza kumudu hali hii kwa kuizoea kuliko Nana.

Ushahidi mwingine wa kuonyesha kuwa Faisal anasumbuliwa na mawazo ya ndani kwa ndani ni kule kuamua kuhama nyumbani kwake na kuacha kazi yenye kipato kikubwa, biashara yake na familia yake. Hili si tendo la kawaida kwa mtu wa haiba yake. Kama anavyotudokezea hapa alikuja kumtafuta mtu ambaye bila shaka ni Bimkubwa.

> Kaambiwa na sauti asiyoijua: *nenda kamtafute.* ...yumo hivi anamtafuta. Kaacha kasri lake Abudhabi. Kaacha mkewe na watoto wake. Kaacha watumishi wake. Kazi yake. Mali yake. Yumo katika msuko wa kutafiti na kutafuta. K.h.j. (uk:4)

Kutokana na kauli hii ni wazi kuwa usasi wa Faisal wa Bimkubwa huku ana mke wa heshima unamfanya aonekane kama mtu anayekumbwa na maradhi fulani (uk:154). Tendo hili linakiuka kaida za kitamaduni zinazopinga mwanamume kumfuatilia mwanamke kwa mapenzi kwani mke mtu hupata kwa kuchaguliwa

na wazazi. Hata hivyo, ulimwengu wa Faisal ni tofauti na jamii yake. Kwa mtazamo wa mwandishi ni kama anachezea moto kwenye mchanga kwani anayetafutwa si binadamu tena bali ni wehu (uk:3).

Faisal vilevile ni mhusika anayekumbwa na ndoto za mchana. Kwa mujibu wa Freud K.h.j. ndoto za mchana hutokana na mawazo mengi yanayompitia binadamu. Faisal alikumbwa na mawazo mengi kumhusu Bimkubwa. Hii ndiyo sababu anaweza kukumbuka kwa usahihi vile walivyokuwa wanakutana na yale waliyofanya pamoja (uk:251-252). Katika baadhi ya ndoto hizi anaona taswira za Bimkubwa kiasi kwamba alipomwona Nana akija aliamini kuwa alikuwa Bimkubwa. Jambo hili lilizua hamaniko kubwa sana kwake hadi aliposikia Nana akimwita ndipo akazinduka. Ndoto za mchana ni dalili ya watu wanaokumbwa na kibuhuti na mpagao mara kwa mara,[3] anayeumia ndani kwa ndani na anayeteswa kiakili.

Fauka ya hayo, Faisal anaonyesha kutatizika kisaikolojia kutokana na tabia ya kuzungumza peke yake. Uzungumzi huu ni ushahidi kuwa mhusika huyu analo tato la kindani lililomlemea. Hali hii inatokea wakati anashiriki uzungumzinafsi ndani unaoambatana na maswali ya balagha ya kujisaili ndani kwa ndani. Mfano huu unaonyesha hali hii.

> Faisal alijiuliza: Nini uzawa? Nini uhai? Nini uwananchi? Nini uraia? Nini kuwepo? Nini maana ya nafasi ndogo isiyo na mwisho? Nini nafasi kubwa yenye upeo mdogo tu wa kujifaragua? K.h.j. (uk:150)

Faisal anasaili kuwepo kwake na maana ya yeye kuwa mtu mwenye nafasi kubwa ambayo haina maana yoyote kwake. Hafurahii mali yake na familia yake ilhali wengi hutamani kuwa katika nafasi hiyo. Huu ndio uchangamano wa maisha ya binadamu. Hali ya kuzungumza peke yake pia ni dalili ya kuwa na vita vya ndani kwa ndani na mawazo chungu nzima yasiyo na uvumbuzi.

Hali ya Faisal kumpenda Nana kwa kumnasibisha na Bimkubwa ina dhima fulani ya kisaikolojia. Alimpenda kwa kutanzwa na sura yake ya kuvutia iliyofanana na ya Bimkubwa na kwa sababu alimkosa Bimkubwa. Huu ni uhusishi kama tulivyokwisha kutaja. Aidha, hali ya yeye kumpenda Nana na kwa wakati huo huo anapendwa na Amour pia ni jambo lenye dhima ya kisaikolojia. Tendo hili linadhihirisha dhana ya Freud ya uana ya Edipode ambapo watoto wavulana huwa katika mashindano na baba zao kummiliki mama. Ingawa Nana si Bi. Matuka lakini kwa kiasi fulani anamwakilisha kwa kuwa na usuhuba

na Faisal. Hali hii imo katika mfumo wa ubinadamu na kwa hivyo hata kama anayegombewa si mama hasa sababu ni dhana hiyo hiyo ya Edipode. Jambo hili linaweza kuwa limetokana na hali ya Amour kutwikwa majukumu mapema kabla hajatangamana na ulimwengu wake ipasavyo. Kwa sababu hiyo hakuweza kutoka katika mashindano hayo. Mshindi katika mchuano huo alikuwa Amour. Faisal aliposhindwa alihamia Morishas. Hata ingawa mapenzi yake kwa Nana hayakuwa mahaba hangevumilia kukosa mapenzi yake Nana ilhali alikuwa karibu naye.

Faisal pia, anaweza kusemwa kuwa mhusika aliyeemewa na hali iliyomkumba na kwa hivyo hakutaka kujitambulisha na tabaka lake. Hii ndiyo sababu alijizika katika muziki wa taarab taaluma ambayo ilidharauliwa wakati wake (uk:46). Kwa kujiingiza katika uimbaji kwa gharama ya mapeni, alitaka kujigeuza kuwa mchochole. Hali hii pia iliambatana na mavazi aliyokuwa akivaa ambayo hayakuakisi tabaka lake ingawa upekuzi wa Nana uligundua mng'aro wa utajiri katika uso wake. Kujigeuza huku kwa Faisal ni uhawilisho wa matamanio yake kwa mambo mengine ambayo ni uimbaji na uchochole.

Usawiri wa Faisal kwa ujumla kama mhusika wa kiume unaonyesha mapinduzi makubwa katika usawiri wa wahusika wa kiume katika kazi za Said Ahmed. Sababu ni kuwa wahusika wengi wa kiume huwa mababe au wanapotaabika si kwa kuathirika na wanawake bali na shida za kawaida. Katika mhusika huyu tunaona taswira ya mwanamume anayeona wanawake kama wenzi na kwa hivyo wanafaa kuheshimiwa. Kupitia mhusika huyu Said Ahmed Mohamed amedhihirisha jinsi riwaya ya kisaikolojia imeweza kupanuliwa kwa kuingiza masuala ya usawa wa kijinsia, haki za watoto na usasa. Kwa njia hii ameonyesha kuwa fasihi ya Kiswahili haizungumzii tu masuala ya kijadi yaliyozoeleka bali inaweza kuyapa masuala ibuka nafasi ili kuakisi jamii inayobadilika kama ilivyo fasihi ya Ki-ulaya.

### 3. 3.2 Wahusika wadogo

Nthenya (2007:84) anawaona wahusika wadogo kama walio na uhusiano wa karibu sana na wahusika wakuu. Hawa ndio wahusika wanaowasaidia wahusika wakuu kujengwa vizuri ili waeleweke. Wahusika wadogo huwa katika kundi mahsusi, yaani kundi la nguli au kundi la mkinzani wa nguli. Katika kazi hii katika kundi la nguli, kuna wahusika wadogo kama Bimkubwa, Bi. Chuma, Bi. Mau na Amour. Katika

kundi la mkinzani kuna wahusika wadogo ambao ni Bwana Hila, Bi. Siri na Ngware. Katika kazi nyingi za Said Ahmed kundi la mkinzani huwa na wahusika wachache. Uchache huu unaweza kuelezewa kuwa wengi huwa ni watu wa daraja la juu ambao si wengi katika jamii.

### 3.3.2.1 Bimkubwa

Bimkubwa alikuwa mpenzi wa kwanza wa Faisal na walikuwa na makubaliano ya kuoana baadaye. Hata hivyo, makubaliano yao hayakutimia kwa sababu kufuatana na desturi za kijamii neno mapenzi halikuwa na mashiko kwani jukumu la kuchagua mchumba lilikuwa la wazazi. Yeye ndiye mama yake Nana na mke wa kwanza wa Bwana Hila. Bimkubwa ni mhusika mdogo kwani sehemu kubwa ya maisha yake inajitokeza katika wahusika wakuu, Nana na Faisal, wakati yeye mwenyewe alikuwa amefariki. Kwa sehemu kubwa amesawiriwa kama mzuka.

Aliwahi kuolewa na wanaume wawili baada ya kutalikiwa na Bw.Hila. Hawa ni Simai na Selemani Kijogoo. Ndoa zote zilikuwa za kitumwa na dhuluma tupu. Ni ndoa hizi zilizochangia kuathirika kwake kimawazo na kihisia. Ndoa yake ya kwanza ilichangia kwa kumfungia ndani na kumnyima uhuru wa kutangamana na watu wengine (uk:.287). Hali hii ya kufungiwa ndani ilimfanya avurugike kimawazo na athari yake ikawa jaribio la kutaka kumwua mume wake. Ndoa yake ya pili ilikumbwa na kupigwa na kwa hivyo haikudumu. Ndoa ya tatu ilipojiri tayari alikuwa amevurugika kimawazo na kihisia. Hali hii ilimfanya ajiachilie tu kwa kila jambo alililotendewa na Selemani Kijogoo na ndiyo iliyomgeuza mwendawazimu. Uwendawazimu huu ndio uliomwangamiza Selemani alipotaka kimwadhibu Bimkubwa (uk:290-291).

Kwa ujumla, Bimkubwa amesawiriwa kama mhusika aliyedhalilishwa na kukandamizwa na wanaume. Hii ni motifu inayojitokeza katika usawiri wa wahusika katika riwaya za Said Ahmed. Kwa mfano, Maimuna katika ***Utengano,*** Semeni katika ***Asali Chungu*** na Bi. Kikuba katika ***Babu Alipofufuka.*** Wahusika wa kazi hizi wanakandamizwa na kuteswa kama alivyofanyiwa Bimkubwa. Kwanza, aligandamizwa na baba yake kwa kumnyima fursa ya kujichagulia mchumba ambaye kwa kuolewa naye ndoa ingedumu kwani hata na yeye Faisal ndoa yake haikudumu bila ya Bimkubwa. Pili, alikandamizwa na waume zake hali iliyovuruga

akili zake hadi akawa mwendawazimu. Tatu, alikandamizwa na jamii kwa kukataa kumtetea ilhali walishuhudia yote aliyotendewa. Hii ni kwa sababu jamii ina jukumu la kuwatetea wanyonge. Wanawake wenzake hasa mama na shangazi yake walikuwa na jukumu la kumpa msaada kwa kumtetea lakini hawakufanya hivyo. Pia, alidhalilishwa na mwajiri wake Subash aliyembaka. Kitendo hiki kilimshikisha mimba akamzaa dada yake Nana, Suria lakini alitendewa dhuluma kwa kunyang'anywa mtoto huyo baada ya siku arobaini tu (uk:288-289). Usawiri huu wa Bimkubwa kama mhusika wa kike aliyedhulumiwa kama ilivyo katika riwaya nyingine za mwandishi huyu ni dhihirisho kuwa jamii husika bado inawadhulumu wanawake. Kwa maana hiyo usawiri huu unalenga kuipiga vita tabia hii.

Katika kazi hii maisha ya Bimkubwa yanasimuliwa kwa mikondo miwili. Mkondo wa kwanza ni ule unamdokeza Bimkubwa kama binadamu na mkondo wa pili unamdokeza kama mzuka. Bimkubwa mwanadamu amepewa sehemu ndogo sana kwani hatumsikii wala hakuonekana waziwazi bali alijitokeza tu kidogo na kukamilisha kusudi lake la kumjeruhi Faisal. Kwa upande mwingine, Bimkubwa mzuka anajitokeza kama sehemu ya mawazo, ndoto na fikira za binti yake. Kutokea huku kwa Bimkubwa katika fikira za Nana kunadhihirisha mafungamano ya mapenzi kati ya Nana na mama yake. Aidha, hali hii ni mbinu ya mwandishi kuonyesha kuwa watu hawafi na kupotea bali kuna vile wanavyorejea kwa jamaa zao kwa ndoto, kumbukizi na kihisia.

### 3.3.2.2 Amour

Amour ni mwanawe Faisal na Bi. Matuka. Yeye ndiye aliyemwoa Nana na kuwa baba yake Faisal mdogo. Baada ya baba yake kufunga safari ya ghafla alimwachia hatamu ya kusimamia biashara yake. Aliifanya kazi hii kwa bidii sana na biashara ikaimarika sana. Namna alivyofanya kazi hiyo kunaonyesha jinsi alivyokuwa kijana mwenye maarifa na bidii. Baada ya mama yake kumwona amepoteza hamu ya chakula na maisha aliingiwa na wasiwasi na akamshauri kuoa bibi. Yeye ni mhusika mdogo ambaye kutokea kwake katika matini kunasaidia kumkuza Nana na Faisal na kutufanya tuwaelewe zaidi.

Katika kazi hii Amour amesawiriwa kama mwanamume wa kisasa anayemwona mwanamke kuwa mwenzi. Kwanza, hashtuki Nana anapompendekezea mapenzi (uk:265). Sababu hapa ni kuwa tayari alijua Nana

alimpenda na kwa hivyo hakuwa na sababu ya kuficha hilo. Pili, alikuwa mpishi mzuri na hakuaibika kupika kwa Nana alipoalikwa ingawa kwa mujibu wa desturi za kijamii alistahili kupikiwa na akaribishwe kama mgeni (uk:272-273).

Amour ndiye aliyebadilisha msimamo wa Nana wa siku zote kuwashuku na kutokuwaamini wanaume. Mabadiliko haya yalitokana na namna alivyojibadilisha alipokuwa anamsaka Nana kwa mapenzi. Aidha, kwa tabia yake alimfanya Nana aamini kuwa wanaume wote si sawa na kuwa ndoa ni shule kama tulivyodokeza hapo awali.

Kupitia mhusika huyu mwandishi, kama tulivyotaja hapo juu, anaonyesha kuwa kuna wanaume waliobadilika katika jamii hii kwa kukaribisha usawa wa kijinsia. Aidha, anawakilisha jamii iliyostaarabika kutokana na utangamano wa kitaifa na kimataifa katika ulimwengu wa utandawazi.

#### 3.3.2.3 Bi. Mau

Bi. Mau alikuwa mama yake Bi. Chuma na nyanya yake Bimkubwa. Yaani, alikuwa nyanya mkuu wa Nana. Waliishi katika makazi mamoja na Bi. Chuma, Faisal na Nana. Alikuwa akikumbwa na ugonjwa wa kifafa mara kwa mara (uk:69). Yeye ni mhusika mdogo anayesaidia tumwelewe Bimkubwa na Nana.

Katika kazi hii, Bi. Mau amesawiriwa kama mkongwe wa ajabu sana. Kuna wakati angemgongea Nana mlango usiku na kumwambia kuwa anamjua yeye na asubuhi anapomuuliza anakataa katakata. Aidha, alikuwa akipigwa na kibuhuti tu kama Nana na kutatizika ndani kwa ndani (uk:70). Kuna wakati hali hii ingemdidimiza hadi kiwango cha chini sana. Hali hii kama tulivyotaja hapo juu ilitokana na yeye kuwa na mawazo mengi kumhusu Bimkubwa na maisha magumu waliyopitia.

Hali kadhalika, Bi. Mau ni mhusika anayekumbwa na ndoto nyingi hasa za usiku. Katika baadhi ya ndoto hizi walikutana na Nana uso kwa uso (uk:175-176). Aidha, katika baadhi ya ndoto aliweza kumwona Bimkubwa akimnyonyesha na kumbembeleza Nana. Kama tulivyotaja, ndoto hizi zilitokana na kumbukumbu za mawazo na mambo aliyoyashuhudhia au yaliyo katika fikira zake. Pia, Bi. Mau alijibainisha kama mtabiri wa mambo kwa usahihi kama alivyotabiri kuwa kitukuu wake Nana atakuja

kuishi nao na ikatimia hivyo.

#### 3.3.2.4 Bi. Chuma

Bi. Chuma ni mama yake Bimkubwa, Tuwera, Mize na Ngware. Yeye ni nyanya yake Nana. Aliishi mjini Sambejambe katika mtaa mmoja wa madongoporomoka. Walikuwa watu wa kipato cha chini na hata makazi hayo walikoishi walijenga kwa msaada wa mume wa binti yao. Katika riwaya hii yeye ni mhusika mdogo au msaidizi. Amesaidia kuwapa makazi wahusika wakuu na kwa njia hiyo kusaidia kuwakuza.

Bi. Chuma amesawiriwa kama mwanamke mkarimu sana. Kama kiongozi wa nyumba ile, alikuwa tayari kuwasaidia watu wa kila sampuli waliohitaji msaada wake. Kwanza, yeye na mama yake wanaonekana kuwa watu wa pekee waliomtembelea Faisal alipokuwa hospitalini (uk:241-242). Na baada ya kutoka hospitalini walimnasihi akae kwao ingawa alikubali kwa sharti la kulipa kodi. Pili, Nana alipotoroka kwao yeye ndiye aliyemkaribisha na kumfaa kwa kila hali. Alipokuwa mgonjwa alikuwa karibu kumhudumia na kumfariji (uk:65-66).

#### 3.3.2.5 Shemsa

Shemsa ni mhusika anayetokea katika kazi hii kwa kushiriki katika kipindi cha *Dukuduku*. Katika kipindi hiki anasimulia namna alivyodhulumiwa na wazazi wake na mume wake Sadiki. Kwanza, ilikuwa vigumu sana kwake kuanza kuhadithia kisa chake. Hali ya kutokuwa tayari inatokana na kaida za jamii husika kutotaka mwanamke afichue yanayomsibu kwa hofu kuwa atachukuliwa kuwa mwanamke mchafu (uk:206).

Katika kisa chake (uk:203-211) alichaguliwa mchumba mara tu alipovunja ungo. Ingawa alikataa katakata alishinikizwa na kulazimishwa kuolewa na Sadiki. Baada ya kuolewa ndoa yake iligeuka balaa na utumwa kwani alifanywa mtumishi wa mume wake, familia yao na marafiki zake kwa kila aina ya utumwa. Mbali na utumwa wa kawaida, inaelekea hata Sadiki alitaka mke wake akubali kushiriki ngono na baadhi ya jamaa zake na rafiki zake (uk:211). Ni wazi kuwa Sadiki hakumpenda mkewe kama ilivyokuwa desturi ya wanaume katika jamii hii.

Kutokana na kisa hiki ndoa ya Shemsa ni kielelezo cha namna ndoa katika jamii hii zilivyogeuka kuwa jela za kuwafungia wanawake na kuendeleza mateso kwao. Ndoa kama taasisi ya mafungamano ya mke na mume inastahili kujengwa katika misingi ya mapenzi, uaminifu, makubaliano na kuheshimiana. Ndoa ya aina hii ndiyo itakayoleta furaha na kuwa kitulizo kwa dhuluma wanazopata kule nje.

### 3.3.2.6 Bwana Hila

Bwana Hila ni baba yake Nana na Imu. Yeye ndiye aliyekuwa mume wa kwanza wa Bimkubwa. Baada ya kumpa Bimkubwa talaka alioa mke mwingine Bi. Siri. Bwana Hila alikuwa mkwasi wa kutajika na kiongozi wa serikali. Kutokana na utajiri wake aliishi maisha ya kifahari (uk:29). Yeye ni mhusika mkinzani anayempinga nguli ambaye ni Nana. Pamoja na kundi la wachache hawakutaka kuona wanawake wakitendewa haki na kuwa na uhuru wa kujiamulia kama binadamu.

Katika kazi hii amesawiriwa kama kiongozi mfisadi (uk:36-37). Aliuendeleza ufisadi serikalini na kuwanyang'anya majirani mashamba yao. Tabia hii ndiyo iliyomsaidia kupata mali kwa haraka na kutajirika baada ya muda mfupi. Serikalini alijipatia mali kwa kuwekeza mitaji serikalini na nje ya serikali. Baadhi ya shughuli zake za kibiashara zilikuwa za kisiri. Hii ni tabia ambayo haikuendelezwa na Bwana Hila pekee bali na viongozi wengi wa jamii hii. Bwana Hila ni kielelezo cha viongozi wafisadi, wasiojali maslahi ya wanyonge na wenye lengo moja tu ; kujitajirisha.

Bwana Hila pia amesawiriwa kama mhusika anayetaka kuendeleza haiba yake na maslahi ya tabaka lake la juu. Hili linaonekana anapomchumbia Nana, Dusa, kijana ya rafiki yake, ambaye alikuwa kufu yao (uk:44-45). Kwake aliona Nana atafurahia uchaguzi huu na maisha yake yangekuwa yenye furaha. Hata hivyo, hakujua kuwa Nana alikuwa binti asiyetetereka katika msimamo wake kwani kwa Nana msingi wa ndoa ni mapenzi (uk:42). Ingawa Nana hakuwa na uhusiano wa kimapenzi na Faisal, baba yake alimwona kama asiyefaa kumkaribia binti yake na kwa hivyo alibisha kualikwa kwake katika sherehe ya kuadhimisha siku ya kuzaliwa kwa Nana (uk:47).

Bwana Hila pia amejitokeza kama mwanamume anayewakandamiza wanawake. Usawiri wa aina hii pia ni motifu inayojitokeza katika riwaya nyingi za Said Ahmed Mohamed kama vile Makusudi katika ***Utengano,***

Fauz katika ***Dunia Mti Mkavu,*** Bwana Juba katika ***Kiza Katika Nuru*** na K katika ***Babu Alipofufuka.*** Alipomwoa Bimkubwa kama tulivyotaja hapo juu hakumpa uhuru wowote. Vilevile, alimfungia Nana na hakutaka atangamane na vijana wengine (uk:36). Ukandamizaji huu uliwanyima wawili hawa uhuru na kuwafanya wavurugike kimawazo. Hali hii ndiyo iliyomfanya Nana amwaze mama yake sana kwa kufikiria kuwa pengine mama yake angekuwepo angekuwa na uhuru zaidi. Aidha, aliendeleza ukandamizaji kwa kumnyang'anya Bimkubwa mtoto wao na kutokumruhusu kuonana naye. Jambo hili lilifanya Nana ayakose malezi ya mama yake kama vile kunyonya, kupakatwa na kushauriwa. Bwana Hila pia anaonyesha ukandamizaji kwa wanawake kwa kumtuma Ngware kuchoma nyumba ya Nana kama mwenyewe anavyokiri kabla hajafa (uk:306). Mwisho, anaonyesha ukandamizaji kwa kumzaba Nana kibao kwa kuwa alimkaribisha Mpiga-gita katika sherehe yake.

Ingawa Bwana hila anajitokeza kwa mengi mabaya kwa upande mwingine alimfadhili binti yake kwa mengi yaliyomfaidhi baadaye. Kwanza, alimpeleka shuleni ambako Nana alionyesha maendeleo mazuri. Pili, alimnunulia matoba kwa matoba ya vitabu ingawa yeye hakuelimika sana (uk:119). Hali kadhalika, maisha ya tunu na tamasha aliyompa yalimsaidia kustaarabika na kuelewa namna anastahili kutangamana na watu wa tabaka la juu kama vile Faisal. Pia, alimfadhili kwa kumnunulia gari. Kwa hivyo, usawiri wake hasi unatokana na kuathirika na mfumo wa jamii alimoishi ambao badala ya kuubeza aliushabikia kwani walioupinga walikuwa wachache sana.

Mwisho wa Bwana Hila ulikuwa wa kusikitisha. Sababu ni kuwa baada ya kuishi maisha ya haiba alikuja kupoteza umaarufu wake serikalini na kwa hivyo mkono uliomshikilia ukakatika ghafla. Kwa hivyo, alifilisika na huenda baadhi ya mali ilitwaliwa kulipia madeni. Alifariki akiishi katika madongoporomoka.

Usawiri huu wa Bw. Hila unaonyesha jinsi hatima ya watu wanaowakandamiza wengine katika jamii itakavyokuwa. Aidha, usawiri huu unaonyesha namna ambavyo jamii ya kisasa inapinga ubabedume na kupigia debe haki za kibinadamu na usawa wa kijinsia pamoja na haki ya urithi wa mali. Kwa njia hii, mwandishi amemtumia Bwana Hila kama taashira ya ubabedume usio na nafasi tena katika jamii ya kisasa.

#### 3.3.2.7 Ngware

Ngware ni mwanawe Bi. Chuma na mjukuu wa Bi. Mau. Yeye ni ndugu yake Bimkubwa, Tuwera na Mize. Alikuwa kitindamimba wa Bi. Chuma. Ngware alianza kutumia madawa ya kulevya katika umri mdogo. Matumizi ya mihadarati yalihitaji pesa na kwa hivyo hitaji hili lilimsukuma katika wizi hadi akaja kuwa jambazi (uk:104). Inaelekea hakuna mtu aliyemwonya mapema dhidi ya tabia hii.

Ngware pia ni mhusika anayetatizika kisaikolojia kwa vile ameshindwa kutangamana kinidhamu na familia yake na jamii pana. Kushindwa huku kumetokana na tabia yake ya kutumia mihadarati, uraibu ambao umemfanya achanganyikiwe kiakili na kwa njia hiyo aridhie matakwa ya wahalifu na uhalifu kiasi cha kudhulumu hata jamaa yake kwa kuwaibia na kuwapiga.

Ngware anawasilisha na kuwakilisha kundi la vijana wa wakati wake ambao wamepotoka kimaadili na wengi wamekuwa wafungwa wa mihadarati. Hali hii imechangia utovu wa adabu, wizi na ujambazi. Akiwa katika hali hii ndipo Bwana Hila alimtuma kuichoma nyumba ya Nana. Ni vijana kama hawa ambao Nana alikuwa na maono ya kubadilisha alipoanzisha mradi wa kubadili tabia za vijana wanaotumia madawa ya kulevya.

## 3.4 Hitimisho

Katika kazi hii wahusika wengi wamesawiriwa kisaikolojia. Wamesawiriwa kwa mbinu kama vile uzungumzinafsi ndani, kwa kukumbwa na ndoto, mkondo wa ung'amuzi na kadhalika. Wahusika ambao wamesawiriwa kisaikolojia ni wale wanaoonyesha hali ya kutatizika kimawazo na kihisia. Hawa ni wahusika kama vile Nana, Faisal, Bimkubwa, Bi. Mau na Amour. Usawiri huu una athari kubwa kwa utanzu wa riwaya kwa ujumla na hasa kitanzu cha riwaya ya kisaikolojia hasa kwa kuonyesha jinsi ukuaji kihusika wa riwaya hii ulivyo. Aidha, usawiri wa wahusika wengi wanaotatizika kimawazo ni dhihirisho kuwa jamii yetu imebadilika sana. Mabadiliko haya yanaonyesha kwamba idadi ya watu wanaokumbwa na matatizo ya kisaikolojia inazidi kuongezeka katika jamii. Mbali na hayo, umbuji wa wahusika unaojitokeza unaonyesha uchangamano wa binadamu ulivyo kwa namna ulimwengu unavyoendelea kubadilika mbali na kuwa ubunifu wa kihusika wa mwandishi umepevuka kwa kiasi kikubwa.

Katika uchunguzi wetu wahusika wanaojibainisha kama wahusika wakuu ni Nana na Faisal. Hawa ni wahusika ambao tumekumbana nao kutoka mwanzo hadi mwisho wa kazi hii. Hata hivyo, Nana ndiye aliyekuzwa zaidi. Mhusika Nana amesawiriwa kwa njia tofauti na ilivyo kawaida katika riwaya za Said Ahmed Mohamed kwani anajitokeza kama mwanamke anayepigania maslahi yake na kufaulu. Nana anaweza kutajwa kuwa mhusika wa kimapinduzi na kiharakati kwa sababu ya kuazimia kubadili dhana ya usawa wa kijinsia na haki za wanawake. Kwa upande wake, Faisal amejitokeza kama mwanamume tofauti sana na wanaume katika kazi nyingi za mwandishi huyu na fasihi ya Kiswahili kwa ujumla kwa kuwaheshimu na kuwajali wanawake. Mhusika huyu pamoja na Amour wanaweza kuangaliwa kama wahusika wa kisasa kwa sababu kwamba wanaakisi mabadiliko ya kijamii ya kuona mwanamke kuwa sawa na mwanamume.

Wahusika katika kazi hii wamegawika kuwili, kundi la nguli na la mkinzani. Ni upande wa nguli unaotupa wahusika wakuu kama dhihirisho kuwa mwandishi anaunga mkono upande huo na kuwa dhamira na falsafa yake inatokana na mambo wanayoyasimamia. Upande wa mkinzani una wahusika wachache sana na mwandishi haonyeshi ari ya kuwajenga kwa undani. Hali hii inaonyesha kuwa hawatilii maanani na badala yake anawadhalilisha na kuwabeza.

Umbuji huu wa wahusika unadhihirisha mabadiliko ya kijamii na masuala ibuka hasa ya haki za kibinadamu na usawa wa kijinsia yanayopinga ubabe katika jamii na kupiga vita tabia za kuwadhulumu wanawake na wanyonge katika jamii. Aidha, usawiri wa wahusika wanaosumbuka na kusumbuliwa kimawazo ni dhihirisho la watu katika jamii kukumbwa na matatizo mengi ya kijamii katika maisha yao.

### 3.5 Tanbihi

1 Kwa maelezo zaidi tazama Wamitila K.W, ***Kamusi ya Fasihi : Istilahi na Nadharia*** (2003). Nairobi: Focus. Uk: 225

2 K.h.j. Mbatiah, M. ***Kamusi ya Fasihi*** (2001). Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing. Uk: 64

3 K.h.j Freud, S. ***Pre-Psychoanalytic Publications and Unpublished Works.*** London: Hogarth press. Uk: 50.

# SURA YA NNE

## MAUDHUI

### 4.1 Utangulizi

Katika sura hii tunazungumzia suala la maudhui. Kuhusu suala hili tunafafanua kwa tafsili suala la maudhui ili kuweka msingi wa uelewa wa masuala ya kimsingi katika sura hii. Kishaye, tunaliangalia suala zima la maudhui katika *Nyuso za Mwanamke* kama motifu muhimu zinazojitokeza na kujirejelea katika riwaya nyingine za Said Ahmed Mohamed. Aidha, tunayaangalia maudhui kama masuala yanayoakisi hali halisi katika jamii iliyosawiriwa.

Kuna maudhui kadha wa kadha ambayo yanajitokeza katika riwaya za Said Ahmed Mohamed. Maudhui haya ni kama ukombozi wa mwanamke, ukoloni mamboleo, mapinduzi, malezi, utawala mbaya, utamaduni na itikadi, uozo wa kimaadili, ufisadi, ubinafsi na utengano katika jamii. Karibu masuala haya yote yanajitokeza katika kazi hizi kwa kiasi fulani. Hili ni dhihirisho kuwa masuala haya yanajitokeza katika jamii husika zinazosawiriwa na kazi hizi. Inaelekea haya ndiyo masuala yanayomshughulisha sana mwandishi kifikira na kumwathiri kimawazo na kihisia. Masuala haya yanajitokeza kama motifu za kimadhui katika kazi hizi.

Motifu, ni elementi fulani ya kimuundo au kimaudhui inayotawala kazi fulani. Elementi hii ya kimuundo inaweza kuwa uhusika wa aina fulani, mandhari, tamathali, dhamira, falsafa au mtindo fulani. Kwa mujibu wa Wamitila (2003:132) motifu pia inaweza kurejelea wazo kuu na sehemu ya dhamira katika kazi ya kifasihi ambacho ni kipengele mojawapo cha motifu. Kwa maelezo haya, maudhui ni kipengele kimoja cha motifu. Katika kazi za Said A. Mohamed, maudhui ya ukombozi wa mwanamke, malezi, utamaduni na itikadi, uongozi mbaya na uozo wa kimaadili hujitokeza kama motifu. Hivyo basi, uchunguzi wetu wa maudhui katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* unalenga kubainisha maudhui kama motifu katika kazi hii na katika kazi za awali. Maudhui kutokea kama motifu ni dhihirisho la mawazo au saikolojia ya mwandishi huyu na jamii yake. Na hii ndiyo sifa mojawapo ya nadharia ya saikolojia changanuzi.

## 4.2 Tafsili ya maudhui

Maudhui yanaweza kuangaliwa kwa ujumla kama yaliyomo katika kazi ya kifasihi. Kulingana na Holman (1976: 528) maudhui ni suala kuu linalojitokeza katika kazi ya kifasihi. Anachosema ni kuwa maudhui ni masuala ya kimsingi yanayoonekana kudokezwa na msanii katika kazi ya kifasihi. Masuala haya yanaweza kufasiriwa kutokana na msuko, hadithi, mandhari, wahusika, taswira na ishara mbalimbali zinazotumika katika kazi hiyo. Kwa hivyo, maudhui yanaweza kuakisi mada ya mjadala katika matini ya kifasihi kwani huwa na mahusiano ya karibu nayo. Kwa mfano, maudhui mojawapo katika riwaya ya ***Utengano*** ni utengano wa kifamilia, maudhui ambayo yanaonekana kuwa na ukaribu na mada ya kazi hiyo.

Maudhui hukuzwa na vipengele vya fani. Vipengele hivi ni mtindo, mandhari, uhusika na wahusika, usimulizi na ploti. Wamitila (2003:190) anaelekea kuunga mkono hoja hii kwa kudai kuwa fani ni jumla ya mbinu, mtindo na nyenzo zinazotumiwa na mwandishi kuwasilisha dhamira na maudhui yake. Kwa maana hii hivyo basi, vipengele hivi ndivyo vinavyokuza maudhui na kuyadokeza kwa uwazi zaidi. Kwa mfano, katika riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke*** msuko, usimulizi na uhusika na wahusika vimejitokeza kuchangia pakubwa kukuza maudhui.

Kulingana na Meyer K.h.j. (uk:247) maudhui yamefungamana na vipengele vingine vya hadithi na kwa hivyo kuyabainisha kunahitaji uchunguzi wa makini wa vipengele hivyo. Uchunguzi wowote wa maudhui ni sharti utofautishe maudhui na mada ya hadithi. Sababu ni kuwa mada hutoa tu ishara kwa maudhui yanayojengwa wala haiwezi kuchukuliwa kuwa ndiyo maudhui. Kwa hivyo, linalohitajika ni kubainisha matukio muhimu yanayokuzwa na kufasiri ujumbe na ishara zinazoambatana nayo. Anaongeza kuwa uchunguzi wa kipengele cha maudhui utahitaji kutambua kama nguli au mkinzani wa kazi ya kifasihi anakuza ufahamu muhimu kutokana na tendo. Aidha, dhamira na malengo ya visa na vitushi katika kazi ya kifasihi yatasaidia kuyadokeza maudhui. Kwa mfano katika ***Nyuso za Mwanamke***, visa vingi vinavyojitokeza vimeambatana na sababu ya kutokea kwake na kwa hivyo vina uamilifu mkubwa katika ukuzaji wa maudhui. Kwa mfano, kisa cha Faisal kumsaka Bimkubwa kinatokea kwa sababu ya mapenzi aliyokuwa nayo kwake. Ni kutokana na sababu hii tunaona kuwa mapenzi ni maudhui mojawapo

katika kazi hii.

Maudhui mara nyingi huambatana na dhamira, itikadi, msimamo, maadili, mafunzo, tasnifu na falsafa. Kulingana na Wamitila (2008: 521) maudhui hujumlisha vipengele hivi. Huu ni ushahidi kuwa maudhui yana mafungamano ya kimaana na vipengele hivyo. Dhamira ni wazo kuu linalotawala kazi ya kifasihi kutoka mwanzo hadi mwisho. Hii ndiyo sababu hutokea pamoja na maudhui. Nayo falsafa ni mwelekeo wa kimawazo ambao unajitokeza katika matini. Hiki ndicho kipengele kinachojitokeza wakati kuna mwelekeo mkubwa wa kubainisha sababu ya kutendeka visa katika matini kama ilivyo katika riwaya ya kisaikolojia.[1] Kwa upande wake, itikadi ni muktadha wa kazi ya kifasihi. Muktadha huu unaweza kuwa wa kisiasa, kiuchumi, kijamii au wa kisaikolojia. Kutokana na maelezo haya vipengele hivi vina ukuruba wa karibu sana na maudhui kwa kiasi kikubwa na hujengwa sambamba na maudhui.

## 4.3 Maudhui katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*

Kama tulivyotaja katika sura ya kwanza, nadharia ya saikolojia changanuzi huiangalia kazi ya kifasihi kama ndoto ya mwandishi, wahusika wake kama watu anaowaona katika taswira ya fikira zake na maudhui kama masuala yanayotokea katika jamii yake. Kwa maana hii, uchunguzi wa maudhui kisaikolojia unayaangalia maudhui kama masuala anayoyashuhudia katika mazingira yake na yaliyohodhiwa katika ung'amuzibwete wake. Kwa upande mwingine kuyachanganua maudhui ni kuichanganua saikolojia ya mwandishi. Kwa hivyo, tunachanganua maudhui kama motifu zinazojirejelea katika *Nyuso za Mwanamke* na katika kazi zake za awali. Aidha, tunayaangalia maudhui kama akisi ya uhalisi wa maisha katika jamii iliyosawiriwa, kama anavyodai Eagleton K.h.j. kuhusu nadharia hii.

### 4.3.1 Utamaduni na itikadi

Kwa mujibu wa David Ministries Foundation (2002:729) utamaduni ni wazo, imani, desturi au mila zinazopokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa maoni yetu utamaduni huu hujitokeza katika jamii fulani mahsusi. Sababu ni kuwa utamaduni hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Aidha, ni muhimu tutaje kuwa utamaduni hujitokeza katika nyanja zote za maisha ya jamii kama vile nyanja ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na sayansi na teknolojia. Itikadi nayo ni imani inayojitokeza katika mfumo wa

kisiasa, kijamii na kiuchumi. Mara nyingi istilahi hii imeambatanishwa na dini kurejelea namna wanajamii wanavyoamini na kuhusiana na miungu yao.

Katika *Nyuso za Mwanamke,* utamaduni ni maudhui yanayojitokeza katika maisha ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Kisiasa utamaduni unajitokeza katika uongozi wa jamii husika. Katika jamii hii ni dhahiri kuwa wanawake hawana nafasi katika uongozi. Sababu ni kuwa hakutajwi popote ambapo mwanamke ni kiongozi. Kwa mfano, ni Bwana Hila na wenzake wanaotajwa kuwa viongozi wa serikali ilhali wake zake Bimkubwa na hata Bi. Siri hawatajwi popote kuwa viongozi (uk:29). Aidha, katika vita vya kuwania madaraka, ni baba yake Faisal na wanaume wengine ndio wanaotajwa (uk: 9). Kwa maana hii ni wazi kuwa huu ulikuwa utamaduni na imani yao kuwa wanawake wanafaa wawekwe pembeni katika masuala ya uongozi. Hii ni motifu inayojitokeza katika riwaya za Said Ahmed Mohamed. Kwa mfano, katika ***Babu Alipofufuka*** Proteus, K, Bw. Mbomba, Bw. Macho, Bw. Sungura, Bw. Kitambi na marafiki zao ndio wanaojitokeza kuwa viongozi wa nchi yao huku wanawake kama Bi. Zuhura Mapozi wakiwaburudisha. Hali hii inajitokeza pia katika ***Dunia Yao*** ambapo wahusika kama Ndi, Ye na Mustafa wanatajwa kuwa ndio waliokuwa katika uongozi wa jamii hiyo lakini hatajwi mwanamke yeyote kuwa kiongozi. Huu ni ushahidi tosha kuwa suala hili ni sehemu ya fikira za mwandishi huyu na ni hali halisi ya jamii hii ambayo haitambui uongozi wa wanawake.

Kijamii utamaduni unajidhihirisha katika dini, ndoa, malezi na masuala ya kijinsia. Kuhusu dini watu wa jamii hii wanaelekea ni Waislamu. Hata hivyo, ni Nana tu anayeonekana kushikilia kusali mara tano kama ilivyo desturi ya waislmu ilhali viongozi kama Bw. Hila walijihusisha na ufisadi na unyang'anyi kutosheleza uchu wao wa mali (uk:98 ). Kwa maana hii, suala la kushika na kuendeleza dini kwa uaminifu halijitokezi kwa sababu ya unafiki wa raia na viongozi waliogubikwa na uozo wa kimaadili kama vile uzinzi, unajisi, ujambazi, ufisadi, ubakaji na mauwaji. Jambo hili pia linajitokeza katika riwaya ya ***Utengano*** ambapo Maksudi ambaye ni Sheikh anashiriki ngono na Kazija pamoja na kumnyang'anya Farashuu urithi wake. Ulinganifu huu kama tulivyotaja hapo juu ni dhihirisho kuwa jamii hii bado inakumbwa na unafiki.

Suala la dini pia linajitokeza katika imani ya kusema na wafu. Suala hili linatokea hivyo kwa sababu katika imani za kijadi na hata za kiislamu watu huamini kuwa wafao hawapotei bali wanabadilishwa tu hali. Kwa sababu hii tunamshuhudia Nana akizungumza na mama yake kana kwamba yu hai ilhali tunajua amefariki. Aidha, itikadi hizi zinajitokeza pale ambapo kunatajwa imani ya Waswahili ya kuosha jimbo na kwamba mtu anapokuwa mgonjwa anafaa akae gizani eti kwa sababu mwangaza huwa sumu (uk:64-65). Jimbo ni dawa ya mitishamba ya kuwaogesha watoto wachanga ili wapate afya njema. Kutokea kwa masuala haya pamoja kunaonyesha kuwa imani za kijadi bado zina nguvu hata ingawa utamaduni mpya umeingia.

Utamaduni kijamii pia unajitokeza katika taasisi ya ndoa katika kazi hii. Ndoa ni taasisi muhimu iliyo na jukumu la kuendeleza kizazi. Katika jamii hii ndoa ndiyo inayoonekana kudhibitiwa na sheria na kaida za kitamaduni kuliko taasisi nyingine. Sheria hizi zinamdhibiti mwanamke kuliko mwanamume. Kwanza, mwanamke hana idhini ya kuchagua mchumba kwani hilo ni jukumu la wazazi, hasa baba yake. Kwa mfano, ingawa Bimkubwa alikuwa na rafiki aliyempenda alichaguliwa Bw. Hila na akalazimishwa kuolewa naye. Naye Nana alichumbiwa Dusa, kijana wa aila tajiri, na baba yake bila ya hiari yake (uk:44). Pili, pindi tu mwanamke anapoolewa hufungiwa ndani na kama si hivyo hudhibitiwa kwa sheria kali zinazomnyima uhuru na haki za kujiamulia kama binadamu. Kifungu kifuatacho kinaonyesha ukweli huu.

> ..bwana huyo alidhani tu …mwanamke ni pambo tu la nyumba kwa hivyo anachostahiki ni kupewa kila kitu alichokitaka isipokuwa kutoka nje ya nyumba' …. Kwa hili Bimkubwa aliudhika. Hakutaka kuuza uhuru wake wa kutoka na kuingia ndani, wa kwenda popote na kurudi wakati anaopenda. K.h.j. (uk: 287)

Hapa Bimkubwa anatudokezea namna alivyodhibitiwa katika ndoa yake na Bw.Hila. Kudhibitiwa huku pasi na kupewa uhuru kulimvuruga akili jambo lililovunja ndoa yao. Katika jamii hii ilikuwa desturi yao kutowaruhusu wanawake kutoka nje kwa dhana kwamba wangeharibika ilhali wanaume hawakufikiriwa hivyo. Kwa maana hii utamaduni huu ulimpendelea mwanamume na kumpa uhuru na haki ya kujichagulia. Hii pia ni motifu inayotokea katika riwaya za ***Babu Alipofufuka*** na ***Utengano*** katika wahusika Bi Kikuba na Bi. Tamima ambao walifungiwa ndani na kunyimwa uhuru wa kutoka nje na haki ya kufurahia ndoa zao na waume zao. Utokeaji huu kimotifu unaonyesha namna kulivyo na mwingilianomatini kimaudhui kati ya kazi hizi za Said Ahmed Mohamed

Zaidi ya hayo, utamaduni wa jamii hii ulikuwa na sheria za kumpendelea mwanamume katika suala la urithi. Sababu ni kuwa uliendeleza aila za kibaba. Hizi ni familia ambazo haki na majukumu ya wanaume yalitimizwa na kulindwa huku yale ya wanawake yakipuuza. Katika aila za aina hii wanaume ndio huwa na usemi mkubwa kuliko wanawake. Katika ***Nyuso za Mwanamke*** kumetajwa wanawake walionyimwa mirathi yao na wanaume kwa kuwa tu wao ni wanawake (uk:183). Mfano ni Bimkubwa ambaye alinyang'anywa watoto wake Nana na Suria bila kuachiwa rasilimali na waume wote aliowahi kuolewa nao (uk:287-290). Kunyang'anywa huku kulimfanya Bimkubwa aonekane kama tasa. Sababu hapa ni kuwa watoto walihesabiwa kuwa wa baba. Mfano mwingine ni wa akina Bi. Mau na Bi.Chuma ambao kama hawangesaidiwa na mkwe wao hawangekuwa na makazi yao. Utamaduni wa aina hii ni wa jamii nyingi katika Bara la Afrika na hukubaliwa na wanawake bila kuteta kwa kuhofia kukiuka kaida za kijamii. Athari ya kunyang'anywa urithi ni wanawake kuwa maskini na kukosa mahitaji ya kimsingi.

Jamii hii pia inao utamaduni wa kuwagawa raia wake kitabaka. Tabaka kwa mujibu wa kamusi ya TUKI (K.h.j. uk:388) ni kundi la watu wenye hali moja linalotokana na jamii yenye mfumo unaowagawa watu kulingana na uwezo wao wa kumiliki na kutawala njia za uzalishaji mali. Tabaka linahusiana pia na hali za kijamii na kisiasa za watu katika jamii kwa sababu umilki wa mali huenda sambamba na umiliki wa siasa za jamii na hali za kijamii za jamii husika. Kuna matabaka matatu makuu ambayo ni tabaka la juu, tabaka la kati na tabaka la chini. Katika ***Nyuso za Mwanamke*** kuna matabaka mawili makuu yanayojitokeza. Kunalo tabaka la juu na tabaka la chini. Tabaka la juu linawakilishwa na Bwana Hila, Dusa, marafiki zake na viongozi wa nchi (uk:31). Tabaka hili lina uwezo mkubwa wa kiuchumi na kisiasa. Uwezo huu unawawezesha kutawala tabaka la chini na kulinyanyasa. Unyanyasaji huu unajitokeza pale Bwana Hila anawanyang'anya majirani mashamba kwa ulaghai na kwa nguvu (uk:35-36). Kwa uwezo waliokuwa nao maskini hawakuwa na la kufanya kwani wao ndio waliokuwa na uwezo serikalini. Kwa sababu hii tabaka hili liliendelea kujilimbikizia mali kwa kuekeza mitaji serikalini na katika sekta ya kibinafsi kwa masharti nafuu na kutajirika huku tabaka la chini likikumbwa na umaskini, magonjwa, ukosefu wa maji, na kukaa katika mazingira machafu (uk:75, 95). Utamaduni wa kitabaka si jambo geni katika kazi za mwandishi

huyu na hata katika kazi za fasihi ya Kiswahili kwa ujumla. Kutokea huku katika kazi hii ni dhihirisho kuwa bado jamii inagawa watu kitabaka na tabaka la juu bado linanyanyasa tabaka la chini.

Utamaduni katika jamii hii ndio unaowapa msukumo mababe kama akina Bwana Hila kuwadhulumu na kuwanyima haki wanawake na kuwanyanyasa wanyonge. Kwa upande mwingine, utamaduni unazua hamaniko kwa wanawake kama Shemsa na Nana kutaka kujikomboa kutokana na nguvu zake ili wapate uhuru wa kujiamulia na usawa wa kijinsia. Kwa njia hii utamaduni ni chanzo kikuu cha msukumo wa hali za kisaikolojia za wahusika na unazua hamaniko kubwa kwao kutaka kujikomboa kutokana na minyororo yake ya kaida na sheria zinazowadhibiti.

### 4.3.2 Ukombozi wa mwanamke.

Ukombozi ni neno linalotokana na kitenzi komboa lenye maana ya hali ya kuokoa kutoka kwenye hali mbaya kama udhalimu au hali duni.[2] Hali mbaya inaweza kujumlisha mateso, utumwa, kubaguliwa, kupigwa, kutukanwa, kunyimwa uhuru au haki za kimsingi. Kwa maelezo hayo, ukombozi wa mwanamke unarejelea juhudi za kumtoa mwanamke katika hali mbaya ya kudhulumiwa au hali duni. Kama tulivyoona hapo juu tamaduni na itikadi nyingi zimechangia kudhulumiwa kwa wanawake ulimwenguni. Tamaduni hizi hutumia kaida na sheria zinazomnyima mwanamke uhuru na kumpendelea mwanamume. Kwa sababu hii mwanamume hutumia hali hii kumnyanyasa mwanamke kwa kuona ni halali kufanya hivyo kwani anaungwa mkono na mila na desturi za jamii yake. Wakati mwingine wanawake wenyewe huridhia hali hii kwa kutafuta fursa ya kujistarehesha.

Katika kazi hii wanawake wamesawiriwa kama wahusika waliodhulumiwa na kudunishwa. Kwa sababu hii wanahitaji ukombozi kutokana na hali hiyo. Kwanza, watoto wa kike wanadhulumiwa na wazazi wao. Kwa mfano, wanatengwa na mama zao na kwa hivyo wanakosa fursa ya kunyonya na kupata mapenzi ya mama zao. Nana ni mhusika aliyekosa malezi ya mama yake alipotalikiwa na baba yake. Tendo hili linakuwa sababu ya Nana kuteseka ndani kwa ndani katika ujana wake hali inayosababisha kukumbwa na shinikizo na kibuhuti. Tendo la aina hii pia lilitokea katika riwaya ya ***Utengano*** pale Bi. Tamima anatengwa na mtoto wake kwa kufukuzwa na Bw. Maksudi mara tu alipojifungua. Aidha, vijana

wanadhulumiwa na wazazi wao kwa kufungiwa ndani kama wafungwa. Kufungiwa huku kunawanyima fursa ya kutangamana na vijana wa rika lao. Ukosefu huu wa utangamano unawazuia kujifunza mengi hasa kuhusu uana suala ambalo linawafanya wakose ujuzi wa kukabiliana na matatizo mengi ya uana kama vile kuhusu ngono, magonjwa ya zinaa, uzazi na mapenzi. Kwa mfano, Nana alizuiwa kutoka na kukurubiana na vijana wengine ambao wanaitwa masimba hasa wavulana (uk: 38). Kuna wakati ambapo Nana anazuiwa kuimba wimbo na anapigwa kwa kumwalika Mpiga-gita (uk: 41-42 na 48). Ni dhahiri kuwa watoto wa kike wanahitaji kukombolewa kutokana na dhuluma zinazoendelezwa na jamii hii kwa sababu zinawaathiri kihasi na kuwafanya washindwe kujimudu ukubwani. Ukombozi huu unafaa uwape uhuru wa kutangamana na vijana wengine kwa lengo la kujifunza mengi kuhusu ujana wao. Aidha, wazazi wanafaa kuwafunza vijana kuhusu masuala ya uana ili waweze kuyamudu katika utu uzima.

Aidha, wanawake wanahitaji ukombozi kwa sababu katika jamii hii wanawake huchaguliwa wachumba wakati wa kuolewa na nyingi ya ndoa hizo ni za balaa tupu. Mfano wa wanawake waliochaguliwa waume ni kama Bimkubwa, Shemsa na Nana. Bimkubwa na Shemsa waliridhia na ukawa mwanzo wa shida katika maisha yao kwani ndoa hizo hazikudumu (uk:232, 204-208). Nana kwa upande wake, alipata afueni kwa kupinga uchaguzi wa baba yake kuolewa na Dusa na baadaye akajipatia mchumba aliyempenda (uk:44, 293). Nana amejitokeza kama mwanamke anayepigania haki zake tofauti na Bimkuwa na Shemsa. Linalodokezwa hapa ni kuwa wanawake wanafaa kujitokeza kupigania maslahi yao badala ya kujikalia tu na kungojea kuhurumiwa na wanaume. Vilevile, sheria na kaida za kitamaduni ambazo zinawanyima uhuru wa kupata haki za kimsingi zinafaa kutupiliwa mbali.

Ukombozi wa wanawake unahitajika kwa sababu hali yao kwa ujumla ni mbaya. Sababu ni kuwa jamii inapokumbwa na mikasa wao ndio wanaobeba mizigo ya kuwakimu watoto. Kauli ifuatayo inasadifu hali hii;

> Wengi nimewaona, wanawake…wanawake waliozeeka,walionyauka ngozi na mchuzi wa uhai. … wamo katika jahanamu ya jangwa na makundi yao ya mbuzi na kondoo wakihangaika kuwatafutia malisho… Au wakibeba mizigo ya majani na kuni kuipeleka nyumbani…wanapepesuka na mashungi yao

yaliyowazonga mwili mzima, wakiinua jembe, kuinama na kupasua aridhi ngumu ili kujaribu kuzalisha kitu kwenye *oasis* ... ( uk: 90-91)

Linalosemwa hapa ni kuwa wanawake wametwikwa mizigo mizito ya kulima, kuchunga ng'ombe na kulisha watoto. Mizigo hii ni mizito kwa namna hali ya kiuchumi na kimazingira inavyobadilika. Kwa hivyo, wanaume hawapaswi kuyatelekeza majukumu yao bali wanastahili kushirikiana na wanawake kama wenzi wao ili kupunguza uzito huu. Sababu ni kuwa wanawake wamechukua baadhi ya majukumu ambayo hata kijadi yalikuwa majukumu ya wanaume.

Kama tulivyotaja hapo juu wanawake katika ***Nyuso za Mwanamke*** wanadhulumiwa katika ndoa zao kwa kunyimwa uhuru na haki za kimsingi, kupigwa, kudhalilishwa na kufanywa watumwa na waume zao. Mambo haya hufanya ndoa kuwa jela kwa wanawake na kwa hivyo kuna haja ya kuwakomboa kutoka katika hali hii (uk:287-291). Ili kuwakomboa kutoka katika lindi hili la shida ni sharti wanawake waamue kupigania haki zao kama alivyoamua Shemsa kudai talaka alipoona kuwa ndoa yake ni utumwa mtupu (uk:211). Aidha, inafaa wanawake wazungumzie hali zinazowakumba hadharani ili jamii ielewe hali halisi wanayopitia. Katika kazi hii Nana kwa kuanzisha kipindi cha *Dukuduku* aliwapa wanawake jukwaa la kujieleza na kuarifu ulimwengu shida wanazopitia katika ndoa (uk:199-211). Mikakati ya wanawake kujikomboa ni suala ambalo linajitokeza dhahiri katika kazi hii kuliko linavyojitokeza katika riwaya za awali za Said Ahmed Mohamed. Kwa sababu tunawaona wanawake wenyewe wakichukua jukumu la kupigania haki zao tofauti na kazi za awali ambapo walingojea kuhurumiwa na wanaume.

Nana ameonyesha mikakati mahsusi ya namna mwanamke anaweza kujikomboa. Alikataa kuzugwa na wanaume na kujidhalilisha (uk:59 na 158). Kumzuga mtu ni kumfanya mtu afanye utakalo bila hiari ya kumudu akili yake. Kwa kukubali kuzugwa wanawake watatendewa lolote na wanaume pasi na wao kuinua kidole kwa lengo la kustareheshwa. Wanawake wengi wanapokumbwa na shida za kifedha wao huona njia ya rahisi ni kujiuza kingono ili wakidhi mahitaji yao bila kujua kuwa huko ni kujidhalilisha (uk:158). Hili ni jambo ambalo Nana alilipinga ingawa alikumbwa na matatizo ya kifedha alipotoroka nyumbani kwao.

Elimu ni suala lingine ambalo linaweza kuchangia ukombozi wa mwanamke. Elimu humpevusha mtu na kumfanya afahamu ulimwengu wake na masuala yaliyo na nguvu za kuwadhibiti wanadamu kama vile falsafa, itikadi, uchumi na siasa. Ufahamu huu ndio uliomsaidia Nana kuelewa masuala haya na hata kuwapiku wanaume kama vile Profesa PKA (uk:275- 282). Nana alitambua umuhimu wa baba yake kumpeleka shuleni na kumnunulia vitabu ingawa mwenyewe hakusoma (uk:119). Elimu pia ilimsaidia kukurubiana na wasomi kama vile Faisal na Devi ambao kutoka kwao alijifunza mengi. Ni kutokana na uhusiano huu na wao alipotunga azma ya kuanzisha kikundi cha taarab. Kwa hivyo, elimu imemsaidia Nana kwa kumweka katika nafasi nzuri ya kuelewa na kupigania haki zake.

Jambo linalolisisitizwa na Nana liwezalo kusaidia pakubwa kuwakomboa wanawake ni kuthubutu, yaani kujaribu. Wanawake wanaokumbwa na shida na hali duni hujikalia wakitarajia miujiza fulani itokee. Kutoka mwanzo Nana anaonyesha kuwa na azma ya kujikomboa kwa kuwa tayari kujaribu analoamini kama anavyosema mwenyewe kuwa;

> Mimi Nana. Mimi mwanamke. Binti. Kijana mwenye roho ya kimamboleo na tamaa ya kesho. Nimebaki ingawa katika kijisehemu kidogo kilichobaki. Nitakiimarisha. Kile kijisehemu changu kilichoachwa ndani ya ufu wangu. K.h.j. (uk: 61)

Ni dhahiri kutokana na kauli hii kuwa wanawake wakitaka kujikomboa kiuchumi, kisiasa na kijamii wanafaa wawe na azma madhubuti ya kujaribu kufanya wanaloamini pamoja na kuwa na malengo bainifu. Malengo haya yanafaa yaende na wakati na wajibidiishe katika shughuli zao ili wafanikiwe. Hivyo ndivyo alivyojiendeleza Nana kwa kujifunza muziki na kutafuta mtaji wa kuanzisha taarab bila kuwategemea wanaume. Kwa njia hii alikataa kujidhalilisha kwa wanaume ingawa Faisal angefurahi kumsaidia kama angemuuliza (uk:158). Hata hivyo, si vibaya kupata msaada kwa wanaume kama nia ya kufanya hivyo si mbaya.

Mwanamke anafaa akombolewe kutokana na vitendo viovu vya kunajisiwa na kubakwa na wanaume ambavyo vinaendelezwa na wanaume katika jamii hii. Mifano ya wanawake waliobakwa na kunajisiwa ni Bimkubwa, Hawa na Fatuma (uk:178-179 na 211). Katika mhusika Nana tunaona namna mwanamke

anaweza kujitayarisha dhidi ya dhuluma za aina hii na hata kuwalinda wengine dhidi ya dhuluma kama hizi. Nana alijifunza karate kutoka shuleni na hata alipotoroka nyumbani aliendelea nayo. Karate ingemsaidia kukabiliana na wanaume iwapo wangedhubutu kumbaka. Ujuzi huu ulisaidia kuwalinda akina Bi. Mau na Bi. Chuma dhidi ya manyanyaso ya Ngware wakati alitaka kumnyang'anya Bi. Mau kidani chake. Alimkabili kwa karate na akamtia adhabu hadi akalazwa hospitalini (uk: 275). Hali ya mwanamke kumtia mwanamume adhabu pia inajitokeza kwa njia ya kulipiza kisasi katika riwaya ya ***Utengano*** pale Kazija anawakutanisha mwana na baba yake katika chumba chake ili amwaibishe Maksudi na kumtia adhabu. Mfano huu unatuonyesha kuwa katika kazi za mwandishi huyu wanawake wanajaribu kuwakabili wanaume kwa dhuluma wanazofanyiwa. Hata hivyo mikakati wanayotumia ni ya kinyonge sana kuliko ule wa Nana wa kukabiliana na wanaume ana kwa ana. Namna hali hii inavyojitokeza ni dhihirisho kuwa riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke*** inaonyesha ukuaji mpevu kimaudhui katika suala hili kuliko katika kazi za awali za Said Ahmed Mohamed.

Wanawake pia wanaweza kujikomboa kwa kujilinda kimaadili. Katika kazi hii Nana alijizuia na jaribio la kuvutwa na pesa za wanaume ambazo kwake aliziona kama mtego hatari wa kuwanasa wanawake (uk:128). Aidha, alijilinda kimaadili kwa kukataa kwenda uchi kufurahisha wanaume (uk:222). Kuumbulika kimaadili ni njia moja ya kujidunisha na anayeumbuliwa hatakuwa na ujasiri wa kuwakabili mahasimu wake. Kwa njia hii alidumisha heshima yake katika jamii na kwa hivyo akawa katika nafasi nzuri ya kupigania haki zake na za wanawake wengine.

Wanawake wanafaa wasaidiane wao kwa wao ili wajikomboe. Mara nyingi wanawake hutarajia msaada kutoka kwa wanaume ambao pengine ni waume zao, rafiki zao au wahisani hata ingawa kunao wanawake wanaojimudu kati yao. Aidha, baadhi ya wanawake wameshuhudia wanawake wakidhulumiwa huku wakinyamaza kwa kuwaogopa wanaume. Mfano mzuri wa hali hii ni wa mama, nyanya na shangazi yake Shemsa ambao walishiriki katika kumshawishi kukubali kuolewa na Sadiki badala ya kumtetea hata baada ya kusema hakumtaka (uk:206, 208). Kushirikiana kwa wanawake kupinga dhuluma zinazoendelezwa dhidi yao kutasaidia kupunguza nguvu za sheria kali zilizopitwa na wakati wanazowekewa. Wanawake pia

wanaweza kusaidiana kifedha wao kwa wao. Jambo hili linadhihirika pale Nana alipofanikiwa aliwachukua akina Bi. Mau na Bi. Chuma na kuishi nao kwa kuwapa mahitaji yote.

Kihamasisho na msukumo wa suala la ukombozi wa wanawake ni dhuluma wanazofanyiwa wanawake na hali ya wanawake kunyimwa haki za kujiamulia na ukosefu wa usawa wa kijinsia. Hali hizi zimehimiliwa na kupewa msukumo na kaida na sheria za kitamaduni zinazompendelea mwanamume. Hali hizi ndizo zinazoibua hamaniko na kumsababishia mwanamke masaibu mengi katika jamii hii. Aidha, utandawazi na elimu ni masuala ambayo yamechangia pakubwa kuwapa wanawake hamu ya kutaka kupigania haki zao.

### 4.3.3 Mapenzi

Mapenzi huleta ukuruba wa karibu na utangamano kati ya binadamu. Kamusi ya TUKI (2004:222) inaieleza dhana hii kama hali ya kuingiwa moyoni na kuthamini mtu au kitu zaidi ya mwingine au kingine. Lililo dhahiri ni kuwa mapenzi ni hali ya kimawazo na kihisia inayoibuka ndani ya mtu kuonyesha upendo, huba au mahaba aliyo nayo kwa mtu au kitu. Kwa maoni yetu, mapenzi ni dhana ya kijumla inayorejelea hali ya kuenzi au kuwa na mahaba na mtu au kitu. Mahaba kama aina ya mapenzi ni mahusiano yanayohusisha uhusiano wa kingono ilhali kuenzi kunahusiana na kupendana kwa kawaida kati ya watu kutokana na kuthaminiana na kusaidiana.

Katika *Nyuso za Mwanamke* mapenzi yanajitokeza kuwili. Kunatajwa mapenzi ya roho na ya mwili (uk: 113). Mapenzi ya mwili ni mapenzi yenye mahaba na mapenzi ya roho ni yale ya kuthaminiana na kusaidiana. Kuna mapenzi kati ya wazazi na watoto na kati ya marafiki. Kwa upande mwingine, kuna mapenzi kati ya wapenzi walio katika mahaba. Mapenzi ambayo ni msingi na kihamasisho cha matukio mengi ni yale kati ya Bimkubwa na Faisal. Haya ni mapenzi yaliyojaa huba kati ya wawili hawa ambao kwa kuyakosa wanabadilika kitabia, kimawazo na kihisia. Mapenzi kati yao yalianza katika ujana wao na walikuwa na azma ya kuoana jambo ambalo halikutokea kwa sababu ya uamuzi wa wazazi wa Bimkubwa kumwoza kwa Bw. Hila (uk:232, 252). Mapenzi haya yalileta hamaniko kubwa kwa Faisal na kumfanya akose furaha na sababu ya maisha. Hali hii ndiyo inayomfanya aanze kumsaka Bimkubwa huku akiwa na mawazo chungu nzima kama inavyodhihirika katika kauli hii.

> … pamoja na hatari zote zilizomkumba hatarudi nyuma. Atavunja kuta. Atapiga teke hilo lango. Na liwe liwalo. Nia iko palepale. … Tamaa haijakatika, ingawa imebaki kama uzi wa hariri. Itabidi asonge mbele. K.h.j. (uk: 6)

Linalodhihirika ni kuwa Faisal ameazimia kumtafuta mpenzi wake hata akikumbwa na hatari za aina gani. Hali hii inaonyesha namna mapenzi juu ya Bimkubwa yanavyomtatiza kimawazo na kihisia. Kutatizika huku na kuwa na hamu ya kumpata ndiyo inayompa motisha ya kumsaka.

Mapenzi kati ya Bimkubwa na Faisal yalikuwa na athari kubwa kwa wawili hawa. Kwanza, yanamwathiri Faisal kwa kumtoa katika nchi yake na kumfanya aache kazi yake na familia yake. Tabia hii inamfanya aonekane kama mgonjwa wa akili (uk:15). Athari nyingine ya mapenzi haya ni kukumbwa na kibuhuti na shinikizo mara kwa mara. Hali hii ilimsababishia maumivu ya ndani kwa ndani (uk:154-155). Faisal pia alikumbwa na ndoto za mchana kutokana na hali hii na akawa mtu wa kuishi katika ndoto. Kuna wakati anaona taswira za Bimkubwa akiwa naye kama walivyokuwa wanakutana wakati wa ujana wao. Mapenzi pia yalimfanya ajigeuze na kuonekana kama mtu wa kawaida ilhali alikuwa mtu wa daraja la juu kama tulivyotaja hapo juu.

Kwa upande wake, Bimkubwa aliathirika na mapenzi haya kwa kukosa mashiko yoyote na mapenzi kwa wanaume wote aliowahi kuolewa kwao. Kwa sababu hii hakushabikia hata mmoja wao pamoja na kuwa ndoa zenyewe zilijaa mateso. Kutokana na hali hii, kama Faisal alipotesa hamu ya maisha. Hali yake ya mwisho inaweza kulinganishwa na ya mhusika Asumini katika ***Tata za Asumini*** ambaye kama Bimkubwa anakuwa mwendawazimu. Hali ya wahusika kuwa wendawazimu kama hatima ya kutatizika kisaikolojia ni motifu inayojitokeza katika kazi za Mohamed kama inavyoonekana pia katika ***Dunia Yao*** ambapo Ndi baada ya kutatizika sana kutokana na matatizo ya kiuchumi anakuwa mwendawazimu. Hali hii inayowakumba wahusika hawa katika kazi hizi ni ithibati kuwa matatizo ya kisaikolojia yanaongezeka katika jamii hii. Aghalabu, matatizo haya huongezeka katika jamii kwa kadiri maendeleo katika jamii yanavyokua na shida nyingi za kijamii, kisiasa na kiuchumi zinavyoibuka.

Mahaba pia yanajitokeza kati ya Nana na Amour. Mapenzi kati yao yanaweza kuelezwa kama ya kisumaku kwa sababu namna yanavyoibuka haieleweki bali kunatokea mvuto ambao hata Nana haelewi ulianza vipi. Hali hii ya kuvutiwa na Amour ilimfanya akumbwe na ndoto ambako kwenye ndoto hizo alijiona akifunzwa mapenzi na kijana huyu (uk:124). Ingawa suala la mapenzi kwa Nana lilikuwa limebanwa lilikuwa katika ung'amuzibwete wake kama mwenyewe anavyodai.

> Kupenda? Kupenda si ajabu. Ni maumbile ya mwanadamu. Kwa hivyo, siku yangu ya kupenda itafika. Nitapenda tokea chini ya nyayo zangu mpaka juu utosini pangu. K.h.j. (uk:42)

Ni wazi kuwa mapenzi yalikuwemo ndani ya nafsi yake na wakati ulipofika hakuweza kujizuia tena. Mapenzi ya Nana kwa Amour ndiyo yaliyobadilisha mkondo wa imani yake juu ya wanaume na kuanza kuwaona kama wenzi pakiwapo na mapenzi ya dhati. Hali hii ilimfanya akumbwe na mjadala wa ndani kwa ndani wa nafsi zake na kumfanya ajisahau hata anapokuwa akiendesha gari barabarani (uk:219-220). Huu ni ushahidi kuwa Nana ni mhusika aliyepagawa na mapenzi kiasi cha kuishi katika utohalisi. Amour naye alimchangamkia Nana lakini alimwona baba yake kuwa kizuizi kwake kumpata Nana kwa sababu hakumbanduka popote walipoenda. Hali hii ilimfanya awe wa kuibiaibia tu kumtazama Nana akiwa na baba yake. Juhudi moja aliyofanya ya kumtafuta na kuwa karibu na Nana ni kuhudhuria kipindi cha *Dukuduku* mara kwa mara. Ili kuonyesha udhati wa mapenzi haya walifunga ndoa na Nana (uk:299-300). Mapenzi kati ya wawili hawa yanaweza kusemwa kuwa akisi ya usasa kwa namna wanavyoonyesha uhuru mwingi wa kutangamana tofauti na ilivyozoeleka katika jamii hii.

Kunayo pia mapenzi kati ya wazazi na watoto. Kwa mfano, kuna mapenzi yaliyo dhahiri kati ya Nana na mama yake. Mapenzi kati yao yamejitokeza kama yasio ya kawaida. Mapenzi hunawiri wakati wa uhai wa watu lakini mhusika anapofariki mapenzi hayo hukatika kwa sababu aliyependwa hayupo. Nana anampenda mama yake na anazungumza na kumsikiliza kana kwamba yu hai ilhali tunajua amefariki. Hali hii inatokana na yeye kumkosa mama yake na kudhulumiwa alikoelekezewa. Bimkubwa naye alimpenda na kumkosa Nana kwa kuzuiwa kumwona na baba yake. Mapenzi haya yanadhihirika wakati anajinyima mahitaji ya kimsingi na kumwekea Nana pesa kwenye benki ambazo zilimsaidia kujikomboa kiuchumi.

Uhusiano wa Nana na mama yake unaonyesha kuwa jamii hii ina mashiko na imani za kishirikina ambazo zinadhihirika katika mawasiliano kati ya Nana na mzuka wa mama yake.

Mapenzi kati ya marafiki pia yanayojitokeza katika kazi hii. Mapenzi haya ni yasiyo ya kawaida kwa sababu yanatokea kati ya marafiki ambao tofauti zao za kiumri ni kubwa. Mapenzi haya yanatokea kati ya Faisal na Nana na Faisal na Suria. Katika mifano hii, mapenzi yanayojitokeza kati yao ni kama ya baba na binti (uk:308). Faisal anaonyesha mapenzi ya uaminifu, ushauri na ufadhili kwa wasichana hawa aliowaenzi. Mapenzi haya yananawiri kutokana na uhawilisho na uhusishi kati ya marafiki hawa.[3]

Mapenzi kama yanavyojitokeza katika kazi hii yanaonyesha athari ya usasa katika jamii hii. Kwa wahusika Bimkubwa na Faisal na Nana na Amour yanaelekea kukiuka desturi zilizozoeleka. Katika jamii hii mapenzi hayana nafasi katika shughuli ya kuchumbiana lakini kwa wahusika hawa ndoa haiwezi kufungwa kama wanaoana hawapendani. Mtazamo huu bila shaka unatokana na athari za kigeni hasa kupitia katika elimu tofauti na ilivyokuwa katika jamii hii.

### 4.3.4 Usasa

Usasa ni hali ya kukaribisha maendeleo na hali za kisasa na kuacha hali za kijadi. Usasa hutokana na kuiga mambo mageni ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiteknolojia yenye mwelekeo wa kimamboleo. Hali hii huwafanya binadamu wabadili tamaduni zao na kuonyesha hali ya kukengeuka kwa kudhihirisha desturi za kigeni. Usasa hutokana na utangamano kati ya watu wa asili mbalimbali. Utangamano huu hutokana na shughuli za kielimu, kisiasa, kibiashara na kidini zinazowaleta watu pamoja.

Katika kazi hii usasa unajitokeza katika hali mbalimbali. Kwanza, unajitokeza katika mapenzi. Mapenzi ni dhana ambayo haina nafasi kubwa katika jamii husika hasa kati ya mke na mume. Hata hivyo, kama tulivyotaja hapo juu, Faisal na Bimkubwa na Amour na Nana wanaonyesha mabadiliko makubwa kwa kudhihirisha kuwa uchumba hauwezi kuwepo bila ya mapenzi. Hii ndiyo sababu Nana alikataa kuchumbiwa na Dusa ambaye hakumpenda. Hata hivyo, walipochumbiana na Amour anafurahia tukio hilo kwa sababu ni kijana aliyempenda. Kwa upande wake, Faisal na Bimkubwa wanatuonyesha kuwa ndoa

isiyo na mapenzi ni chapwa kwa wao kushindwa kufurahia ndoa zao baada ya kuzuiliwa kuoana. Ndoa nyingi za wakati wao zilikuwa za kuvumiliwa tu na wanawake kwa sababu zilikosa mapenzi kwa wao kuchaguliwa wachumba na wazazi wao. Tabia wanaoionyesha ni ngeni sana katika jamii hii na wanajamii wanaiona kama ukiukaji wa desturi zao.

Usasa pia unajitokeza katika itikadi za uponyaji wa magonjwa. Bi. Mau na Bi.Chuma wanaamini kuwa mtu anapokuwa mgonjwa hahitaji mwangaza kwa sababu wanaamini kuwa mwangaza ni sumu. Pia, wanaamini kuwa mtoto azaliwapo anafaa aogoshwe jimbo ili awe na afya njema (uk:64-65). Jimbo kama tulivyotaja hapo juu ni dawa ya mitishamba ya kuwaogeshea watoto wachanga ili wapate afya njema. Hata hivyo, Bwana Hila anapinga imani hii kwani anaiona kama iliyopitwa na wakati. Yeye ni mwakilishi wa usasa ambaye anaona kuwa mtu anapokuwa mgonjwa anafaa kupelekwa hospitalini. Kwake giza haliwezi kuwa uponyaji kwa mgonjwa bali ni taashira ya uovu katika imani za kidini za kisasa. Jambo hili ndilo lililosababisha mashindano kati yake na Bimkubwa kuhusu Nana kuogeshwa jimbo. Linalodokezwa ni kuwa katika jamii ya kisasa imani za aina hii zinastahili kutupiliwa mbali.

Sherehe ni kiwakilishi kikubwa cha usasa. Sherehe mara nyingi huonyesha mabadiliko mbalimbali katika jamii. Sherehe zinazofanywa katika makazi ya Bwana Hila zinaakisi usasa katika jamii hii. Hizi ni sherehe za kuadhimisha siku ya kuzaliwa, kupandishwa cheo, ufanisi katika biashara na kwa kila tukio lililochukuliwa na familia hii kuwa la muhimu (uk:29-30). Sherehe hizi ni ushahidi wa tabaka la juu kama hatua za kustaarabika kwa kuegemea ustaarabu wa kigeni ambao si kawaida ya jamii hii. Sherehe za harusi zinazotokea katika kazi hii pia zinaonyesha usasa. Sherehe mojawapo ni ile inayotokea kati ya Amour na Nana. Katika sherehe hii kuna milolongo mirefu ya magari, fataki, fashifashi, muziki na kila aina ya mapambo na mbwembwe. Jambo lingine lisilo la kawaida ni kuwa mwimbaji katika arusi hii ni bibi arusi mwenyewe (uk:298-299). Kwa ujumla, sherehe hii inaakisi usasa kwa namna harusi hiyo ilivyofanywa kinyume na arusi nyingine zilivyofanywa.

Usawa wa kijinsia ni kitengo kingine ambapo tunaona usasa ukijitokeza katika kazi hii. Usawa wa kijinsia ni dhana inayorejelea hali ya wanawake na wanaume kuwa sawa kijamii, kiuchumi na kisiasa. Kwa maana

hii wanawake na wanaume watajiona wanaolingana katika masuala yote katika jamii bila kubagua jinsia yoyote. Usawa wa kijinsia unajitokeza katika mahusiano ya kimapenzi. Katika mahusiano haya Nana anaonyesha ujasiri wa kumwalika Amour ili wajadiliane kuhusu uhusiano wao na katika mkutano huu yeye ndiye anayeanzisha mazungumzo kuhusu mapenzi kati yao jambo lisilo la kawaida katika jamii hii (uk:264). Usawa wa kijinsia pia unajitokeza katika majukumu ya kijamii kama vile katika kazi za kinyumbani. Tangu jadi kazi hizi zimeachiwa wanawake. Hata hivyo, kuna wanaume wanaoona kuwa kupika, kuosha na kufagia ni kazi zinazoweza kufanywa na wao bila athari yoyote. Hawa ni Amour na Faisal ambao wanaweza kupika na kufanya kazi nyingine za nyumbani. Wanaonyesha kuwa wanawake ni kama wanaume na kwa hivyo hawapaswi kuachiwa kila kazi kwa kizingizio cha kitamaduni. Hata hivyo, suala hili linapaswa kukaribiwa kwa maelewano kati ya mwanamke na mwanamume ili utangamano wa kijamii uhifadhiwe.

Usasa una athari chanya kama ambavyo tumeona. Hata hivyo, usasa unaweza kuwa na athari hasi katika jamii. Jambo hili linajitokeza katika kauli ifuatayo;

> Alitambua kwamba 'usasa' (kwa maana mbovu kabisa) ni kasi kubwa sana inayokuja kuficha utulivu wa zamani wa mji huu mkongwe. Kwa hivyo upya wa mji ulimfuma kwa hofu kubwa sana. K.h.j. (uk: 8)

Ni wazi kutokana na kauli hii ya Faisal kuwa usasa huweza kuleta matokeo mabaya. Kwanza, kuna kuyaacha ya kale ambayo yanahitajika kusaidia jamii ya sasa kama maadili mema. Inapotendeka hivyo hujipenyeza tabia ngeni yenye athari hasi. Kwa mfano, kunatokea vijana ambao hawajali tena kuwaheshimu wazazi wao na kujali ujamaa. Vijana wa aina hii ndio wanaojiingiza katika matumizi ya madawa ya kulevya na wizi kama anavyojitokeza Ngware .

Yanayojitokeza katika sehemu hii yanadhihirisha kuwa jamii hii inafumbata maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwani inaakisi hali halisi za kijamii zilivyo ulimwenguni ambazo hubadilika kila kuchao kimaadili, kisiasa, kiteknolojia na kiuchumi. Hata hivyo, kuna mvutano kati ya usasa na ukale pale ambapo usasa unataka ubishwe na ukale nao ukale unateta (uk:64). Linalohitajika ni usasa na ukale kukamilishana ili yaliyo mazuri katika ukale yajumuishwe katika usasa kusudi kuwe na mshikamano wa vizazi vyote

viwili. Usawazishaji huu unajitokeza katika mhusika Nana ambaye anakaribisha usasa na wakati uo huo anaendeleza maadili ya kijadi ya kujidhibiti na kujiheshimu.

Ni muhimu kutaja kuwa utandawazi ni kihamasisho kikubwa cha usasa katika jamii hii. Utandawazi unaweza kuchukuliwa kama mfumo wa mahusiano ya kimataifa ambao umeufanya ulimwengu kuwa kama kijiji. Utandawazi katika jamii iliyosawiriwa umeiathiri kisiasa, kiuchumi, kijamii na kimaadili. Umefaulu kuleta athari hizi kutokana na walimwengu kutangamana katika nyanja mbalimbali za maisha. Kisiasa umebadilisha mfumo wa utawala kuakisi utawala wa nchi za kimagharibi. Mabadiliko haya yamefanya nchi za ulimwengu wa tatu kudhibitiwa kisiasa na kiuchumi na nchi zilizoendelea (uk:81, 214). Aidha, utandawazi umewawezesha wanajamii hawa kupata bidhaa za kisasa kama runinga, video na tarakilishi. Mbali na kuwa na athari za kiuchumi na za kisiasa, umeathiri wanajamii kimaadili kwa kuingiza tabia ngeni za kufanya sherehe, matumizi ya mihadarati na mahusiano ya kimapenzi na kindoa kama tulivyotaja hapo juu. Kwa ujumla utandawazi umekuwa na athari chanya na hasi katika kuleta mabadiliko ya kisasa, kiuchumi, kitamaduni na kisayansi na kiteknolojia katika jamii hii.

## 4.4 Hitimisho

Maudhui katika kazi hii yanafanana sana na maudhui mengi yanayojitokeza katika kazi nyingine za Said Ahmed Mohamed. Haya ni maudhui kama vile utamaduni na itikadi, ukombozi wa mwanamke, uozo wa kimaadili na utawala mbaya. Hata hivyo, kuna tofauti za wazi kwa namna baadhi ya maudhui yamekuzwa katika kazi hii. Kwa mfano, katika kazi hii wanawake wanaonyesha ujasiri mkubwa kupigania haki zao kwa kukabiliana na wanaume ana kwa ana kama anavyofanya Nana. Hali hii inaakisi mabadiliko yaliyotokea katika jamii nyingi ulimwenguni kuhusu masuala ibuka kama vile usawa wa kijinsia. Hili ni dhihirisho la upanuzi wa fasihi ya Kiswahili kuingiza masuala ibuka ambayo hayakuwepo katika kazi za awali. Kujirejelea kwa baadhi ya maudhui katika kazi hii yaliyo katika kazi za awali ni dhihirisho kuwa masuala haya ndiyo anayokumbana nayo mwandishi katika jamii yake na kwa hivyo ni sehemu ya ung'amuzibwete wake. Kwa hivyo, maudhui haya yamejitokeza kama motifu katika kazi hii na katika kazi za awali. Suala la usasa namna linavyojitokeza katika kazi hii ni kwa njia ya kipekee sana hasa katika

mapenzi, sherehe na ndoa ambapo kunaonekana kutokea mapinduzi makubwa kwa kukiuka kaida zilizozoeleka katika jamii hii. Mapinduzi haya ndiyo yanayoakisi jamii ya kisasa inayobadilika kutokana na athari za utandawazi uliofanya ulimwengu kuwa kama kijiji na kuongeza maingiliano kati ya watu kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiteknolojia. Usasa huu unaonyesha pia kuwa usanii huu umeathirika na mabadilko yanayotokea ulimwenguni na unataka kuihimiza jamii hii ibadilike kichanya ili isibaki nyuma.

Maudhui mengi yamejitokeza katika kazi hii. Baadhi ya maudhui yaliyokuzwa yanaakisi upanuzi wa riwaya ya Kiswahili kuhusisha masuala ibuka katika jamii. Masuala haya ni kama utandawazi, usasa, sayansi na teknolojia, haki za kibinadamu na usawa wa kijinsia. Upanuzi huu unaonyesha jinsi waandishi wa fasihi ya Kiswahili wanaunda kazi zao kusawiri hali halisi za kijamii, kisiasa, kisayansi na kiuchumi kama zilivyo fasihi nyingine duniani kama vile fasihi ya Ki-ulaya na za nchi nyingine za Kiafrika. Kukuzwa kwa maudhui kudokeza hali halisi katika jamii ni ushahidi wa saikolojia ya mwandishi kujitokeza.

## 4.5 Tanbihi

1 Kwa maelezo zaidi tazama Frye n. w , ***The Harper Hanbook of Literature*** (1985) New York: Harper Collins.

2 K.h.j. TUKI ***Kamusi ya Kiswahili Sanifu*** (2004). Nairobi: Oxford University Press.

3 K.h.j. Freud, S. ***On the History of the Psychoanalytic Movement, Papers on Metapsychology and Other Works*** (1916). London: Hogarth Press.

## SURA YA TANO

# MTINDO WA USANII WA *NYUSO ZA MWANAMKE*

## 5.1 Utangulizi

Katika sura hii tunajadili suala la mtindo wa usanii. Hizi ni mbinu mbalimbali ambazo kwazo msanii anaweza kulitokeza umbo la kisanii la matini yake ili kuwe na athari ya kiujumi katika kazi yake. Mtindo kama kipengele cha fani ni sehemu muhimu ya kazi ya kifasihi. Kwa ujumla mtindo unahusiana na namna msanii ametumia lugha kuiunda kazi yake ili iwe ya kusisimua na kuvutia. Kuhusu mtindo, tunajadili vipengele vyake ambavyo vina athari kubwa ya kisaikolojia. Baadhi ya vipengele tunavyovijadili ni pamoja na lugha ya kitamathali, uwasilishaji wa mawazo, sintaksia na matumizi ya italiki. Kuhusu lugha ya kitamathali tunachunguza mbinu kama ishara na uashiriaji, balagha katika usemaji, tasfida na miiko na ritifaa.

## 5.2 Dhana ya Mtindo

Dhana ya mtindo inahusiana na namna msanii wa kazi ya kifasihi anavyojieleza. Kwa mujibu wa Frye na wenzake (1985:447) mtindo unarejelea jinsi msanii anavyotumia lugha kujieleza. Analosema ni kuwa mtindo unahusiana na jinsi msanii anavyoiunda matini ya kifasihi kwa kutumia lugha kwa lengo la kubuni umbo la kisanii linalovutia. Kulingana na Holman (1976:320) mtindo una vitengo viwili, yaani jinsi wazo linavyodokezwa na ubinafsi wa mwandishi. Hivyo basi, mtindo hulenga kudhihirisha ubinafsi wa mwandishi, mawazo na lengo la fikira zake. Kwa maana hii mtindo unaweza kurejelewa kama mtu au usanii wa kazi hiyo. Kwa maana hiyo, tunaweza kuwa na mtindo-mtu na mtindo-usanii. Mtindo-mtu ni aina ya mtindo unaotumiwa na mwandishi fulani kumtofautisha na waandishi wengine wa kazi ya kifasihi. Kwa mfano, Wamitila (2003:145) anadai kuwa kazi za Mohamed Said Ahmed zina matumizi mapana ya jazanda na sitiari pamoja na unyumbufu wa kisintaksia tofauti na kazi za Adamu Shafi zilizo na lugha nyepesi na uchache wa tamathali. Kutokana na mifano hii tunaweza kuwatofautisha waandishi hawa kwa mitindo yao. Nao mtindo-usanii ni aina ya mtindo unaodhibitiwa na muktadha wa kazi yenyewe na hali zinazojitokeza katika kazi hiyo. Katika utafiti huu tunarejelea mtindo-usanii kwa kuiangalia kazi hii

kwa upekee wake ingawa tunaweza pia kurejelea mtindo wa kazi hii kama mtindo uliozoeleka kwa Said Mohamed hapa na pale.

Pamoja na hayo, mtindo kama wanavyoongeza akina Frye, unaweza kuakisi kipindi mahsusi cha wakati. Huu unaweza kuitwa mtindo kipindi kwa kule kurejelea kipindi mahsusi cha wakati wa kihistoria. Katika kipindi kama hicho huweza kuibuka mtindo wa namna kazi za kifasihi zinavyoandikwa. Kwa mfano, katika kipindi cha mwongo mmoja uliopita baadhi ya riwaya za Kiswahili zilizoandikwa zina mwelekeo mkubwa wa kutumia mbinu za mtindo wa riwaya mpya. Riwaya hizi zimetumia mbinu kama vile uzungumzinafsia, lugha ya kitamathali, sintaksia yenye nyufa, uhalisiajabu, italiki, uwasilishaji wa mawazo kisaikolojia na mbinu za kibalagha. Hizi ni riwaya kama vile ***Babu Alipofufuka, Bina-Adamu!, Musaleo!, Dunia Yao*** na ***Mafamba.*** Mtindo unaojitokeza katika kazi hizi unaakisi mtindo kipindi wa mwongo tuliotaja.

Mtindo ni kipengele cha fani kilicho muhimu sana katika kazi ya kifasihi. Kwanza, mtindo hutumiwa kukuza maudhui na dhamira katika fasihi. Mtindo hufanya hivi kwa kutumia mbinu zake kama usimulizi, lugha ya kitamathali na uwasilishaji wa mawazo. Kulingana na Njogu na Chimerah (1999:47) mtindo ni nyenzo kuu ya kusanifu kazi nzima. Maana ya hoja hii ni kuwa mtindo ndicho kipengele kinacholeta ujumi katika kazi ya kifasihi. Hali hii ndiyo inayoifanya matini kuwa ya kusisimua na kuvutia.

Uchunguzi wa mtindo hujikita kwenye mbinu za kujieleza kilugha ambazo mwandishi amezitumia katika kazi yake. Henderson na wenzake (1994:9) wanadai kuwa uchunguzi huu utajihusisha na uteuzi wa msamiati, muundo wa sentensi (sintaksia) na mbinu za kitamathali kama tashbihi, sitiari, taashira na ishara zinazobainisha toni na kudhihirisha ubinafsi wa mwandishi kama tulivyotaja hapo juu. Kwa maoni yetu hivi sio vipengele pekee vya kuchunguzwa katika mtindo. Kuna vipengele vingine kama uwasilishaji wa mawazo, usimulizi, mtazamo, uchimuzi, sauti na toni, lugha na itikadi na muwala na mshikamano.[1] Kwa upande wa mbinu za kitamathali kunazo mbinu nyingine kama matumizi ya maswali ya balagha, tasfida, usambamba, kinaya, dhihaka, chuku, tashtiti na takriri. Aidha, mtindo unaweza kuangaliwa kama nyenzo ya kuvijenga vipengele vya fani kama vile uhusika na wahusika na ploti. Kwa mfano, kuna mtindo wa kujenga ploti kwa kutumia mbinu rejeshi, mbinu elekezi, uzungumzinafsi ndani na mkondo wa ung'amuzi.

Kwa upande wake, mtindo wa usawiri wa wahusika unaweza kujumlisha usawiri wa wahusika kisaikolojia, kiishara, kisitiari pamoja na ukuzaji wa wahusika changamano au sahili. Kwa mujibu wa utafiti huu tunavichunguza vile vipengele vya mtindo ambavyo vina athari ya kisaikolojia katika matumizi yake. Hii ndiyo maana tumeamua kujadili uwasilishaji wa mawazo, sintaksia na lugha ya kitamathali kwa sababu mbinu hizi za mtindo zina mwelekeo mkubwa wa kisaikolojia na zimejitokeza vizuri katika riwaya hii. Aidha, katika utafiti wowote mtafiti hawezi kuyatafiti masuala yote kwani anadhibitiwa na muda uliowekwa. Mbinu za usimulizi hazitarejelewa hapa ingawa zina uamilifu wa kisaikolojia kwa sababu tumefafanua baadhi ya mbinu zake katika sura ya pili. Kwa upande wake, itikadi kama mwelekeo wa mawazo yanayojitokeza katika matini imejitokeza kama sehemu ya maudhui ingawa si kwa undani zaidi.

### 5.2.1 Sintaksia yenye nyufa

Sintaksia inarejelea muundo wa sentensi. Kwa mujibu wa utafiti wetu hatuliingilii suala la sintaksia kwa undani. Kwa sababu hiyo tuliangalia namna nukta na kistari vimetumika kuakisi sintaksia yenye nyufa. Kwa mujibu wa Frye (k.h.j. uk:446), riwaya ya kisaikolojia huonyesha mkurupuko wa fikira kupitia sintaksia yenye nyufa, sentensi zisizokamilika, dondoo, matumizi ya mistari, herufi kubwa, italiki, wino mzito na sentensi zisizoakifishwa. Mbinu hizi zina manufaa makubwa katika uakisi wa mawazo ya wahusika na athari kwa saikolojia ya msomaji.

Sintaksia yenye nyufa ni dhana ambayo tunaitumia kurejelea muundo wa sentensi ulio na mapengo. Mapengo haya yana nukta au kistari kifupi badala ya maneno ambayo yangekamilisha sentensi hizo. Kama tulivyotaja hapo juu matumizi ya nukta na kistari kifupi huonyesha mkurupuko wa mawazo ya wahusika. Yaani matumizi ya mbinu hizi huonyesha namna mawazo ya mwanadamu yalivyo katika ung'amuzibwete na yanapodokezwa vile yalivyo huacha mapengo ambayo yanafaa yajazwe kwa kuundwa upya ili yawe na mantiki. Uundaji huu mpya ndiyo dhana ya Freud ya masahihisho ya kiupili. Hivyo basi, matumizi ya nukta na kistari huonyesha uhalisi wa mawazo ya binadamu yalivyo na uchangamano wa mawazo yenyewe. Matumizi ya mbinu hizi yana athari kubwa kwa msomaji kwa kumfanya atafakari kinachosemwa ili apate maana inayokusudiwa kama inavyojitokeza katika usemi huu.

> "Nimeingia miezini…Nimeingia miezini! Baada ya miaka ishirini na moja nimezaliwa upya! … Nimezaliwa upya! … Nimezaliwa upya… Sasa nimeshakuwa mwanamke kamili … Nimeshakuwa mtu mzima!" K.h.j. (uk: 28)

Hapa Nana anaonyesha hisia za furaha kwa tukio la kuvunja ungo kiasi kwamba hawezi kueleza furaha yake kwa mtiririko. Kwa sababu hiyo kuna maneno ambayo yameachwa ili msomaji ajijazie. Kwa mfano, tunajiuliza amezaliwa upya vipi na amekuwa mwanamke kamili ili afanye nini. Kuna wakati mwingine ambapo mbinu hii hutumika hasa pale ambapo kuna maneno ambayo msemaji haruhusiwi kuyatamka hadharani kutokana na kaida za kijamii kama inavyodhihirika katika kauli hii hapa chini.

> "…. Alinifanya mtumishi tu wa kupikia familia yake kubwa, … Na si kupika tu, bali kufua, kupiga pasi, kufagia, kutandika na kutandua. Na labda hayo hayakuwa makubwa, sadiki alitaka… alitaka… aaaa, siwezi… siwezi kusema!" K.h.j. (uk:211)

Inaelekea tendo ambalo Sadiki alitaka kumtendea Shemsa lilikuwa mwiko kutajwa moja kwa moja. Kwa maoni yetu huenda alimtaka afanye ngono na rafiki zake. Kaida zinazowazuia watu kutaja mambo fulani zimehifadhiwa katika ung'amuzibwete wao na kwa hivyo inawawia vigumu kwao kuyataja hadharani kwa kuhofia kukiuka kaida hizo.

### 5.2.2 Italiki

Kwa mujibu wa Mathews (1997:189) italiki hutumika kuonyesha maneno na mifano ya dhana na maoni katika maandishi. Italiki huandikwa kwa mwandiko wa mlazo kuelekea kulia. Katika fasihi, kama anavyotaja Shaw (1972:208), italiki hutumiwa kutofautisha mawazo, maneno na dhana mbalimbali ili kuleta msisitizo kwa msomaji. Utiaji mkazo hufanywa ili msomaji ayape maandishi hayo uzingatifu unaohitajika. Kwa njia hii anaathiri uwazaji wa msomaji kwa kumfanya amakinike na kwa hivyo kuathiri saikolojia yake hasa utambuzi na uwezo wa akili yake. Kwa maana hii italiki inaweza kutumiwa katika uchanganuzi wa saikolojia ya msomaji.

Katika kazi hii italiki imetumika kurejelea maneno mapya na istilahi mpya. Aidha, italiki imetumika kuonyesha nyimbo, barua na maneno hasa yaliyotamkwa na wahusika. Italiki inapotumika kuonyesha maneno na istilahi mpya huyafanya yazingatiwe na msomaji na kwa njia hiyo kusisitiza kuwepo kwake na

ujumbe uliomo. Maneno yanayotokea katika vifungu vifuatavyo yanaonyesha hali hii;

Pasi na *kudhukuriwa.* (uk:6)

Nyota *zikahaha* na kucheza. (uk:54)

... kwa uso uliojaa machozi *nyekenyeke.* (uk:112)

... nilipopenya na kuzamia *umatemate* wa macho yake... (uk:113)

... ninapaswa kufafanua *vivuli-tatizi* vya maneno yake. K.h.j. (uk:116)

Maneno katika italiki yametumiwa kuleta msisitizo na nguvu mahsusi kwa msomaji. Ingawa ni maneno ya kawaida mwandishi ameyatumia kusisitiza ujumbe ili ujitokeze kwa nguvu kwa msomaji. Hii ni tofauti sana na jinsi mwandishi huyu anavyotumia italiki katika riwaya yake ya ***Babu Alipofufuka*** ambapo unaweza kupata aya nzima imeandikwa kwa italiki. Mtindo huu wa kuendeleza maneno umetumika katika kila sura katika kazi hii kama mtindo wa kuyaendeleza maneno haya kimdundo na kuleta msisitizo.

Italiki pia huakisi usemi mahsusi wa mhusika kama inavyojitokeza katika kauli hii ya Nana.

*Mimi nani? Natoka wapi? Nakwenda wapi? Nitakuwaje kesho? Hapa wapi nilipo? Nini maana ya baba au mama? Nini maana ya kwetu? Nini maana ya nchi yangu?* K.h.j. (uk:61-62)

Nana anajisaili katika mkondo wa kujitambua kutokana na masaibu yanayomkumba. Mbali na kuakisi yaliyosemwa na mhusika huyu, italiki na maswali ya balagha, yanamwelekeza msomaji katika tafakuri ya mhusika ili aweze kumtambua Nana na yale yanayomkumba. Ili kuonyesha yaliyosemwa hasa na wahusika mwandishi ametumia pia italiki katika barua za wahusika na nyimbo zao. Hali hii inajitokeza katika wimbo huu hapa chini.

*Nusu chupa kanilaze kitandani nisahau yaliyopita*
*Kanilaze niamke ningoje yanayokuja yatayoleta* K.h.j. (uk:100)

Huu ni wimbo wa mlevi mmoja ambaye Nana alimsikia akiimba siku moja. Ingawa umeimbwa na mlevi unadokeza ukweli kuwa jamii hii imekumbwa na matatizo mengi. Wanajamii wengi hasa wa kijiji cha akina Bi. Chuma hawana matumaini na kwa hivyo wanajizika katika ulevi ambao wanafikiria utawasaidia kusahau shida zao lakini si suluhisho. Kutamauka huku kumekuwa sehemu ya imani yao na mawazo yao.

### 5.2.3 Lugha ya kitamathali

Holman (1976:224) anaieleza lugha ya kitamathali kama lugha inayokiuka kaida za kawaida za kuunda, kupanga na kutumia lugha ili kuleta athari mpya na maana. Linalojitokeza ni kuwa lugha hii ni ukiushi wa kanuni zilizozoeleka katika kiwango cha maana na mpangilio wa maneno katika matumizi ya lugha. Kwa maoni yetu ukiushi huu huwa wa kimaksudi unaolenga kuleta maana mpya na kusisitiza ujumbe unaodokezwa. Mbali na tamathali kuleta maana mpya na kusisitiza ujumbe pia huzua picha anuwai katika fikira za msomaji ambazo huchangia uelewa wa kazi za kinathari na kuacha athari ya muda mrefu. Picha hizi zinazojitokeza kutokana na matumizi ya tamathali ni sehemu ya taswira zinazompitia msanii katika mawazo yake.

Katika kazi ya kifasihi lugha ya kitamathali kama kipengele cha mtindo hujitokeza katika matumizi ya tamathali za usemi kama sitiari, tashibihi, tashihisi, ukinzani, chuku, kinaya, dhihaka, ishara, metonimia, majazi kati ya nyingine. Wamitila (2008: 407) ameainisha tamathali za usemi katika makundi manne ambayo ni tamathali za kisentensi, tamathali za maneno, tamathali za kisauti na tamathali za kitafkira. Kwake yeye tamathali za kisentensi zinajumuisha mdokezo, maswali ya balagha na usambamaba huku tamathali za kitafkira zikijumuisha ritifaa, kijembe, dhihaka na tanakuzi. Nazo tamathali za kisauti zina tanakali za sauti, anafora, vikae na tauria huku tamathali za kimaneno zikiwa na chuku, tabaini na tasifida.[2] Uainishaji huu ni mzuri kwa vile umezingatia muundo wa tamathali na uamilifu wake. Hata hivyo kunayo haja ya kukaribisha uainishaji mwingine kama vile tamathali za kisaikolojia kama maswali ya balagha, ishara na taashira, tasfida na ritifaa.

#### 5.2.3.1 Tasifida na miko

Tasifida ni mbinu ya lugha ya kitamathali ambapo kuna matumizi ya usemi unaokubalika na kufurahisha badala ya ule mchafu, usiopendeza au usiofurahisha msikilizaji. Kwa mujibu wa Frye na wenzake (k.h.j.) tasifida huwa usemi usio wa moja kwa moja unaolenga kupunguza ukali wa usemi na wakati huo huo ukijiepusha na kutaja jambo kwa njia ya moja kwa moja. Yaani, tasifida husaidia kuzuia hali ya watu kuwa na haya au aibu wakati wa mazungumzo au katika maandishi. Kwa maoni yetu matumizi yake hivyo basi ni

mbinu ya masahihisho ya kiupili[3] kama anavyotaja Freud (1890) ambapo msanii huunda upya usemi kwa kuteua muundo na lugha inayokubalika na wasikilizaji au hadhira yake. Kwa njia hii msanii huepuka kukiuka kaida za kijamii zenye makatazo ya kutaja mambo machafu hadharani.

Miko ndiyo inayosababisha matumizi ya tasifida katika diskosi. Miko inaweza kuelezwa kama mambo ambayo mtu haruhusiwi kuyatenda au kuyatamka kutokana na makatazo ya kaida au desturi za kijamii. Kwa mujibu wa kamusi ya TUKI (2004:296) miko pia inaweza kuwepo kwa sababu ya imani au itikadi fulani wanazoshikilia wanajamii. Kwa mfano, katika jamii nyingi za Kiafrika kuna miko inayowazuia watu wa jinsia moja kujamiana, kutaja tendo hilo na la kwenda haja hadharani kati ya mengine. Ni kutokana na miko ya aina hii ndipo tasifida hubuniwa kukidhi mahitaji ya lugha ya wanajamii yenye heshima na ustaarabu katika jamii yao. Miko hii huwa katika ung'amuzi wa mzungumzaji na kila wakati hisia humwonya kutokuasi kaida hizo.

Tasifida hutumiwa kwa lengo la kuficha usiri, ubaya, uozo au uovu katika maongezi au maandishi ili kudumisha heshima inayokubalika na jamii fulani. Usiri kwa viwango vya kijamii unaweza kuwa mambo ya aibu kama kujamiana, sehemu nyeti au mambo ya kafara. Ubaya nao unaweza kuwa kutaja vitu vitishao kama nyoka kama ilivyo katika jamii ya Agikuyu huku uovu ni kama vile wizi, ulozi, urogi na kadhalika.

Katika *Nyuso za Mwanamke* tasifida imetumika sana kama inavyoonekana katika mifano tunayoorodhesha hapa chini.

| **Tasifida** | **Maana ya moja kwa moja** |
|---|---|
| ...uchafu umemtapakaa nyuma na mbele. (uk:24) | kutapakaa mavi na mkojo |
| ... nimeingia miezini. (uk:28) | kuwa na hedhi |
| ... tukamsikia kapiga mzinga.. (uk:70) | kutoa hewa au kujamba |
| ... kuibiwa sehemu muhimu... (uk:178) | kunajisiwa |
| ... ugonjwa huo mbaya. (uk:197) | ukimwi |
| ... kokochi za kifua... (uk:205) | matiti |
| ... bwana alipokula soro... (uk:236) | kufanya ngono |

Mifano hii inatuonyesha kuwa katika jamii iliyosawiriwa ilikuwa mwiko kutaja mambo kuhusu ngono,

kwenda haja, sehemu nyeti za mwili na baadhi ya magonjwa. Kwa sababu hiyo tasifida imetumiwa kurejelea masuala hayo. Kama anavyodai Mohamed (1995:126) dhana na matendo ya sirini hayapaswi kutajwa ovyoovyo. Kwa sababu hii hakutaka kuwakasirisha wasomaji wake katika jamii hiyo ili kazi yake isikataliwe.

### 5.2.3.2 Ishara na uashiriaji

Ishara ni kitu kinachosimamia kitu kingine kinachohusiana nacho. Kulingana na Frye na wenzake (k.h.j. uk: 451) ishara ni kiashirii na kile inachosimamia ni kiashiriwa. Kwa mfano, msalaba ni ishara ya Ukristo na rangi nyeusi kwa Wazungu ni ishara ya kuomboleza. Kwa maoni yao ishara huwakilisha kifikira hali ya kitu kinachoashiriwa. Maana inayojitokeza hapa ni kuwa uhusiano uliopo kati ya ishara na kiashiriwa ni wa kidhahania kwani ni wa kufikirika tu ingawa kunayo mahusiano kati yao. Kwa upande wake uashiriaji ni mbinu ya kuviwasilisha vitu au dhana kwa kutumia ishara. Kwa sababu hiyo maana za kiishara hupewa vitu, nyakati, tukio, dhana na mahusiano.

Katika matini za kifasihi ishara zina umuhimu mkubwa katika mchakato wa ujenzi wa kazi ya kifasihi. Kwanza, ishara hukuza maana iliyo zaidi ya maana ya kawaida na kwa njia hiyo kusaidia kukuza maana katika kazi hiyo. Ishara huwa dokezi kama kifaa cha kudokeza maana za ziada ili iweze kuibua fikira na hisia changamano bila maelezo marefu. Kwa njia hii ishara huakisi dhima ya itikisadi katika matumizi ya lugha na wakati huo huo ikidokeza maana mbalimbali kama tulivyotaja hapo juu. Uibuaji wa fikira na hisia huzifanya ishara ziwe na uamilifu wa kudokeza hali za kisaikolojia katika kazi za kinathari kama inavyojitokeza katika mfano huu.

> ...alimwona pugi juu ya mpendapendapo ambapo alianza kulia kwa sauti ya ajabu. Ilikuwa si sauti ya huzuni wala furaha. Sauti ya mkato tu- isiyotiwa chumvi wala sukari, sikwambii limau. ...mlio wa leo ... haukufanana na mlio wowote aliowahi kuusikia. K.h.j. (uk:246)

Mlio wa pugi usio wa kawaida ni ishara ya mabadiliko katika ulimwengu wa Faisal na ulimwengu kwa ujumla kama inavyodhihirika na uharibifu wa mazingira. Aidha, ni taashira ya hali ya Faisal kuendelea kutulia ingawa haiwezi kusemwa kuwa imeboreka.

Kulingana na Meyer (2002:220) maana za kiishara huwa zimejikita katika muundo wa hadithi na huwekwa pale kwa usanii mkubwa. Kwa njia hii maana hizi huchangia ujenzi wa maudhui yanayokuzwa kwani hurejelea muktadha wa hadithi hiyo. Katika ***Nyuso za Mwanamke*** mfano ufuatao unaweza kuakisi ukweli huu.

> Haraka kunguru dume na jike walikata hewa. Je, hao ni yeye na Bimkubwa katika mbio za kukimbiana na kutafutana? K.h.j. (uk:14)

Kunguru dume na jike ni ishara za Faisal na Bimkubwa. Kitendo cha kukimbiana ni tukio la Bimkubwa kumkimbia Faisal. Mfano huu umejikita vizuri katika msuko wa kazi hii kwa vile unaakisi juhudi za Faisal kumsaka Bimkubwa na wakati huo huo kuwa kijenzi kizuri cha maudhui ya mapenzi.

Katika matini za kifasihi ishara zinazojitokeza zinaweza kuwa za jamii husika au za kiubia kwa maana kwamba zinatumika kote ulimwenguni. Ishara za kiubia ni ishara zinazokubalika kimataifa. Kunayo mifano inayoweza kuchukuliwa kuwa za kiubia kama mfano huu.

> Je, kulikuwa na ishara njema kwangu zilizotoka kwenye uso wa maumbile? Baadaye madege ya pwani yalikuja kunizunguka mara saba. Yalinizunguka kwa kwenzi juu ya kichwa changu kama vile wakinizingua K.h.j. (uk:129)

Namba saba ni motifu inayojitokeza katika kazi nyingi za kifasihi hasa zenye mafungamano na Ukristo na Uislamu. Namba saba ni motifu ya kikale inayorejelea ukamilifu au kilele cha ufanisi. Kwa maana hii tendo la madege kumzunguka Nana mara saba ni ishara ya Nana kufikia kilele cha ufanisi katika maisha yake. Baada ya muda usiokuwa mrefu tunamwona Nana akifanikiwa kupata hundi aliyowekewa na mama yake iliyomsaidia kuanzisha biashara kubwa sana. Ishara hii imetumiwa kama utabiri wa kuboreka kwa maisha ya Nana baadaye. Ni dhihirisho la nguvu kama za kiungu katika maisha ya mhusika huyu za kuyaona mambo mema kwa mbali kabla hayajatokea.

Baadhi ya ishara zinaweza kuwa za kijadi kwa kuwa zina historia ndefu katika jamii husika na hujitokeza kama sehemu ya utamaduni wake. Ishara za aina hii pia zinajitokeza katika kazi hii. Katika mfano huu hapa chini kuna milio ya ndege na wanyama ambayo katika jamii za kijadi za Kiafrika huchukuliwa kuonyesha

kutokea kwa tukio baya au mkosi.

> Ilibidi hatimaye sikio la ndani lifumbuke aliposikia sauti ya bundi ikiritibua utulivu alioutaka uendelee... "Hoooood!" Bundi alilia. Tena zikafuata kwerezo za popo kama msumeno uliokata Chuma. "Kweeerrrch!" Baadaye mpazo wa sauti ya punda isiyoweza kuelezeka "Haaa-mb, haaa-mb." Tena ghafla, kipepo, vuuuu, kikajiingiza ndani pasi na kukaribishwa. Halafu kimya, kimya kilichonata ute mweusi wa usiku. K.h.j (uk:229)

Milio ya wanyama mara nyingi huwa ni ishara ya mkosi katika makazi ya mtu inaposikika katika jamii nyingi za Kiafrika. Milio hii kwa maoni yetu inahusiana pakubwa na mkosi wa kuchomwa kwa nyumba ya Nana kunakotokea wakati wa harusi. Aidha, utulivu unaoshuhudiwa baada ya milio hii ni ishara ya utulivu anaopata Nana katika maisha yake baada ya hamkani nyingi. Ishara hizi zinaonyesha kuwa ingawa Nana amestaarabika bado anaamini masuala ya ushirikina. Kwa maana hii itikadi za kijadi bado zina nafasi katika maisha yake na jamii iliyosawiriwa.

Kwa ujumla ishara katika kazi hii zina mchango mkubwa na zimetumiwa kurejelea vitu, dhana na watu. Kwa mfano, vipepeo na maua yametumiwa kurejelea dhana ya mapenzi huku mwangaza wa mshumaa umetumiwa kuakisi kunawiri kwa uhusiano kati ya Nana na Amour (uk:251,252 na 264). Wahusika pia wametumika kiishara. Kwa mfano, mhusika Nana amesawiriwa kama ishara ya ukombozi wa mwanamke kwa namna anavyoongoza juhudi za kujikomboa na kuwakomboa wanawake wengine. Mhusika Bimkubwa naye ni ishara ya udhalilishwaji wa wanawake wa upeo wa juu sana katika jamii hii kwa jinsi anavyokumbwa na mateso ya kila aina hadi akawa mwendawazimu na akajinyonga.

Ishara zozote zile huwa zimejulikana na watu wa jamii husika. Maana hapa ni kuwa ishara hizi huwa ni sehemu ya mambo yaliyohifadhiwa katika ung'amuzibwete wa binadamu na hujitokeza katika ung'amuzi wao kusawiri hali mbalimbali zinazojitokeza katika jamii. Kwa hivyo, mwandishi anapozitumia katika matini tayari anazo katika hifadhi yake na hujua maana yake. Hivyo basi, jinsi ishara hizi zimetumiwa zinaweza kuchanganua saikolojia ya mwandishi huyu kwa kuonyesha itikadi yake juu ya mapenzi, usasa, usawa wa kijnsia na dini.

#### 5.2.3.3 Ritifaa

Istilahi ritifaa ni ya asili ya neno la Kigiriki lenye maana ya "kwenda mbali."[4] Kama asili yake ilivyo hii ni tamathali ya usemi ambapo mwandishi au mzungumzaji huelekeza usemi wake kwa mtu wa kufikirika, kitu au sifa ya kidhahania au dhana. Mbatiah (2001:70) anaiona ritifaa kama mbinu ambapo mtunzi au mhusika anaongea na mtu au kitu kisichokuwepo ili kutoa hisia, fikira au mawazo yake kuhusu kitu hicho. Kitu hapa kinaweza kuwa kiumbe cha kuaminika tu kama malaika, Mungu, kizuu, mzuka au kitu chochote kisicho na uhai. Kwa mfano, mhusika katika kazi ya kifasihi anaweza kuzungumza na mlima au msitu kama anavyoongea na binadamu. Naye mtu anaweza kuongea na mtu ambaye hayuko kana kwamba mtu huyo yuko.

Ritifaa ni mbinu ya kitamathali ambayo ina mwelekeo mkubwa wa kisaikolojia na huweza kujitokeza kama uzungumzinafsi ndani. Kwa njia hii, ritifaa huweza kudokeza mawazo na hisia za kindani za mhusika. Mbinu hii hulenga kuibua hisia kwa msomaji na kwa njia hii kuwa na athari ya kisaikolojia kwa msomaji kama inavyojitokeza kama uzungumzi wa Nana hapa chini.

> Kumbuka tulivyotengwa na kudura ya mambo. Kumbuka tulivyopagazwa shehena ya miaka midhalilifu- na yote hayo kwa utoto na umama. Sijui kama unahisi maumivu nihisiyo mimi.Mimi niliyetimbwa na maumivu tokea utotoni nilipokuhitaji zaidi, ... K.h.j. (uk:19)

Nana anazungumza na mzuka wa mama yake kama yu hai. Katika uzungumzi huu tunaona namna Nana alivyo na hisia za upweke kwa kumkosa mama yake na shida ambazo zimemkumba na kumsababishia maumivu maishani. Kauli yake inaibua hisia za huzuni na huruma kwa msomaji. Mfano huu umejikita katika hadithi kuu na kwa hivyo unachangia katika ujenzi wa ploti kuu ya kazi hii. Mbali na hayo, kifungu hiki kama vingine kinautilia nguvu ujumbe mkuu wa kazi hii na kinatuonyesha vile mwanamke anateseka na kwa hivyo anahitaji ukombozi.

Kwa mujibu wa Wamitila (2008:406) mbinu hii inatokea pia pale mhusika fulani anasikiliza maneno yanayosemwa na mtu au kiumbe kisichoonekana. Katika hali kama hii mhusika huamini kuwa anayoyasikia ni ya kweli na huweza kuyatekeleza kana kwamba yamesemwa na mtu aliye hai. Hali hii inatokea katika ***Nyuso za Mwanamke*** wakati Nana anausikiliza mzuka wa mama yake na kufanya

anayoagizwa kama kuchukua kibegi kabatini, kusoma barua, kutandika mkeka na kuomba (uk:24-25). Nana anayafanya haya yote kwa kuamini kuwa mama yake yuko ingawa amefariki. Kuna wakati pia ambapo anasikiliza mzuka huu ukimsimulia maisha ya mama yake (uk:285-292). Hili ni dhihirisho kuwa Nana amegubikwa na mawazo kuhusu maisha ya mama yake ambayo yamekuwa sehemu ya ung'amuzibwete wake kiasi cha kuyaunda kuwa hadithi ya kuaminika na kusisimua. Kama tulivyotaja katika sura ya pili mawazo haya yanajitokeza kama ndoto za mchana. Nana anaathirika nayo na kwayo anatuathiri kama hadhira ya kazi hii.

### 5.4.4 Maswali ya balagha

Neno balagha ambalo ni *rhetoric* katika Kiingereza lina maana ya "kuzungumza au kusema." Kwa mujibu wa Wamitila (2003:27) balagha ni dhana inayoelezea sanaa ya usemaji na mbinu za uwasilishaji wa usemi kwa njia ya kushawishi na kuathiri msikilizaji. Kwa maana hiyo balagha ni ufundi wa kisanaa wa usemaji au uzungumzaji wenye lengo la kuwasilisha ujumbe kwa msikilizaji kwa njia ya kushawishi. Ushawishi huu unadhamiria kumfanya avutiwe na yanayosemwa ili asikilize. Kwa upande wake, maswali ya balagha ni mbinu ya kitamathali ambapo msemaji huuliza maswali ambayo hayahitaji kujibiwa kwa vile majibu yake yako dhahiri kwa msikilizaji. Kulingana na Holman (1976:452) mbinu hii hulenga kumshawishi msikilizaji kwa kumpa changamoto ya kuyapata majibu ili asiwe msikilizaji tuli bali awe mshirika wa mchakato wa mawasiliano. Kwa maoni yetu, hali hii humtia hamasa ya kuchangamkia anayoambiwa. Kwa mfano, Nana baada ya kuusikia wimbo wa Faisal kwa mara ya kwanza anatumia mbinu hii kusaili ujumbe na ishara zilizomo kwenye wimbo huo kama inavyojitokeza hapa chini.

> Yale maneno anayoyatamka na kuyapangizia mizani, ... lakini hayasemi waziwazi. Njia gani? Inaelekea wapi? Kani na kamiyo zipi? Za nini? Anazishusha nani? Namna gani yeye anaweza kuzipa kisogo? Anaweza au hawezi? Vilio? Analilia nini? Na nani? Kwa nini? Hisia gani zinazomkoroga? Kwa nini moyo wake umeshikwa na tego? Kwa nini anaungama kilio? Kwa nini njia imeziba ugo? Njia ya kwenda wapi? Kumfikia nani? K.h.j. (uk:41)

Maswali haya yanatupa changamoto ya kuurejelea wimbo ule tuuchungue tena ili tupate maana kamili. Aidha, maswali haya yanatuzindua kumakinika wakati tunaendelea kusoma kwa madhumuni ya kupata

ujumbe unaojitokeza katika matini pamoja na kutufanya washiriki wa mchakato wa usemi wake.

Pamoja na hayo, maswali ya balagha ni nyenzo ya kuyadokeza mawazo na hisia za wahusika. Kwa njia hii tunaweza kuingizwa katika mkondo wa uwazaji wa wahusika na wakati huo huo kuhisi wanavyohisi. Kwa njia hii tunaweza kuwahurumia na kuchukizwa na dhuluma zinazoendelezwa dhidi yao au tufurahie mafanikio yao. Hoja hii inajitokeza vizuri pale Nana anasaili sababu ya tabia ya baba yake ya kumdhibiti.

> Ilinishitusha sana kauli hiyo. Mimi sawasawa na mama yangu kwa vipi? Kwa utukutu wangu labda? Kwa kukataa na kususia kwangu? Kwa kutetea haki yangu? Kwa kuhalifu amri? K.h.j. (uk:44)

Maswali haya yamedhamiria kutufanya tuathirike na vitendo ambavyo Nana anafanyiwa na baba yake. Kutokana na kuathirika huko tunaweza kujiasa na kujirekebisha kama binadamu. Pamoja na hayo, kinalenga kutufanya tujitambulishe na Nana kama tunachukizwa na vitendo vya baba yake au tumbeze Nana kwa kumwona msichana mkaidi. Inaelekea mwandishi alikusudia tuchukue msimamo wa kuona namna Nana anavyokandamizwa na baba yake.

Wakati mwingine mbinu hii hutumiwa kusisitiza ujumbe unaojengwa pale mbinu hii imetumika. Maswali haya hufanya hivyo kwa kutumia kiulizi kimoja kiuradidi kuonyesha msisitizo huo. Kifungu kama hiki kinatilia mkazo wazo au ujumbe fulani unaodhamiriwa kumfikia msomaji.

> Pamoja na hayo, Faisal alijiuliza: 'Nini uhai? Nini uwananchi? Nini uraia? Nini kuwepo? Nini maana ya nafasi ndogo isiyo mwisho? Nini nafasi kubwa yenye upeo mdogo tu wa kujifaragua? K.h.j. (uk:150)

Maswali haya ya kibalagha yanasisitiza suala zima la maana ya maisha na nafasi ya mtu katika maisha hayo. Kwa kukosa maana ya maisha, ingawa Faisal alikuwa mkwasi, anatuzindua sisi kwa kutuweka katika mkondo wake wa mawazo ili tulichungue suala hili la ni nini maana ya maisha.

Kama anavyodai Katie (2001:407) maswali ya balagha yanaweza kutumiwa pia kama dalili ya kuwepo msimulizi maizi. Msimulizi maizi ni aina ya msimulizi anayejua kila kitu na ana uwezo wa kupenya hisia na mawazo ya wahusika kama inavyojitokeza katika mhusika Bimkubwa ambaye ni mzuka.

> "Kwa nini hutaki kunisikia? Kwa nini huambiziki? ... Unataka kuolewa, hujui ...kuolewa ni kudhibitiwa na mwanamume? ... wewe unamjua Faisal au huyo mwanawe? ... Enh, wewe unajua nini kuhusu wanaume? Unajua nini kuhusu ndoa... ngoja mimi nikuambie." K.h.j. (uk:286-287)

Mzuka wa Bimkubwa unaelekea kujua mipango yote ya Nana ya kutaka kuolewa na unamwonya kuhusu masaibu ya ndoa na wanaume. Mzuka unajua anayowaza na anavyohisi juu mapenzi na ndoa. Mfano huu unatuonyesha namna mbinu hii inaweza kupenya hisia, makusudio na mawazo ya wahusika kwa kutumia usimulizi maizi.

### 5.2.4 Uwasilishaji wa mawazo kisaikolojia katika *Nyuso za Mwanamke*

Uwasilishaji wa mawazo ni mbinu za kimtindo zinazotumiwa kuyadokeza mawazo ya wahusika katika matini za kifasihi. Kwa mujibu wa Leech na Short (2007:270) uwasilishaji wa mawazo hutuwezesha kujua mawazo ya wahusika na ya mwandishi kutegemea mbinu iliyotumiwa kuwasilisha mawazo hayo. Mbinu za uwasilishaji wa mawazo ni kama vile uwasilishaji halisi wa mawazo, uwasilishaji taarifa wa mawazo, uwasilishaji halisi huru wa mawazo, uwasilishaji taarifa huru wa mawazo na ripoti ya usimulizi wa tendo la mawazo. Kimsingi mbinu za uwasilishaji wa mawazo husaidia kudokeza madhumuni ya matendo ya wahusika, fikira na misimamo yao na wasifu wao. Kwa njia hii tunaweza kujua tajriba na ung'amuzi wa mawazo yao. Tunalosema hapa ni kuwa uwasilishaji wa mawazo husaidia kusawiri wahusika na kudokeza ujumbe unaokuzwa katika kazi ya kifasihi.

#### 5.2.4.1 Uwasilishaji halisi wa mawazo

Mbinu hii ya uwasilishaji wa mawazo hurejelea usemi uliotamkwa na mhusika bila kuufanyia mabadiliko. Katika mbinu hii alama za kunukuu hutumika na inaweza kuambatana na kitangulizi cha usemi huo. Kulingana na Leech na Short (k.h.j uk:271) kiambishi cha nafsi ya kwanza -ni- cha umoja au tu- cha wingi hutumika katika njeo iliopo. Mawazo yanayojitokeza katika mbinu hii ni ya mhusika na kwa njia hii tunaweza kubainisha anavyowaza na anavyohisi. Mbinu hii ndiyo nyenzo kuu ya dayolojia. Kwa maana hii matumizi yake hufanya kazi ya kinathari kuwa hai kwa kuleta drama katika nathari.

Katika kazi hii mbinu hii imetumika kwingi kuakisi mazungumzo kati ya wahusika mbalimbali. Mfano mzuri ni wa mazungumzo kati ya Amour na Nana.

> Nana aliibuka kutokana na kitambo cha fikira akaanza kumchokonoa Amour.
>
> "Nini msimamo wako kuhusu kuwa na mwenzako? Mwanamke nakusudia .."
>
> "Kuwa na mwenzi?" Amour pia aliyeibuka mawazoni, alijibu suala la Nana kwa suala…
>
> "Eeen, kuwa na mwenzi? Nauliza kuwa na mwenzi maana yake nini kwako?" Nana aliradidi swali.
>
> "Huu ni mtihani wa mapenzi au vipi?" Amour alikuwa akitabasamu. K.h.j. (uk:264)

Hapa tunaona kuwa Nana anaonyesha kuwa na uhuru wa kumsaili mwenzake kuhusu suala la mapenzi. Kutokana na maswali yake tunaona kuwa Nana anamtaka Amour kwa mapenzi. Kutokana na anayosema tunapata mawazo yao na hisia zao kuhusu suala la mapenzi na msukumo wa kukutana kwao.

### 5.2.4.2 Uwasilishaji taarifa wa mawazo

Mbinu hii hurejelea hali ambapo mhusika anaripoti tendo la usemi aliloshuhudia au aliloambiwa katika njeo iliyopita. Alama za kunukuu hazitumiki kama ilivyo katika uwasilishaji halisi wa mawazo. Kwa mujibu wa Toolan (1998:107) viambishi vya nafsi ya tatu ndivyo vinavyotumika. Mbinu hii huakisi usemi unaodokezwa na msimulizi wa nafsi ya tatu ambao huweza kufanywa na mwandishi wa kazi husika. Matumizi yake yanatusaidia kuelewa mtazamo na msimamo wa mwandishi kwa vile nafasi ya uwasilishaji wa mawazo huchukuliwa na mwandishi. Uwasilishaji wa taarifa ya mawazo ndiyo mbinu ya kijadi ya kuwasilisha mawazo katika nathari. Hii ndio mbinu ambayo inajitokeza katika kila sura katika kazi hii na imetumika kuelezea matukio, mandhari, wasifu na hisia za wahusika mbalimbali kama inavyojitokeza hapa chini.

> Bosi aliemewa alipomwona Nana anaingiliza kwa shoti. Mshangao ulipomshuka baada ya kuupima uzuri wake alimtafadhalisha aketi kitini mbele yake. Na hapo tena wakawa wanatazamana. Nana alimkagua meneja huyo na kumgundua kuwa ni mmoja wa wale ambao kila siku wanatazamiwa kupewa zawadi na kila anayeingia ofisini mwake kwa kile ambacho wao hudhani ni fursa waliyopewa…. K.h.j. (uk:163)

Mfano huu unatupa taswira ya jinsi Nana alivyoingia na wasifu wa meneja huyo na matarajio yake. Mbinu hii kama inavyojitokeza hapa inaweza kutumiwa kuyaeleza mambo kwa undani zaidi kuliko mbinu ya uwasilishaji halisi wa mawazo. Hata hivyo, mawazo na hisia halisi za mhusika hazijitokezi waziwazi kwa

vile tunayaona kwa jicho la msimulizi na wala si la mhusika mwenyewe. Pamoja na hayo, ni mtazamo na msimamo wa msimulizi unaojitokeza na wala si wa mhusika anayerejelewa.

### 5.2.4.3 Uwasilishaji halisi huru wa mawazo

Kwa mujibu wa Toolan (k.h.j. uk:109) uwasilishaji halisi huru wa mawazo ni mbinu ya uwasilishaji wa mawazo ambapo kuna mtiririko huru wa mawazo halisi ya mhusika bila ya alama za kunukuu. Kwa mujibu wa Leech na Short (k.h.j) mbinu hii inatofautiana na uwasilishaji halisi wa mawazo kwa vile haina kitangulizi cha taarifa. Hii ni mbinu inayokaribiana na mkondo wa ung'amuzi[5] ambapo pia kuna mtiririko huru wa mawazo. Kimsingi, inadhihirisha mawazo hai yanayompitikia mhusika yanayowasilishwa kama aina fulani ya usemi. Uwasilishaji huu una mwelekeo mkubwa wa kisaikolojia kwa vile unadhihirisha mawazo halisi yanayompitikia mhusika na huweza kudokeza hisia zake kwa ukamilifu. Aidha, matumizi ya mbinu hii katika kazi ya kifasihi yanaweza kusaidia kuonyesha fikira na msimamo wa mhusika fulani. Kutokana na mtiririko huo tunaweza kubainisha mambo yanayowatanza akilini mwao na katika maisha yao kwa ujumla.

Uwasilishaji halisi huru wa mawazo unajitokeza katika baadhi ya sura katika ***Nyuso za Mwanamke***. Kwa ujumla imetumiwa kuakisi hali za kisaikolojia za wahusika hasa kuonyesha jinsi walivyogubikwa na mawazo chungu nzima kuhusu mateso wanayopitia na hali zao za furaha na machukizo. Mbinu hii hasa inajitokeza katika wahusika wawili, Nana na Faisal.

> Lo, tazama! Hutaka kuifukuzilia mbali fikira ya kutokukuona, lakini sijui kwa nini mpaka dakika hii, nafsi yangu inakataa kuipeperusha fikra hiyo! Haitaki nafsi yangu kukubali kwamba hutajitokeza tena. Kwa sababu uliahidi utakuja. Utakuja ngozi, mwili na mifupa. Sijasahau. Nakumbuka kila kitu. K.h.j. (uk:20)

Haya ni mawazo hai yaliyo katika ung'amuzi wa Nana hasa kumhusu mama yake. Yanajitokeza kana kwamba Nana anazungumza na mama yake aliye hai.Yanaakisi hamu aliyo nayo ya kumwona mama yake ambaye hayuko tena. Kwa njia hii mbinu hii inaonyesha mawazo halisi ya mhusika huyu na kwa hivyo mtazamo unaojitokeza ni wa mhusika mwenyewe. Kutokana na kifungu hiki pia tunaweza kupata hisia za ndani za mhusika huyu pamoja na kuelewa kuwa anakumbwa na ndoto za mchana.

#### 5.2.4.4 Uwasilishaji taarifa huru wa mawazo

Kwa mujibu wa Leech na Short (k.h.j), hii ni mbinu ya kuwasilisha taarifa ya mawazo ya mhusika yanayowasilishwa na msimulizi wa nafsi ya tatu ambaye hamiliki tendo la usemi. Uwasilishaji huu hufanywa katika njeo iliyopita. Kwa njia hii mawazo ya mhusika anayezungumziwa huweza kujitokeza bila ya kuathirika na mtazamo wa msimulizi. Kule kutomiliki tendo la usemi hufanya mtazamo wa mawazo yale uwe wa mhusika huyo na bali si wa msimulizi kwani yeye hutumika tu kama nyenzo ya kupitisha mawazo. Mbinu hii pia inaweza kujitokeza kama muundo wa kuuliza swali na ndiyo maana wakati mwingine hujitokeza katika mbinu ya maswali ya balagha hasa kunapotumika usimulizi wa nafsi ya tatu. Mbinu hii inadhamiria kumfahamisha msomaji matukio na mawazo ya mhusika ili apate ujumbe ule unaokusudiwa katika usemi. Mfano wa matumizi yake ni kama huu;

> Yeye amekuwa akimwandama Bimkubwa karne nzima. Aaaa, eti mapenzi! Mapenzi gani? Labda ugonjwa. Au kutekwa akili pengine, kwani kutekwa akili nako si ugonjwa mdogo! Donge la tamaa na kukata tamaa na kisha kung'ang'ania tamaa tena. Unyamavu na kushitakia hali na unyamavu tena. Labda huko aliko Bimkubwa anajiona mwenyewe katika mnyumbuko wa maisha yake. K.h.j. (uk:15)

Haijulikani waziwazi anayemiliki usimulizi, kama ni Faisal ambaye anazungumziwa au msimulizi. Na huu ndio utata wa mbinu hii ya uwasilishaji wa mawazo ambapo msimulizi hamiliki usimulizi moja kwa moja. Hali hii inafanya mawazo yanayodokezwa hapa kuhusu hali ya Faisal kumsaka Bimkubwa kwa kunaswa na mapenzi yawe ya Faisal mwenyewe. Uhuru wa uwasilishaji huu pia unatuwezesha kubaini hisia alizo nazo Faisal juu ya Bimkubwa na kwa hivyo kutufanya tujitambulishe na hali zinazomkumba. Mbinu hii pia inaonyesha mwelekeo mkubwa wa kuyadokeza mawazo na hisia za wahusika kisaikolojia. Na kwa hivyo, msukumo wa matendo na tabia zao unaweza kubainika waziwazi.

#### 5.2.4.5 Ripoti ya usimulizi wa tendo la uwazaji

Kwa mujibu wa Katie (2001:266) mbinu hii hurejelea muhtasari wa mawazo ya mhusika fulani kama dhihirisho kuwa kumekuwepo na usemi wa mhusika huyo. Muhtasari huu wa mawazo huwasilishwa katika njeo iliyopita pamoja na matumizi ya viambishi vya nafsi ya tatu. Mbinu hii hutumika katika kazi za kinathari, hasa riwaya, kuonyesha kuwa mawasiliano au usemi umekuwepo lakini haukuwa na dondoti au

mawazo mengi. Anaongeza kuwa taarifa ya usimulizi wa tendo la mawazo inaweza kutumika kutuonyesha tajriba za kifikira za mhusika. Kwa sababu hii mbinu hii inayo uamilifu fulani wa kisaikolojia katika kazi za kifasihi hususani kuyadokeza mawazo na msimamo wa mhusika. Mwandishi anapotumia mbinu hii hulenga tuyaone mawazo, msimamo na tabia za mhusika kwa mtazamo wa mhusika mwenyewe. Kwa njia hiyo msimulizi huwa amejitenga na mawazo hayo lakini anabaki kama msimulizi wake. Hapa kuna mfano unaoakisi mbinu hii.

> Tulipompita Gandhi alituona… Akapiga kelele kutuasa twende polepole ili tufike salama. Tena akatuonya tuchunge amani tunakokwenda. K.h.j. (uk:85)

Hapa kunajitokeza muhtasari wa mawazo ya Gandhi kuhusu amani yanayodokezwa na msimulizi Nana. Ingawa Nana ndiye msimulizi tunayatambua mawazo hayo kama mawazo ya Gandhi kwa vile yanarejelea moja kwa moja yale yaliyonenwa na Gandhi mwenyewe. Ingawa mbinu hii inaweza kuyadokeza mawazo ya mhusika haifanyi hivyo kwa undani na mawazo yanayojitokeza hayaibui hisia kali kama mbinu nyingine za uwasilishaji wa mawazo.

## 5.3 Hitimisho

Katika sura hii tumejadili mtindo kama nyenzo ya kujieleza kilugha na kisanii. Kwa mujibu wa uchunguzi huu tumechunguza vipengele vinne muhimu vya mtindo ambavyo ni sintaksia, matumizi ya italiki, lugha ya kitamathali na uwasilishaji wa mawazo. Kuhusu sintaksia tumeona kuwa mbinu hii inachangia kumzindua msomaji ayape maandishi uzingatifu ufaao ili apate maana inayojitokeza katika sentensi. Mbinu hii pia imetumika kuonyesha mkurupuko wa mawazo ya wahusika na hali ya kukosa utulivu wa kimawazo. Italiki nayo imetumika kama mbinu ya kusisitiza maneno na vifungu fulani ili msomaji avipe uzingatifu zaidi. Lugha ya kitamathali imetumika pakubwa katika kazi hii. Hata hivyo, tumejadili tu mbinu chache ambazo kwetu tuliona zina uamilifu mkubwa wa kisaikolojia ambazo ni tasifida, ishara na uashiriaji, ritifaa na maswali ya balagha. Matumizi ya tasifida kwa kiwango kikubwa imedhibitiwa na kaida za kijamii na imetumika kudumisha heshima na kuficha mambo mabaya na ya aibu ambayo katika jamii iliyosawiriwa hayaruhusiwi kutajwa hadharani. Ishara nazo zimejitokeza kama nyenzo ya kukuza maudhui pamoja na usawiri wa wahusika. Kunao hata wahusika waliosawiriwa kiishara kama vile Nana na Bimkubwa. Kwa

upande wake, mbinu za uwasilishaji wa mawazo zimetumika kuyadokeza mawazo, hisia, matendo na mitazamo ya wahusika. Kwa ujumla mbinu hizi zimefaulu kusawiri hali za kisaikolojia za wahusika.

Kutokana na maelezo haya ni wazi kuwa mtindo umetumika kiufundi kudokeza hali za kisaikoljia za wahusika. Mbinu za kimtindo zinaonyesha ukuaji wa kimtindo katika riwaya ya kisaikolojia na riwaya ya Kiswahili kwa ujumla. Aidha, matumizi ya mbinu mbalimbali za kimtindo yanaakisi maendeleo makubwa ambayo yanatokea katika fasihi ya Kiswahili kuenda sambamba na fasihi nyingine za kilimwengu hasa fasihi ya Ki-ulaya.

## 5.4 Tanbihi

1. Kwa maelezo zaidi tazama Wamitila, K. W, ***Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*** (2008).

   Nairobi: Vide~Muwa. Uk:512-520.

2. K.h.j. uk:393-408

3. K.h.j. Freud , S. ***The Interpretation of Dreams*** (1900). London: Hogarth Press. Uk:489-492

4. K.h.j. http://en.wikipedia.org/wiki/apostrophe

5. K.h.j. http://en.wikipedia.org/wiki/psychological novel

# SURA YA SITA

## MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 6.1 Utangulizi

Katika sura hii tunatoa muhtasari wa matokeo ya utafiti wetu na mchango wetu ambao tunaona tumeudokeza kwa uwazi pamoja na mahitimisho yetu. Pamoja na hayo, tunathibitisha uhalali wa nadharia tete kwa kuonyesha kama zilifaa au zimetimizwa. Aidha, tunatoa mapendekezo kwa wasomi na watafiti wa siku za usoni kwa ujumla yanayoweza kuwasaidia kufanya utafiti zaidi.

### 6.2 Utathmini wa nadharia tete

Utafiti huu uliongozwa na nadharia tete tatu. Kwanza, uliongozwa na nadharia iliyodai kuwa riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* inaweza kuainishwa kama riwaya ya kisaikolojia. Kwa mujibu wa ugunduzi wetu, nadharia tete hii imetimizwa. Sababu ya kusema hivyo ni kuwa, ili riwaya itajwe kuwa ya kisaikolojia ni sharti iwe na sifa fulani dhahiri. Katika kazi hii, kama ilivyo katika riwaya za kisaikolojia, kunao wahusika waliosawiriwa kudokeza hali zao za ndani kama vile Nana, Faisal, Bi. Mau na Hawa. Wahusika hawa wanaonyesha hali za kutatizika ndani kwa ndani, kukumbwa na mfadhaiko, kibuhuti na mpagao. Aidha, ploti ya kazi hii imejengwa kwa mbinu zenye mwelekeo mkubwa wa kisaikolojia kama uzungumzinafsi ndani, mkondo wa ung'amuzi, ndoto na dayolojia ya ndani. Mbinu hizi zimetumiwa kwa lengo la kuonyesha uhusiano kati ya hali za kisaikolojia za wahusika na matendo yao. Kunayo matumizi mapana ya ishara, ritifaa, maswali ya balagha na tasifida kwa njia ya kudokeza mawazo, hisia na makusudio ya wahusika. Kunazo pia motifu za kimaudhui, kihusika, kiishara na kiploti kama usawiri wa mawazo na saikolojia ya mwandishi kwa ujumla. Kwa maana hii nadharia tete hii imetimia na kufaulu kwa kiasi kikubwa.

Pili, utafiti huu uliongozwa na nadharia tete iliyodai kuwa riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke*** inaonyesha ukamilifu katika kipengele cha umbuji wa wahusika kati ya vipengele vingine vya riwaya ya kisaikolojia. Katika uchunguzi wetu tulipata kuwa katika riwaya hii tofauti na ilivyo katika riwaya nyingine za kisaikolojia, kuna wahusika kadhaa waliosawiriwa kisaikolojia. Usawiri wao ni wa kipekee kwa sababu

karibu kila kipengele cha kimsingi cha kazi hii kina jukumu fulani katika usawiri huu wa wahusika. Kwa mfano, mbinu ambazo zimetumiwa kujenga ploti ya kazi hii zina mchango mkubwa katika usawiri wa wahusika kisaikolojia. Aidha, mbinu za usimulizi nafsia kama vile usimulizi wa nafsi ya kwanza na ya tatu zimetumiwa kwa upenyezi mkubwa kwa lengo hilo hilo. Kwa ujumla, vipengele vyote vya riwaya hii kikiwemo kipengele cha mtindo na maudhui ni vihamsisho vya ukuzaji na usawiri wa kisaikolojia wa wahusika. Hivyo basi, kama nadharia tete ya kwanza, hii pia imetimia na kufaulu vizuri kwa kuonyesha kuwa riwaya hii inaonyesha ukamilifu katika kipengele cha umbuji wa wahusika.

Mwisho, tuliongozwa na nadharia tete iliyodokeza kuwa mtindo si nyenzo kuu katika kuiunda kisanii riwaya ya ***Nyuso za Mwanamke*** kama riwaya ya kisaikolojia. Mtindo kama namna ya kujieleza kilugha na jinsi ya kuumba umbo la kisanii hujihusisha na umbuji wa wahusika, usukaji wa matukio, mbinu za usimulizi, uwasilishaji wa mawazo na lugha ya kitamathali miongoni mwa nyingine. Mbinu hizi za kimtindo na nyingine zimechangia pakubwa katika kuiunda kazi hii kisanii. Kwanza, kimtindo wahusika kama Nana na Bimkubwa wamesawiriwa kama ishara ya ukombozi na udhalilishwaji mtawalia. Pili, usukaji wa matukio umefanywa kwa mbinu za kimtindo kama vile mbinu rejeshi, mbinu elekezi na ndoto kudokeza masuala na matukio muhimu kwa njia isiyo ya kawaida. Tatu, lugha ya kitamathali kama vile tasifida imetumiwa kwa njia ya kukidhi matakwa ya kijamii kiufundi. Kwa hivyo, mtindo unajitokeza kama nyenzo kuu ya umbuji wa kazi hii kisanaa kwa maana kwamba nadharia tete tuliyopendekeza haikutimia. Kutokana na maelezo haya ni nadharia tete mbili tu zilizotimia kwa mujibu wa utafiti wetu.

## 6.3 Maoni kwa ujumla

Utafiti huu ulikuwa wa maktabani. Kwa maana hii tulifanya utafiti huu kwa kuzidurusu kazi za wataalamu mbalimbali pamoja na data yetu. Udurusu huu ulituwezesha kuwa na ufahamu na mwongozo wa kuichanganua data yetu ipasavyo. Ufahamu na mwongozo huo ulitusaidia kuchangua masuala tuliyokusudia kuyachanganua. Hata hivyo, kwa maoni yetu kama tungepata shajara za mwandishi husika na kuweza kuwahoji watu walio karibu na mwandishi tungeweza kubaini ufahamu zaidi wa masuala yanayomshughulisha sana na anayoamini na kushikilia. Ufahamu huu ungetusaidia kuchanganua saikolojia

yake ipasavyo ambayo ingetusaidia kuchanganua maudhui na wasifu wa wahusika kwa undani zaidi.

Utafiti wetu ulilenga kubainisha kwa uwazi mitagusano inayoibuka katika jamii husika na namna wahusika wanavyoathirika. Kutokana na uchunguzi wetu tumepata kuwa kuna mitagusano mingi inayojitokeza kama vile kati ya mke na mume, watoto na wazazi na wanawake na jamii. Mtigusano hii kwa kiasi kikubwa inawaathiri wanawake kuliko wanaume. Athari hii inawafanya wanawake wasawiriwe na nyuso mbalimbali kutokana na awamu za maisha yao zinazodhihirisha mateso, dhuluma na ukandamizaji wanaoelekezewa. Wanawake waliosawiriwa na nyuso za aina hii ni kama vile Bimkubwa, Shemsa, Mwanamkuu na Hawa. Hali hii inatokana na kaida, desturi, na mila za jamii hii ambazo bado zina nguvu na ndizo zinazotumiwa kuwakandamiza na kuwadhulumu wanawake. Jamii inafaa ibadili kwa namna inavyomtendea mwanamke ili imchukulie kama binadamu aliye na haki na uhuru kama alivyo mwanamume.

Aidha, tulilenga kubainisha mbinu za usukaji wa matukio muhimu kama matukio yenye mwelekeo wa kisaikolojia ili kuchunguza uhusiano uliopo kati ya hali za kisaikolojia za wahusika na matendo yao. Tumegundua kwamba mbinu nne muhimu zimefaulu sana kuonyesha usukaji wa matukio yenye mwelekeo wa kisaikolojia. Nazo ni uzungumzinafsi ndani, mkondo wa ung'amuzi, dayolojia ya ndani na ndoto. Mbinu hizi zimefaulu kuyadokeza matukio kama mapenzi kati ya Faisal na Nana, uhusiano kati ya Nana na baba yake, maisha ya ndoa ya Bimkubwa na kuchumbiana kwa Amour na Nana. Kupitia katika matukio ya aina hii mawazo, hisia na mitazamo ya wahusika imeweza kubainika.

Katika utafiti wetu tumegundua kuwa riwaya ya ***Nyuso za mwanamke*** ni riwaya ya kisasa ya kisaikolojia. Kwanza, mwandishi ameweka msisitizo mkubwa wa kazi hii kwenye uhusika wa ndani kama tulivyotaja hapo juu ambapo kunajitokeza wahusika wanaoumia ndani kwa ndani kama Faisal na Nana. Pili, kuna mbinu za kisaikolojia zilizotumiwa kujenga msuko wa kazi hii na mbinu za usimulizi nafsia zenye upenyezi wa mawazo na hisia za wahusika kama usimulizi wa nafsi ya kwanza na ya tatu. Tatu, kuna mbinu za kimtindo zilizotumiwa kwa lengo la kuathiri msomaji kimawazo na kihisia. Mbinu hizi ni kama lugha ya kitamathali, matumizi ya italiki, sintaksia yenye nyufa na uwasilishaji wa mawazo. Matumizi ya mbinu hizi mbali na kudokeza mawazo na hisia za wahusika zinamweka msomaji katika mkondo wa mawazo ya

wahusika na kumfanya awaze wanavyowaza na ahisi wanavyohisi. Kwa hivyo msomaji anaweza kuathirika na mchakato mzima wa uwasilishaji wa mawazo ya mwandishi. Kwa njia hii saikolojia ya msomaji inaweza kubainika. Nne, tumethibitisha kuwa riwaya hii ni ya kisaikolojia kwa kurejelea kazi za watalamu mbalimbali ambao walitafiti na kutoa ufafanuzi mbalimbali kuhusu riwaya ya kisaikolojia. Urejelezi huu ulitupa mwangaza uliotuwezesha kuimulika kazi hii kitalaamu kwa kusudi la kubainisha sifa za kimsingi zinazojitokeza katika riwaya hii kama ambavyo tumedokeza hapo juu.

Riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* ni upeo wa maendeleo ya riwaya ya kisaikolojia ya Kiswahili. Tuna sababu kadhaa za kusema hivyo. Kwanza, tofauti na riwaya nyingine za kisaikolojia, riwaya hii inao wahusika wengi waliosawiriwa kisaikolojia. Hawa ni wahusika kama Faisal, Nana, Bimkubwa, Mwanamkuu na Hawa. Kufaulu kwa mwandishi huyu kusawiri wahusika wengi kisaikolojia ni hatua mbele kwa sababu katika kazi za awali ilikuwa ni desturi kumtumia mhusika mmoja kuwakilisha jamii inayotatizika kisaikolojia. Usawiri huu wa wahusika wengi kisaikolojia unaenda sambamba na mabadiliko ya kijamii ambapo watu wengi wanakumbwa na matatizo ya kisaikolojia kutokana na kuongezeka kwa matatizo ya kijamii. Pili, usawiri wa wahusika wa kike wanaopigania haki zao kwa ari na msukumo ni ushahidi mwingine wa upeo wa juu wa maendeleo ya riwaya hii. Katika riwaya hii tunapata mhusika Nana ambaye anapigania haki zake bila ya kuhofia kaida za jamii zinazowadhibiti wanawake. Aidha, Shemsa anamtaliki Sadiki na baada ya hapo anadokeza madhila aliyopitia hadharani jambo ambalo wanawake wengi hawakufanya. Hii ni tofauti na riwaya za awali ambapo wanawake walijililia tu na kungojea kuhurumiwa. Nne, riwaya hii inaonyesha kilele cha utunzi wa riwaya ya kisaikolojia kwa kutumia karibu sifa zote za kimsingi za riwaya ya kisaikolojia. Hizi ni sifa kama uhusika wa ndani, usukaji wa matukio kisaikolojia na wahusika kuonyesha ubanaji, uhusishi, uhawilisho na ubadilishaji wa matakwa. Haya ndiyo masuala ya kimsingi yanayotokea katika riwaya ya kisaikolojia. Wahusika katika kazi hii ambao wameonyesha ubanaji, uhusishi, uhawilisho na ubadilishaji ni Nana, Faisal na Bimkubwa.

Uchunguzi huu, umeongozwa na nadharia ya saikolojia changanuzi. Hii ni nadharia inayoiona kazi ya kifasihi kama ndoto ya mwandishi na wahusika kama binadamu anaokumbana nao katika jamii yake na

wana athari katika maisha yake. Aidha, inaiona kazi ya kifasihi kama akisi ya uhalisi inayoonyesha tajriba ya binadamu, lengo la mwandishi na muundo wa fikira za ung'amuzibwete wake. Kwa mujibu wa nadharia hii ufasiri wa maana na ujumbe katika matini unafaa uhusishe ufasiri wa ishara mbalimbali zinazojitokeza katika kazi hiyo. Kutokana na uchunguzi wetu, nadharia hii imetufaa sana katika utafiti wetu. Sababu ni kuwa imetupa mwongozo mzuri wa kuchanganua usukaji wa matukio, usawiri wa wahusika na uchanganuzi wa mtindo. Saikolojia changanuzi imetusaidia kubainisha uwasilishaji wa mawazo na hisia za ndani za wahusika na msukukumo wa matukio ya wahusika. Aidha, imetusaidia kubainisha uhusiano uliopo kati ya uashiriaji wa mambo, taswira za kufikirika na hali halisi katika matini. Aidha, uchunguzi wa wahusika, saikolojia ya mwandishi, sifa za kiutanzu za riwaya ya kisaikolojia na saikolojia ya msomaji kwa mtazamo wa nadharia hii unaweza kusaidia kuchanganua utamaduni wa jamii husika. Utamaduni huu unaweza kubainika kutokana na kudokezwa mambo yaliyo katika ung'amuzibwete wa wahusika, misukumo ya matukio muhimu na kaida za kijamii zinazowadhibiti wahusika na kuwasababishia kuumia ndani kwa ndani. Haya ndiyo mambo yanayojitokeza katika kazi hii usawa wa kijinsia na ukombozi wa wanawake.

Ingawa nadharia hii inaweza kuchanganua maudhui kwa kuyaangalia kama motifu zinazojitokeza katika kazi ya kifasihi, inaelekea kuwa na upungufu katika kuyachanganua bila ya kuhusisha suala la mwingilianomatini. Pamoja na hayo, nadharia hii inawachukulia wahusika na mwandishi kama watu walioathirika kisaikolojia. Maana hapa ni kuwa msukumo wa matendo na mawazo yao ni athari ya hali zao za kimawazo na kihisia. Kwa mfano, wahusika Bimkubwa, Faisal na Nana ni wahusika walioathirika kisaikolojia na msukumo wa matendo yao ni mambo yaliyo katika ung'amuzibwete wao. Kwa hali hii tunawaona kama watu ambao hawaishi katika uhalisi jambo ambalo linaweza kuwafanya wasomaji waipuzilie mbali kazi ya mwandishi kuwa ni ndoto tu na wala haina mashiko na uhalisi. Mwisho, nadharia hii kuichukulia kazi ya kifasihi kama upeo wa juu wa ukiukaji wa kaida za kijamii kunawaweka waandishi katika hatari fulani hasa dhidi ya jamii zisizo na uhuru kamili wa kujieleza. Kwa njia hii, mifumo ya utawala inaweza kuanza kuwaangalia kwa jicho la kuwadhibiti na kwa hivyo kukwamiza kazi ya uandishi

## 6.4 Mapendekezo

Utafiti wa saikolojia changanuzi unaweza kufanywa kwa kuzichunguza shajara za mwandishi pamoja na kuwahoji watu walio karibu naye. Kwa njia hii saikolojia ya mwandishi inaweza kujitokeza vizuri. Kwa maana hiyo, kuna haja ya kufanya hivyo katika tafiti nyingine kwa mtazamo huu katika kiwango cha uzamili. Uchunguzi kama huu utasaidia kuchanganua saikolojia ya mwandishi kwa undani zaidi.

Riwaya ya kisaikolojia ya Kiswahili ina mafungamano ya kiutanzu, kimtindo na kiistilahi na riwaya ya kisaikolojia ya Ki-ulaya. Kwa sababu hii riwaya ya Kiswahili imekopa mengi kutokana na riwaya ya Ki-ulaya. Kwa maana hii ipo haja ya kuchunguza mafungamano na mahusiano haya kati ya riwaya ya Kiswahili na riwaya ya Ki-ulaya kitaalamu kwa kutumia nadharia ya saikolojia changanuzi. Utafiti wa aina hii unaweza kusaidia kuonyesha namna ambavyo kuna mwingiliano wa kimatini na athari ambayo riwaya ya Ki-ulaya inayo kwa riwaya ya Kiswahili. Kwa sababu utafiti wa aina hii unahitaji muda na unaweza kuwa mrefu, unafaa ufanywe katika kiwango cha uzamifu.

Suala la mwingilianomatini kama kitengo cha kimtindo katika riwaya za kisaikolojia linaweza kuwa la kusisimua sana. Maana ya kusema hivyo ni kuwa riwaya za kisaikolojia tulizozirejelea zilionyesha mwingilianomatini kwa kiwango kikubwa. Hizi ni riwaya kama ***Tata za Asumini, Babu Alipofufuka, Bina-Adamu!, Dunia Yao*** na ***Nyuso za Mwanamke.*** Uchunguzi wa aina hii unaweza kulinganisha na kulinganua suala hili ili kuonyesha namna zinavyolingana na kutofautiana kimtindo, kihusika, kimsuko na kimaudhui kwa kutumia nadharia ya saikolojia changanuzi. Utafiti huu unaweza kufanywa katika kiwango cha uzamili au wa uzamifu kutegemea uzito wa masuala ya utafiti yaliyochaguliwa kutafitiwa.

Suala la uchanganuzi wa uhusika na wahusika kisaikolojia na motifu au vikale ni masuala ambayo yamerejelewa sana. Hii ina maana kwamba masuala kama vile mtindo na wasifu wa ploti kwa mtazamo huu hayajapewa nafasi kubwa kwa kadiri tunavyojua. Uchanganuzi wa masuala haya utaweza kuipa riwaya ya kisaikolojia mmuliko mpya ambao haujashughulikiwa na kwa hivyo kuifanya ieleweke zaidi. Utafiti huu unaweza kufanywa kwa mtazamo tuliotumia katika kiwango cha uzamili.

## 6.5 Sherehe

**Dayolojia ya ndani:** mawasiliano ya ndani kwa ndani kati ya nafsi za mhusika au kati ya nafsi yake na kiumbe kisichoonekana ambapo kuna majibizano.

**Dhana ya Edipode:** dhana inayotokana na kisasili cha kiyunani ambapo mtoto wa kiume hubishana na baba kuwa karibu na mama.

**Dhana ya Elektrika:** dhana inayotokana na kisasili cha kiyunani ambapo mtoto wa kike hushindana na mama kuwa karibu na baba.

**Kaida:** sheria au desturi za kitamaduni za jamii fulani.

**Kibuhuti** (pressure)**:** mshtuko au bumbuazi anayokuwa nayo mtu kutokana na fikira au mawazo ya huzuni.

**Vikale:** vipengele vya kifani au kimaana vinavyotawala kazi ya kifasihi ambavyo ni sehemu ya utamaduni wa jamii kama vile matambiko, sherehe, nyimbo na historia.

**Masahihisho ya kiupili**(secondary revision)**:** hali ya kuunda upya mawazo au fikira za ung'amuzibwete au ndoto ili ziwe na mantiki.

**Mfadhaiko**(hsyteria)**:** wasiwasi mkubwa unaoambatana na kuchanganyikiwa kimawazo.

**Mkinzani:** mhusika katika kazi ya kifasihi anayepinga harakati nzuri za nguli au shujaa wa kazi ya kifasihi.

**Mkondo wa ung'amuzi**: mtiririko huru wa mawazo yasiosemwa yanayompitikia mhusika hasa katika kazi za kinathari.

**Motifu:** elementi ya kimuundo au kimaudhui inayotawala kazi ya kifasihi.

**Mwananyurolojia:** mtalaamu wa kutibu wagonjwa wa matatizo ya kisaikolojia.

**Mzuka:** kiumbe cha kipepo au kizimwi kinachohusiana na mtu aliyefariki kinachoaminika kuwa na uwezo wa kusema na mtu aliye hai.

**Nguli:** Mhusika mkuu katika kazi ya kifasihi anayewasilisha na kuwakilisha maadili na msimamo wa jamii fulani.

**Saikolojia changanuzi:** nadharia ya uhakiki wa kazi ya kifasihi inayoiangalia matini kama ndoto na hulka ya mwandishi na hutumia ujuzi wa kisaikolojia kuchanganua saikolojia ya mwandishi, msomaji na wahusika.

**Tamathali:** istilahi inayorejelea ishara zinazohusu hali ya kike au kiume katika saikoljia changanuzi.

**Ubanaji**(suppression)**:** hali ya mhusika aliye na matatizo ya kisaikolojia kuzuia au kuzuiwa kimakusudi

kufikiria au kuzungumzia mambo, matendo au kumbukizi za hali zinazomkumba.

**Ubadilishaji**(substitution)**:** hali ya ugeuzaji wa matamanio ya mhusika yaliyobanwa kabisa kwa mambo mengine au hali nyingine.

**Udenguzi**: mbinu ya kihakiki inayotilia mkazo lugha ya kifasihi na huangalia viashirii vya kazi ya kifasihi kama vilivyo huru.

**Udidimivu** (regression)**:** hali ya mhusika wa nyurolojia kurejelea hali za utotoni.

**Uhawilisho** (transfer): Hali ya mhusika aliye na matatizo ya kisaikolojia kuhamishia kwingine lawama ya hali inayomkumba kwa lengo la kuzuia aibu.

**Uhusishaji** (association)**:** hali ya mhusika kuhamishia matamanio yake kwa hali, mtu au kitu ambacho kinafanana na kile kilichobanwa.

**Ung'amuzi:** sehemu ya fikira za binadamu iliyo na mawazo na mambo ambayo tunayafahamu.

**Ung'amuzibwete**: sehemu ya fikira za binadamu inayohodhi mawazo, hofu na mitazamo hasi isiyokubalika na jamii inayojitokeza kama ndoto.

**Upinzani** (resistance)**:** hali ya mhusika wa matatizo ya kisaikolojia kutotaka kufichua hali inayomkabili ili uvumbuzi upatikane.

**Uzungumzinafsi ndani**: mazungumzo ya ndani kwa ndani ya upande mmoja kati ya nafsi za mhusika na kiumbe asiyeonekana.

## 6.6 Marejeleo


Baldic, C. (2001) ***Oxford Concise Dictionary of Literary Terms.*** Oxford: Oxford University Press.

Berger, M. (1977) ***Real and Imagined Worlds: The Novel and Social Science***. Cambridge: Havard University Press.

Bloom, H. (1997) ***"Poetry, Revisionism and Reppression,"*** in Twenth-Century Literary Theory, Newton, K.W. (mh.) uk:148-152. Pelgrave: Macmillan.

David Ministries Foundation (2002) ***The Complete Christian Dictionary: for Home Use, School and Office.*** Geneva: Oasis International Ltd.

Diyanni, R. (1998) ***Literature: Reading Fiction, Poetry and Essay***. (tol. 4.) Boston : MacGraw Hill.

Dorsch, T.S (1965) mh. ***Classical Literary Criticism***. New York: Penguin

Eagleton, T. (1996) ***Literary Theory: An Introduction***. Malden: Blackwell.

Freud, S. (1899) ***Pre-Psychoanalytic Publications and Unpublished Works.*** London: Hogarth Press.

...........(1900) ***The Interpretation of Dreams.*** London: Hogarth Press.

...........(1910) ***Five Lectures on Psychoanalysis, Leonardo da Vinci and Other Works.*** London: Hogarth Press.

...........(1916) ***On the History of Pychoanalytic Movement, Papers on Metapsychology and Other Works.*** London: Hogarth Press.

...........(1961) ***The Ego and the Id and Other Works.*** London: Hogarth Press.

Frye, N., Baker, S. na Perkins, G. (1985) ***The Harper Handbook of Literature***. New York: The Harper Collins.

Henderson, G., Day, W. na Waller, S. (1994) ***Literature and Ourselves.*** New York: Harper Collins College Publishers.

Holland, N.N (1997) ' ***Reading and Identity: A psychoanalytic Revolution'*** in Twentieth Century Literary Theory. Newton, K.W (mh.) Palgrave: Macmillan

Holman, C.H. (1976) ***A Handbook of Literature***. Indianapolis: The Odyssey Press

Katie, W. (2001) ***A Dictionary of Stylistics.*** London : Longman.

Kennedy, X.J. na Gioia, D. (2005) ***Literature: An Introduction to Fiction, Poetry and Drama***. New York: Longman.

Lacan, J. (1977) ***"The Function and Field of Speech and Language in Psychoanalysis."*** Trans. Allan Sheridan. Ecrits: A Selection. New York: W.W. Norton & Co. Uk:30-113.

Leech, G. na Short, M.(2007) ***Style in Fiction: A linguistic Introduction to English Fictional Prose*** (tol.2). Harlow: Longman.

Lidell, R. (1947) ***Some Principles of Fiction.*** London: Jonathan Cape.

Mathews, P.H. (1997) ***Oxford Concise Dictionary Of Linguistics***. Oxford: Oxford University Press.

Mbatiah, M. (2001) ***Kamusi ya Fasihi***. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Meyer, M. (2002) ***The Bedford Introduction to Literature.*** London: Bedford and Martins.

Mohamed, S.A. (1980) ***Utengano*** Nairobi: Longhorn

...........(1995) ***Kunga za Nathari ya Kiswahili: Tamthilia, Riwaya na Hadithi Fupi.*** Nairobi: East African Educational Publishers.

...........(1990) ***Tata za Asumini.*** Nairobi: Longman.

...........(2001) ***Babu Alipofufuka.*** Nairobi: Longhorn.

...........(2006) ***Dunia Yao*** Nairobi: Oxford University Press.

...........(2010) ***Nyuso za Mwanamke.*** Nairobi: Longhorn.

Njogu,K. na Chimerah, R. (1999) ***Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.*** Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nthenya, S. E. (2007) ***Uhakiki wa Haini Kama Riwaya ya Kihistoria.*** Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Okello, M. S.A. (1992) ***The Motifs of Dreams, Madness and Mimicry in Francis Imbuga's plays.*** Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Olali, T. (2010) "***Structure and Anti-structure of a Swahili New Novel: A Stylistic Analysis of Babu Alipofufuka***," in The Nairobi Journal of Literature. Na. 6 uk:81-98.

Peck, J. (1984) ***Literary Terms and Criticism: A Student's Guide***. Hampshire: Macmillan.

Rimmon-Kenan, S. (2002) ***Narrative Fiction: Contemporary Poetics*** (Tol. 2). London: Routledge

Roberts, E.V. na Jacobs, H.E. (1992) ***Literature: An Introduction to Reading and Writing*** (tol.3) New Jersey: Prentice Hall.

Shaw, H. (1972) ***A Dictionary of Literary Terms***. New York: MacGraw Hill.

Toolan, M. (1996) ***Language in Literature: An Introduction to Stylistics.*** London: Arnold.

Traore, F.A. (2008) "***Family and Society in Said Ahmed Mohamed's Novels***," in Swahili Forum Na. 15 uk: 63-72

TUKI (2004) ***Kamusi ya Kiswahili Sanifu.*** Nairobi: Oxford University Press.

Wafula, R.M. na Njogu, K. (2007) ***Nadharia ya Uhakiki wa Fasihi***. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. W.(2002) ***Bina-Adamu!*** Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

.........(2003a) ***Kichocheo cha Fasihi.*** Nairobi: Focus

.........(2003b) ***Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia***.Nairobi: Focus Publications Ltd.

.........(2004) ***Musaleo!*** Nairobi: Vide~Muwa.

.........(2008) ***Msingi wa Uchanganuzi wa Fasihi***. Nairobi: Vide- Muwa.

Wa Mutiso, K. (1996) ***Archetypal Motifs in Swahili Islamic Poetry: Kasida ya Burudai***. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.